

**MIKAKATI YA KUAFIKIA ULINGANIFU WA MAANA KATIKA TAFSIRI  
YA KIFASIHI: TATHMINI YA TAFSIRI ZA KAZI MBILI TEULE ZA  
BARBARA KIMENYE**

**JANEROSE I. KAMUNDI**


**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza  
Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya  
Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA  
SEPTEMBER, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

### Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada au stashahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi ..   
Janerose Igoki Kamundi  
AM12/11680/12

Tarehe... 13/09/2019

### Idhini

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi ..   
Prof. John M. Kobia  
Idara ya Fani  
Chuo Kikuu cha Chuka

Tarehe... 13/09/2019

Sahihi ..   
Dkt. Allan Mugambi  
Idara ya Fani  
Chuo Kikuu cha Chuka

Tarehe... 13/09/2019

## **HATILINZI**

©2019

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

## **TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa marehemu nyanyangu Elizabeth Mukwandiga M'Nkambi aliyenihimiza sana kuyapenda masomo hasa nilipokuwa mtoto mdogo. Mungu airehemu roho yake.

## **SHUKURANI**

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kila nilichohitaji ili kuikamilisha kazi hii. Bila wewe Baba nisingefika popote. Ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. John Kobia na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri wao ulionikwamua kila mara nilipoelekea kukwama katika kuiendeleza kazi hii. Siwezi kumsahau Bw. Enock Matundura aliyenifaa kwa kutenga muda wake kunielekeza na kunifafanulia mambo yaliyoelekea kunilemaza katika utafiti huu. Nasaha zako za mara kwa mara ziliniwezesha kuipa kazi hii mwelekeo bora.

Nitakuwa mchache wa shukurani nikimsahau Dkt. Mercy Njagi kwa kunihimiza kuendelea na kazi hii kila mambo yaliponiwia magumu. Wanafunzi wenzangu hasa Lucyline Njeri na Catherine Njeru, nawashukuru kwa kunitia moyo katika kipindi chote cha utafiti.

Siwezi kumsahau mume wangu Patrick Kamau na watoto wetu Mwenda Wangai na Amigo Munene waliokuwa nguzo wakati wote niliokuwa nikifanya utafiti huu. Kila nilipoonyesha dalili za kukata tamaa mlinihimiza kuendelea. Kwa kila aliyechangia kuifanikisha kazi hii ninasema, Asanteni sana.

## IKISIRI

Ulinganifu, usahihi pamoja na uwazi ni vipengee muhimu vya kuchunguzia kazi za fasihi tafsiri. Utafiti huu ulilenga kutafiti ulinganifu katika mtiririko wa kazi mbili teule za Kimenye (1968): *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost* zilizotafsiriwa ili kubainisha umuhimu wa kutumia mikakati mwafaka ya kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ili kupata tafsiri wasilifu. Utafiti huu ulijibu maswali kuhusu mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali mbalimbali ili kubainisha ulinganifu katika tafsiri za Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* na kuhusu ulinganifu na usahihi katika tafsiri za nomino za pekee katika tafsiri za *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo*. Katika kuyajibu maswali haya, mifano ilitolewa kutoka kwenye tafsiri za Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* na matini zake za Kiingereza za Kimenye (1968): *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost*. Msururu wa Musa ultieliwa kwa kuwa umeandikwa na mwandishi mmoja na kutafsiriwa na mtafsiri mmoja. Kwa hivyo kuna uthabiti kwa upande wa mwandishi na mtafsiri. Aidha, huu ndio msururu wa pekee kuwahi kutafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Sababu ya kuteua *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* ni kuwa kazi hizi zimesheheni tamathali za usemi na hivyo mtafiti alitazamia kupata data ya kutosha kuweza kuafikia madhumuni ya utafiti. Aidha kazi hizi hazijafanyiwa utafiti. Nadharia ya Ulinganifu ilitumiwa kuchunguza matini mbili za Kimenye (1968) zilizoteuliwa kama kielelezo. Utafiti huu ulifanyika maktabani. Data ilichanganuliwa kwa mbinu elezi kwani ilikuwa data ya nathari. Sampuli ilikuwa vitabu vinne vilivyoteuliwa kuwakilisha vingine: viwili vilivyoandikwa kwa Kiingereza na tafsiri zao za Kiswahili. Uteuzi huu ulifanywa kimakusudi kwa kuwa msururu mzima una wahusika walewale, mandhari haibadiliki ila matukio tu ndiyo tofauti. Vifaa vilivyotumika kukusanya data kutoka kwa sampuli vilikuwa matini mbili za Kimenye (1968): *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost* pamoja na tafsiri zao za Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo*. Utafiti huu uligundua kwamba mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi hutumiwa kimwingiliano ili kuweza kuhamisha ujumbe usio na dosari. Ilibainika pia kuwa mikakati inayotumika kutafsiri nomino za pekee kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili hutegemea mchango wa nomino husika katika matini. Matokeo ya utafiti huu yataifaidi taaluma ya fasihi tafsiri kwa kuwapa wasomi wa tafsiri mwongozo wa kurejelea watakapokuwa wakifanya tafiti zao. Vilevile matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa muhimu kwa watafsiri chipukizi kwa kuwapa mwongozo kuhusu mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi hasa istiari, tashbihi na nahau.

## ABSTRACT

Equivalence coupled with clarity are important aspects in evaluating literary translation work. This research study investigated meaning equivalence in the two selected books written by Kimenye (1968): *Moses in Trouble* and *Moses and the Ghost* and their Kiswahili translation by Matundura (2013): *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo*. The aim was to put into perspective the importance of adopting the appropriate translation strategies of translating figures of speech and proper nouns in order to achieve translation equivalence. The study tried to answer questions concerning the most used strategies in translating the figures of speech in order to achieve equivalence in the translations of Matundura (2013): *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo* and also concerning equivalence and clarity in the translations of proper nouns in *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo*. In answering these questions, examples were drawn from the translations by Matundura (2013): *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo* and their original English texts by Kimenye (1968): *Moses in Trouble* and *Moses and the Ghost*. Moses series was selected because the entire series is written by the same author and translated by the same translator and therefore there is consistency in terms of the author and translator. Moses series is the only series that has been translated from English to Kiswahili. The two books: *Moses in Trouble* and *Moses and the Ghost* together with their Kiswahili translations: *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo* were selected because the language used is rich in figures of speech which enabled the researcher to gather enough data to achieve the objectives of the study. Further, no research has been done on the two books. Equivalence theory was applied to investigate equivalence in the translations of the two selected texts. This study was carried out in the library. Descriptive analysis was employed in analyzing the data. The target population for the study was twenty two books: eleven original texts written in English by Kimenye (1968) and their Kiswahili translations by Matundura (2013). The sample population for this study was four books: two texts written in English by Kimenye (1968) and their Kiswahili translations by Matundura (2013). These books were selected purposefully because in the entire series the characters and the scene of the acts do not change from one text to another. It is only the episodes that are different. The instruments used to collect data from the sample were two books by Kimenye (1968), *Moses in Trouble* and *Moses and the Ghost* and their Kiswahili translations by Matundura (2013), *Musa Mashakani* and *Musa na Pepo*. This study established that no one translation strategy is sufficient to translate all the figures of speech. It was also established that to translate a proper noun effectively, the translator should start by establishing the role played by the noun in the original text. The research findings of this study will give insight to translation scholars doing research in translation equivalence issues. It will also provide additional information to the already existing knowledge on literary translation. Further, the findings will be useful by upcoming translators who will learn more suitable strategies for translating figures of speech such as idioms, metaphors and similes.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINI.....</b>	<b>ii</b>
<b>HATILINZI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vi</b>
<b>ABSTRACT.....</b>	<b>vii</b>
<b>YALIYOMO.....</b>	<b>viii</b>
<b>MAELEZO YA VIFUPISHO .....</b>	<b>xi</b>

<b>SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
---	----------

1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	3
1.3 Madhumuni ya Utafiti .....	4
1.4 Maswali ya Utafiti .....	4
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	4
1.6 Upeo wa Utafiti .....	4
1.7 Maelezo ya Istilahi .....	6

<b>SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI.....</b>	<b>7</b>
--	----------

2.1 Dhana ya Tafsiri .....	7
2.2 Utafiti Katika Taaluma ya Tafsiri ya Kiswahili .....	10
2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mikakati ya Kutafsiri.....	14
2.4 Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi .....	17
2.4.1 Mikakati ya Kutafsiri Nahau .....	18
2.4.2 Mikakati ya Kutafsiri Istiari .....	19
2.4.3 Mikakati ya Kutafsiri Tashbih.....	21
2.5 Mikakati ya Kutafsiri Nomino za Pekee .....	22
2.6 Misingi ya Kinadharia.....	23
2.7 Hitimisho.....	28

<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI .....</b>	<b>29</b>
---	-----------

3.1 Mpango wa Utafiti .....	29
3.2 Idadi Lengwa.....	29
3.3 Uteuzi wa Sampuli .....	29
3.4 Maadili katika Utafiti .....	30
3.5 Ukusanyaji wa Data .....	30
3.6 Uchanganuzi wa Data.....	30

<b>SURA YA NNE: MIKAKATI YA KUTAFSIRI TAMATHALI ZA USEMI KATIKA RIWAYA ZA MUSA NA PEPO NA MUSA MASHAKANI .....</b>	<b>32</b>
4.1 Muhtasari wa <i>Musa Mashakani</i> .....	32
4.2 Muhtasari wa <i>Musa na Pepo</i> .....	32
4.3 Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi .....	32
4.3.1 Mikakati ya Kutafsiri Nahau .....	33
4.3.2 Mkakati wa Kutumia Nahau Sawa Kimaana na Kileksia.....	33
4.3.3 Mkakati wa Kutumia Nahau Tofauti lakini yenyé Maana Sawa .....	38
4.3.4 Mkakati wa Kutafsiri Nahau kwa Ufafanuzi .....	42
4.3.5 Mkakati wa Kuifutilia mbali Nahau .....	51
4.4 Mikakati ya Kutafsiri Istiari .....	51
4.4.1 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Kuzihifadhi .....	52
4.4.2 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Istiari.....	58
4.4.3 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Kisawe cha Tashbihi .....	61
4.4.4 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Ufafanuzi .....	62
4.5.4 Mkakati wa Kuifutilia Mbali Istiari.....	70
4.5 Mikakati ya Kutafsiri Tashbihi .....	71
4.5.1 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Kuzihifadhi .....	71
4.5.2 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Dhana.....	79
4.5.3 Mkakati wa kutafsiri Tashbihi kwa Istiari .....	83
4.5.4 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Tashbihi yenyé maana sawa .....	84
4.6 Hitimisho.....	86
<b>SURA YA TANO: MIKAKATI YA KUTAFSIRI NOMINO ZA PEKEE KATIKA MUSA MASHAKANI NA MUSA NA PEPO.....</b>	<b>89</b>
5.1 Utangulizi .....	Error! Bookmark not defined.

5.2 Mkakati wa Kuhamisha Jina Moja kwa Moja.....	89
5.3 Mkakati wa Kulitohoa Jina .....	89
5.4 Mkakati wa Mwatiko wa Utamaduni .....	89
5.5 Mikakati Mingine .....	90
5.6 Hitimisho.....	97
<b>SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>98</b>
6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	98
6.2 Hitimisho.....	98
6.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi.....	99
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>100</b>
<b>KIAMBATISHO I: BARUA YA IDHINI.....</b>	<b>104</b>
<b>KIAMBATISHO II: CHETI CHA IDHINI .....</b>	<b>105</b>
<b>KIAMBATISHO III: IDADI YA MANENO .....</b>	<b>106</b>

## **MAELEZO YA VIFUPISHO**

<b>LC</b>	Lugha Chanzi
<b>LL</b>	Lugha Lengwa
<b>MC</b>	Matini Chanzi
<b>ML</b>	Matini Lengwa
<b>NP</b>	Nomino za Pekee
<b>TU</b>	Tamathali za Usemi

## **SURA YA KWANZA UTANGULIZI**

### **1.1 Usuli wa Mada**

Tafsiri daima imechukuliwa kuwa shughuli muhimu inayowapa wasomaji wasiofikia matini chanzi (tangu hapa MC) nafasi ya kuisoma. Hata hivyo, tafsiri imepata umaarufu zaidi katika Karne ya Ishirini kutokana na sababu kadha. Baadhi ya sababu hizi ni kama vile kuwepo na mahitaji ya mawasiliano na maelewano ya karibu kati ya mataifa pamoja na kuimarika kwa viwango vya elimu, uchumi na teknolojia. Katika miaka ya nyuma wataalamu wa fasihi, watu waliokuwa mashuhuri katika dini pamoja na wanafalsafa wamekuwa na maoni tofautitofauti kuhusu tafsiri. Maoni ya kila mmoja wao yalitokana na uzoefu wake kama mtu binafsi. Mada kuu katika majadiliano yao ilihusu suala la iwapo mtafsiri analazimika kuzingatia kwa uaminifu MC au kuwa huru. Tytler (1797), anasema kuwa tafsiri lazima izingatie kwa karibu sana maana katika MC. Anaongeza kuwa mtindo anaotumia mtafsiri pamoja na jinsi ya kuandika lazima iwe sawa na ile ya MC. Hata hivyo, kulingana na Barnwell (1986), mtafsiri akizingatia kwa karibu sana sarufi na maneno ya lugha chanzi (tangu hapa LC), tafsiri hiyo inaweza kukosa uasilia, ikawa tatanishi na inaweza kupotosha maana. Tafsiri ya kifasihi kwa hivyo haipaswi kuonekana kama tafsiri bali kama kazi asilia kwa kuwakutafsiri kazi ya kifasihi ni sawa na kuiandika upya (Venuti, 1998).

Tafsiri haitoeki katika ombwe tupu bali inatokea katika utamaduni na mazingira maalum. Mtafsiri anakuwa wakala anayefahamu barabara nafasi ya tafsiri katika utamaduni lengwa, mfumo wa fasihi, mitindo, kaida na vikwazo alivyowekewa na jamii. Mtafsiri bora hufahamu kwamba jumuia mbalimbali zina njia zao za kufikiria na kujieleza kutokana na ukweli kuwa kila jumuia ina tamaduni na miundo yake ya lugha.

Kila utamaduni una uwezo wa kukumbatia istilahi na mawazo mapya. Hata hivyo, kama hoja zote zilizo katika MC zitajumuishwa, nafasi kubwa zaidi itahitajika katika maandishi ya lugha lengwa (tangu hapa LL). Hii ndiyo sababu Catford (1965) anasema kuwa maana ni muhimu sana katika tafsiri. Aidha, anaendelea kusema kuwa tafsiri mara nyingi inafafanuliwa kwa kurejelea maana; kuwa tafsiri inayokubalika haina budi kuwasilisha maana sawa na ile ya MC. Maana ni sifa ya lugha na kwa hivyo lazima maandishi ya LC yawe na maana ya LC, nayo maandishi ya LL yawe na

maana ya LL. Hii ni kwa sababu vipengee vya LC na vile vya LL haviwezi kuwa na maana sawa kisarufi ila vinaweza kuwa na utendakazi sawa katika mazingira sawa. Ni muhimu kutaja kuwa tafsiri iliyo sahihi si ile inayozingatia kwa karibu sana muundo wa LC lakini ni ile inayowasilisha maana ya MC kwa usahihi iwezekanavyo (Barnwell, 1986).

Kwa mujibu wa Mollanazar (2001), kuna matumizi ya kiasili ya miundo ya kiisimu ambayo hutokea kwa kawaida kwa wasemaji asili wa kila lugha. Hii ndiyo sababu mtafsiri anapaswa kujiuliza swali: Je, hii ndiyo lugha inayotumiwa na wazungumzaji wa LL? Mtafsiri asipokuwa mwangalifu anaweza kuhamisha kwa njia ya moja kwa moja vishazi vya LC na kwa hivyo akawasilisha ujumbe potovu. Mtafsiri kwa hivyo analazimika kutafuta kwa ufundi vishazi na nahau asili katika LL. Ukiukaji wa ulinganifu husababisha tafsiri kupotosha maana na kazi yenye kuuonekana chapwa. Hata hivyo, lugha daima inabadilika na kuchukua mambo mapya na mengine ya kigeni. Hoja hapa ni kwamba lugha ina kiwango cha uvumilivu katika kukubali na kujitwalia mambo ya kigeni. Mara nyingi watafsiri hukosolewa kwa kukiuka vizingiti hivi lakini, iwapo watafanya kazi bila kukiuka mipaka yao wanapongezwa kwa kuwa wabunifu na kupanua uwezo wa lugha.

Kuhusu nadharia ya tafsiri katika fasihi, Nida (1964) anafafanua tafsiri kwa msingi wa ulinganifu. Anaeleza tafsiri kama ulinganifu asili wa karibu sana na ujumbe katika lugha asilia (Mollanazar, 2001). Kwa hivyo, ulinganifu unahusu tafsiri inayolenga maana. Aidha, katika kuchangia kuhusu ulinganifu, Nida na Taber (1969) wanasisitiza kwamba tafsiri bora haipaswi kuonekana kama tafsiri. Mtafsiri huwa mtunzi mwenza wa mwandishi anayehakikisha tafsiri linganifu. Jukumu la mtafsiri ni kudhahirisha katika lugha tofauti na LC yaliyomo katika MC. Utafiti huu ulichunguza ubunifu wa mtafsiri katika kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee katika kazi husika ili kutoa tafsiri wasilifu.

Lugha na utamaduni ni mambo mawili ambayo hayawesi kutenganishwa. Kulingana na Lyons (1977), lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni na kwamba tofauti za kileksia zinazotokana na kila lugha zitaonyesha sifa muhimu (za kitamaduni) za vitu, taasisi na shughuli katika jamii lugha ambapo lugha hii inatumika. Newmark (2001) anaendelea kusema kuwa utamaduni ni mwenendo wa maisha na hujidhirisha kwa

njia ya kipekee kwa jamii ambayo inatumia lugha fulani kama njia ya kujieleza. Kulingana na maoni ya Newmark, ikiwa mtafsiri atachukua visawe katika LL, tafsiri hiyo inaweza kukosa ulinganifu na kuwa potovu.

Kwa kuwa tafsiri inalenga kufafanua kazi ngeni, unapotafsiri maandishi ya kigeni, unatambulisha utamaduni wake pia. Mabadiliko ya baadhi ya taswira zinazowakilisha utamaduni yatapunguza wajibu wa kitamaduni wa lugha hiyo na kuacha kazi ya kutambulisha utamaduni kupitia tafsiri hiyo bila kukamilika. Haikubaliki, kwa hivyo, kutumia mifano ya moja kwa moja ya elementi kutoka kwa utamaduni lengwa badala ya elementi za utamaduni wa MC; inakubalika kuhifadhi kiasi fulani cha ugeni (Dayan, 2012). Utafiti huu uliangazia jinsi ambavyo mambo yaliyodokezwa katika MC yalivyotafsiriwa ili kuhakikisha tafsiri linganifu.

Binadamu huwa na sifa za kimtzamo na kimwitikio ambazo hujitokeza wanapozungumza na ambazo zinaweza kunaswa na kutafsiriwa. Kulingana na Dayan (2012), uwezo wa mpokeaji kuiga kiasi fulani cha ugeni katika tafsiri unakubalika, hasa wakati istilahi mpya zinapotambulishwa katika hatua ya awali katika mawasiliano ya kitamaduni. Kwa jumla, tafsiri kuonekana asili kwa mpokeaji ni sawa, ingawa kuhifadhi ugeni kwa kiasi fulani pia kunaruhusiwa. Katika hali hii, ingawa elementi za kitamaduni kutoka lugha asilia lazima zihifadhiwe, inahalisi tafsiri isomeke kama tafsiri.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Ingawa tahakiki za tafsiri kadha zimefanywa katika lugha mbalimbali, taaluma ya tafsiri ya Kiswahili haijakuwa na msururu wowote wa tafsiri ya kifasihi ambao umehakikiwa kwa mkabala wa mikakati ya uafikiaji wa ulinganifu wa maana. Aidha, wataalamu mbalimbali wameshughulikia tafsiri katika mikabala ya tafsiri mbaya na athari yake kwa mawasiliano, wajibu wa mtafsiri kwa tafsiri, suala la ukiushi katika tafsiri, tofauti za kilugha katika tafsiri na uundaji wa nadharia katika tafsiri. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umeshughulikia suala la ulinganifu wa maana katika tafsiri kuhusu msururu wa kazi za kifasihi. Suala ambalo ni kiini cha utafiti huu.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kufafanua mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi ili kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri za kifasihi za *Musa Mashakani* (2013) na *Musa na Pepo* (2013).
2. Kutathmini ulinganifu wa maana katika tafsiri za nomino za pekee katika *Musa Mashakani* (2013) na *Musa na Pepo* (2013).

### **1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Mtafsiri alitumia mikakati ipi kutafsiri tamathali za usemi katika kuhakikisha ulinganifu wa maana katika tafsiri za *Musa Mashakani* (2013) na *Musa na Pepo* (2013)?
2. Ni mikakati gani aliyotumia mtafsiri ili kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri za nomino za pekee katika *Musa Mashakani* (2013) na *Musa na Pepo* (2013)?

### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha wasomi wa somo la fasihi tafsiri kwa kuwapa mwongozo wa kurejelea watakapokuwa wakichunguza masuala kuhusu fasihi tafsiri. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatawapa changamoto watafsiri wa matini za kifasihi kuwa waangalifu zaidi wanapotafsiri matini. Matokeo ya uchunguzi huu pia yatakuwa yenye manufaa kwa watafsiri chipukizi kwa kuwaelekeza kuhusu mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi hasa istiari, nahau na tashbihi.

### **1.6 Upeo wa Utafiti**

Mwandishi Barbara Kimenye ametunga vitabu kumi na vitatu katika msururu wa Moses Series. Kati ya vitabu hivi, kumi na kimoja (11) vilichapishwa na Oxford University Press na viwili vikachapishwa na Macmillan Publishers. Hata hivyo idadi iliyotafsiriwa ni vitabu kumi na kimoja ambavyo vimechapishwa na Oxford University Press. Kwa hivyo tafsiri za vitabu viwili vya Kimenye (1968): *Musa Mashakani* (2013) na *Musa na Pepo* (2013) viliteuliwa. Mikakati iliyotumiwa kutafsiri nomino za pekee (tangu hapa NP) na tamathali za usemi (tangu hapa TU) ilichunguzwa. Tamathali za usemi zilizoshughulikiwa ni pamoja na istiari, nahau na

tashbihi. Msururu wa Moses Series umeteuliwa kwa kuwa huu ndio msururu mrefu zaidi ambao umeandikwa na mwandishi mmoja: Kimenye (1968) na kutafsiriwa na mtafsiri mmoja kwa lugha ya Kiswahili. Kazi za Kimenye: *Moses in Trouble* (1968) na *Moses and the Ghost* (1968) pamoja na tafsiri zao: *Musa Mashakani* (Matundura, 2013) na *Musa na Pepo* (Matundura, 2013) ziliteuliwa kwa misingi kuwa zimesheheni TU na NP za kutosha kumpa mtafiti data yote anayohitaji kwa kusudi la kazi hii. Aidha, katika vitabu vyote wahusika ni wale wale, mandhari ni ile ile ila matukio ni tofauti. Kwa hivyo vitabu *Moses and the Ghost* (1968) na *Moses in Trouble* (1968) na tafsiri zao: *Musa na Pepo* (2013) na *Musa Mashakani* viliteuliwa kimakusudi kwani kuufanya msururu wote utafiti kungehitaji muda mrefu zaidi.

## **1.7 Maelezo ya Istilahi**

Istilahi zifuatazo zimetumiwa katika utafiti huu:

- Tafsiri:** Mchakato wa kuhamisha yaliyoandikwa katika lugha moja hadi nyingine kwa njia ambayo itawasilisha ujumbe uliokusudiwa na LC.
- Tafsiri Sisisi:** Tafsiri ya moja kwa moja
- Mikakati ya kutafsiri:** Mbinu anazotumia mtafsiri kukabiliana na changamoto ambazo anakumbana nazo anapotafsiri matini au sehemu ya matini.
- Ulinganifu wa maana:** Uwiano wa maana baina ya MC na ML.
- Lugha Chanzi:** Lugha ambayo imetumika katika kuandika matini ambazo tafsiri zake zinachunguzwa katika utafiti huu.
- Lugha Lengwa:** Lugha ambayo imetumika katika kuandika matini tafsiri.
- Matini Chanzi:** Matini ambazo tafsiri zao zinachunguzwa.
- Matini Lengwa:** Matini zinazoafikiwa kutokana na kutafsiri matini chanzi.
- Mwatiko wa Utamaduni:** Mkakati wa kutafsiri nomino za pekee ambapo majina katika LC yanabadilishwa na majina ya kiasili ya LL ambayo yanadokeza hali zinazolingana katika tamaduni husika.

## **SURA YA PILI**

### **MWAUO WA MAANDISHI**

#### **2.1 Dhana ya Tafsiri**

Wataalamu mbalimbali wamefafanua maana ya tafsiri. Baadhi ya wataalamu kama vile Belloc (1931), Catford (1965), Nida na Taber (1969), Bell (1991) na Gutt (1999) wanasisitiza maana na muundo na aidha kutilia mkazo umuhimu wa ulinganifu katika tafsiri. Wataalamu hawa wanafafanua tafsiri kama mchakato wa kuhamisha lugha moja hadi nyingine kwa namna ambavyo LL itawasilisha ujumbe uliokusudiwa na LC. Hawa wana maoni kuwa tafsiri bora haipaswi kuonekana kama tafsiri.

Kulingana na Belloc (1931), ili kupata tafsiri bora ni lazima mtafsiri afanye uamuzi makusudi kuzingatia maana ya maandishi ya awali. Kwa hivyo inamlazimu mtafsiri kuunda upya wala sio kufanya tafsiri ya moja kwa moja. Belloc anashauri kuwa kuna lazima ya mtafsiri kujikomboa kutokana na masharti mbalimbali kama vile mwandishi alivyojikomboa alipokuwa akiandika MC. Kulingana na maoni haya ya Belloc, ubunifu wa mtafsiri ni muhimu ili kuweza kuafikia tafsiri wasilifu. Kwa kuzingatia maoni haya ya Belloc, utafiti huu ulichunguza ubunifu wa mtafsiri katika kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ili kupata tafsiri linganifu.

Tafsiri inatarajiwa kwa kawaida kutoa kwa uaminifu sifa zote muhimu za MC (Nida na Taber, 1969). Hata hivyo haimaanishi hapa kwamba tafsiri iwe sawasawa na MC bali iwe na ulinganifu wa kiwango fulani. Hii, kwa mujibu wa House (1977), inatokana na ukweli kwamba lugha zinatofautiana. Baadhi ya wanaisimu pamoja na wahakiki wa fasihi, wanachukulia kwamba dhana ya uaminifu inaweza kuhusishwa na ulinganifu. Hapa, ulinganifu unamaanisha upeo wa juu iwezekanavyo wa uwiano baina ya MC na ML bali si usawa.

Gutt (1999) anasema kuwa tafsiri iliyo bora haipaswi kuonekana kama tafsiri bali inapaswa kusomeka kama maandishi ya awali ya LL. Anasema kuwa tafsiri haipaswi kuonyesha ugeni wowote au hata kuonekana kama tafsiri. Aidha, anasema kwamba ili tafsiri iweze kukubalika au kufaa mtafsiri anapaswa kuzingatia miundo iliyo asili ya LL. Maoni haya ya Gutt yalichangia katika utafiti huu kwa kuwa yalimwongoza mtafiti katika kuchunguza tafsiri za tamathali mbalimbali ili kubainisha ulinganifu katika tafsiri hizo. Mtafiti alichunguza iwapo tafsiri za tamathali mbalimbali pamoja

na nomino za pekee zinawasilisha maana ya MC kwa msomaji wa ML kwa lugha isiyoonyesha ugeni kwake.

Kazi zinazoonyesha ugeni katika maisha ya wasomaji huwatatanisha na ujumbe uliokusudiwa na mtunzi wa MC hukosa kuwafikia kwa namna aliyokusudia. Kazi kuu katika utekelezaji wa tafsiri kwa hivyo ni kuwasilisha maana ya MC katika LL. Kulingana na Nyangeri (2014), katika mchakato wa kutafsiri, mtafsiri huibua tendo jipya la mawasiliano kutoka lile lililoko. Mtafsiri kwa hivyo hutoa matini mbalimbali katika lugha nyinginezo na kwa hivyo kupanua idadi ya wasomaji.

Larson (1984) kwa mfano anasema kuwa tafsiri inapaswa kuwasilisha maana ile ile iliyowasilishwa kwa mzungumzaji wa LC kwa kuzingatia muundo wa kawaida wa LL. Kwa mujibu wa Larson (1984), inamlazimu mtafsiri kukiuka miundo ya LC na kuzingatia ile ya LL bila kupotosha maana. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kwamba lengo la mtafsiri linapaswa kuwa kuandika katika LL tafsiri iliyo na maana sawa na maandishi ya LC yakiwa yameelezwa kwa kuzingatia fani ya LL. Newmark (1988) anasema kwamba kutafsiri ni kuandika MC katika sarufi, nahau na maneno ya LL. Anaendelea kusema kwamba kutafsiri ni kufafanua maana ya matini katika lugha nyingine kwa njia aliyokusudia mwandishi wa maandishi ya awali. Kwa jumla, tafsiri ni mchakato wa kufafanua maana, mawazo au ujumbe wa matini kutoka lugha moja hadi nyingine. Mchakato wa kutafsiri huongozwa na mambo kama vile usahihi na ulinganifu kulingana na maana, mawazo au ujumbe katika tafsiri. Newmark (1988) anaendelea kusema kuwa tafsiri hueleza kwa uaminifu maana ya MC kulingana na muktadha wake kutegemea miundo ya kisarufi ya LL. Fafanuzi hizi zinasisitiza kwamba ulinganifu una umuhimu mkubwa katika tafsiri yenyе kuwasilisha maana kwa msomaji lengwa.

Kimsingi, kulingana na As-Safi (1997), tafsiri ni aina ya mawasiliano. Kwa sababu hii, kazi ya kimsingi katika shughuli ya kutafsiri ni kupata ulinganifu kati ya MC na ML. Hii ni kwa kuwa ulinganifu ni kipengee muhimu sana katika kufanikisha mawasiliano katika tafsiri. Ulinganifu ndio unaohusisha MC na ML; bila ulinganifu wa kiwango fulani matini tafsiri haiwezi kuchukuliwa kuwa tafsiri ya MC (Zhongde, 1991). Katika utafiti huu mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi pamoja na

nomino za pekee katika tafsiri husika ilichunguzwa ili kubainisha ufaafu wa mikakati hiyo katika kufanikisha ulinganifu kati ya MC na ML.

Larson (2001), akifafanua tafsiri bora, anasema kuwa matini iliyotafsiriwa lazima iwapashe ujumbe hadhira lengwa watakaoitumia. Hapa Larson ana maana kuwa mtafsiri hana budi kuufikisha ujumbe wa MC kwa hadhira lengwa. Larson anaendelea kusema kuwa katika tafsiri bora, miundo ya lugha iliyotumiwa haina budi kuwa ile inayowezesha ujumbe wa ML kueleweka kwa urahisi sawa na jinsi MC yalivyokuwa rahisi kueleweka na wasomaji wake.

Uchunguzi wa Williams (2005) unaonyesha umuhimu wa utamaduni katika tafsiri. Uchunguzi huu unadhihirisha kwamba kutokuwa na ujuzi wa utamaduni kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya lugha au kupotosha maana; jambo ambalo huathiri vibaya tafsiri yenyewe. Utafiti wa Williams' una uhusiano na utafiti huu kwa kuwa katika utafiti huu mtafiti alichunguza kama kulikuwa na mgongano wa kitamaduni uliosababisha kupotoka kwa maana hasa kutokana na namna tamathali mbalimbali pamoja na nomino za pekee zilivyotafsiriwa.

Kuna mtindo wa tafsiri zote nzuri kuwa ndefu kuliko maandishi ya awali. Hii haina maana kwamba tafsiri zote nzuri ni lazima ziwe ndefu. Inamaanisha kwamba katika mchakato wa kuhamisha kutoka muundo mmoja wa lugha na utamaduni hadi mwingine, kurefuka kwa tafsiri ni jambo lisiloweza kuepukika. Mtindo huu wa urefu mkubwa, kulingana na Nida na Taber (1969), hutokana na ukweli kwamba mtafsiri hulazimika kueleza kila kitu kilicho katika mawasiliano ya awali. Pia analazimika kuweka wazi kwa lugha pokezi kile ambacho si dhahiri katika maandishi ya lugha ya awali. Hii ni kwa sababu inaaminiwa kuwa wapokeaji asili wa mawasiliano haya walikuwa na usuli uliohitajika kuelewa yaliyomo katika ujumbe. Hivyo, kama mtafsiri analazimika kudhihirisha katika LL kuliko katika lugha asilia, kurefuka kwa tafsiri hakutaepukika.

Kwa jumla, kwa kuwa tafsiri ni aina ya mawasiliano, ni muhimu mawasiliano haya yakamfikia msomaji wa ML kwa njia iliyo asili kwake. Wataalamu wote ambao wametajwa hapo juu wameonyesha kwamba ulinganifu ni muhimu katika tafsiri

yooyote inayokusudiwa kuwasiliana na msomaji. Tafsiri inapokosa ulinganifu wa kiasi fulani na MC basi tafsiri hiyo haifai kuitwa tafsiri ya MC. Katika kusisitiza umuhimu wa ulinganifu katika tafsiri Catford (1965) anasema kuwa ulinganifu ndilo tatizo la kimsingi linalopaswa kushughulikiwa katika tafsiri.

## **2.2 Utafiti Katika Taaluma ya Tafsiri ya Kiswahili**

Ali (1981) alishughulikia tafsiri za taarifa za habari kutoka Kiingereza hadi Kiswahili katika kituo cha redio cha *Sauti ya Kenya* (sasa KBC) ambapo alishughulikia baadhi ya matatizo ambayo hutokea katika taarifa za habari zilizotafsiriwa. Aligundua kuwa tafsiri mbaya ya taarifa hizi iliathiri vibaya mawasiliano kati ya watangazaji na wasikilizaji. Kulingana na Ali, tafsiri hizi mbaya hutokana na watafsiri wasiokuwa na ujuzi na pia muda mfupi unaotumika kuziandika na kuzitafsiri habari hizi.

Utafiti wa Omboga (1986) ulichunguza matatizo yanayokumba tafsiri ya maandishi ya kifasihi katika Kiswahili. Alikusudia kuangazia matatizo na athari za tafsiri kutokana na udhaifu na hali duni ya kazi za tafsiri. Omboga (1986) aliangazia tafsiri ya riwaya *Wema Hawajazaliwa* ya Ayi Kwei Armah. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, tafsiri kama hii isiyo kamilifu hutokana na kutokuwa na msingi bora wa kinadharia, mtafsiri kutoelewa wajibu wake vizuri na aidha mtafsiri kutoelewa tamaduni za lugha mbili zilizohusika. Hii ilisababisha kutafsiri lugha peke yake na kupuuza vipengele vingine kama vile muktadha na utamaduni. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa tafsiri nyingi zina makosa yaliyo dhahiri na kwa hivyo zinaweza kutatiza uwasilifu katika tafsiri. Uchunguzi wa Omboga ulichangia utafiti huu kwa kuwa, kuwa na msingi bora wa kinadharia, mtafsiri kuelewa wajibu wake vizuri na mtafsiri kuelewa tamaduni za lugha zinazohusika ni baadhi ya mambo yanayochangia ulinganifu katika tafsiri – jambo ambalo lilishughulikiwa katika utafiti huu.

Mutahi (1987) amechunguza matatizo ya kutafsiri kutoka lugha ya Gikuyu hadi Kiingereza. Mutahi (1987) alitafiti tafsiri ya shairi *Gicandi*. Anasema kuwa tafsiri hiyo haikufanikiwa kwa sababu ya mtafsiri kutofahamu vizuri utamaduni na sheria za kisarufi za lugha ya Gikuyu. Utafiti huu ulinufaika kutokana na uchunguzi wa mtaalamu huyu kwa kuwa ulinganifu katika tafsiri za Matundura (2013) haungeweza

kuafikiwa bila ya mtafsiri kuwa na ujuzi wa utamaduni na kanuni za kisarufi za lugha za Kiingereza na Kiswahili.

Uchunguzi wa Shitemi (1990) ulishughulikia mawasiliano katika tafsiri ambapo anasema kuwa matumizi ya dhana za kigeni katika MC ni baadhi ya mambo yanayosababisha tafsiri pungufu. Katika utafiti wake anafafanua sifa mojawapo ya tafsiri nzuri kuwa uwezo wa tafsiri hiyo kudhihirisha maana inayopatikana kwenye MC. Uchunguzi wa Shitemi unahusiana na utafiti huu kwa kuwa kipengele cha mawasiliano ndicho kinacholengwa na matumizi ya lugha kisanaa katika matumizi ya tamathali za usemi na nomino za pekee wakati wa kutafsiri. Utafiti huu ulichunguza namna tamathali za usemi na nomino za pekee zilivyotafsiriwa na aidha kutathmini ufanisi wa tafsiri hizo katika kuwasilisha ujumbe wa MC kwa walengwa.

Namulungu (1999) alichunguza suala la ukiushi katika tafsiri. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa ukiushi ni mbinu inayotumiwa na mtafsiri katika tafsiri. Utafiti wake unaonyesha kuwa ukiushi hudhihirika katika kazi za tafsiri kama njia ya kukabiliana na changamoto katika tafsiri. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa ukiushi hubainika katika tafsiri kwa kuwa lugha hutofautiana kwa njia mbalimbali. Anaeleza kuwa ukiushi humfanya mtafsiri kutumia lugha kwa njia inayoonyesha hali ya kukiuka matumizi ya lugha kwa njia ya kawaida ili ujumbe wa MC uweze kuhamishwa kikamilifu. Utafiti wa Namulungu ulikuwa wenyе manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa ulichunguza jinsi mtafsiri alivyohamisha ujumbe kikamilifu kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili kwa njia iliyo asili kwa msomaji wa Kiswahili; jambo ambalo lilishughulikiwa na uchunguzi huu.

Uchunguzi uliofanywa na Wangia (2003) kuhusu makosa katika tafsiri ya Biblia ya Kilulogooli ya 1951 kutoka Kiingereza unadhihirisha kuwa kuna upungufu mwangi unaojitokeza katika tafsiri hii ambaо unapotosha ujumbe na maana ya MC. Kulingana na Wangia, matatizo haya yanatokana na tofauti kati ya lugha hizi mbili zilizotumiwa: Kiingereza na Kilulogooli katika upande wa muundo. Lugha zinazohusika katika utafiti huu: Kiswahili na Kiingereza zinatofautiana sana kimuundo. Utafiti wa Wangia ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa uchunguzi huu ulichunguza jinsi tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili zilivyoshughulikiwa ili kutoa tafsiri linganifu.

Utafiti wa Muigai (2005) umechunguza ubunifu wa mtafsiri katika tafsiri ya tamthilia ya *Masaibu ya Ndugu Jero*. Alilenga kubainisha jinsi mtafsiri alivyotumia lugha kiubunifu kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe kwa walengwa. Kwa mujibu wa Muigai, ingawa ubunifu wa mtafsiri huchukuliwa kama upotovu katika tafsiri wakati mwingine mtafsiri hutumia maneno tofauti kimakusudi kwa kuzingatia hadhira yake. Uchunguzi wa Muigai (2005) ulinufaisha utafiti huu kwa kuwa ubunifu wa mtafsiri hasa katika kutafsiri tamathali mbalimbali ulichunguzwa kwa kuwa ubunifu wake unafaa ili kutoa tafsiri wasilifu katika LL.

Omboga (2006) ametafiti kuhusu uundaji wa nadharia ya tafsiri ya matini za fasihi, kwa kuonyesha jinsi tafiti zimezingatia kubainisha makosa ya tafsiri bila kujihusisha na kutafuta njia mwafaka za kutafsiri. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya mwitikio wa msomaji. Anasema katika utafiti wake kuwa ni ukweli usioweza kukanushika kuwa kila wakati MC ikilinganishwa na ML hiyo ML hupotoka kimakusudi au hata bila kukusudia. Aligundua kuwa upotovu wa kimakusudi ni mbinu ambayo mtafsiri hutumia kwa nia ya kuwasilisha ujumbe wake kwa walengwa. Utafiti wa Omboga unahusiana na aidha kutofautiana na utafiti huu. Unahusiana kwa kuwa matumizi ya mikakati mwafaka ya kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ni njia moja ambayo mtafsiri anaweza kufanya upotovu wa kimakusudi ili aweze kuwasilisha ujumbe. Unatofautiana kwa kuwa Omboga (2006) alichunguza uundaji wa nadharia ya tafsiri nao utafiti huu unashughulikia mikakati ya kuafikia ulinganifu katika tafsiri za kifasihi. Utafiti wa Omboga ulichangia utafiti huu kwa kuwa katika kutathmini mikakati ya kuafikia ulinganifu katika tafsiri za tamathali za usemi na nomino za pekee, matumizi ya upotovu kama mbinu ya mkakati wa kutafsiri yatabainishwa.

Uchunguzi wa Ondara (2010) ulilenga kuchunguza ufaafu wa maana katika tafsiri ya nyimbo za dini. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa maana asilia ya nyimbo hupotoka katika tafsiri. Ondara alibainisha kuwa mtafsiri hakuzingatia tafsiri ya tamathali za usemi zilizotumiwa bali alijaribu kuzikwepa na hivyo basi maana asilia haikuwasilishwa kikamilifu. Utafiti wa Ondara unaonyesha kuwa kupotoka kwa nyimbo tafsiri kunachangiwa na kuepa kutafsiri tamathali za usemi. Utafiti wa Ondara

(2010) ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa matumizi ya mikakati mwafaka kutafsiri tamathali za usemi ili kuafikia ulinganifu yalichunguzwa.

Nyangeri (2014) alishughulikia vitendo usemi na ulinganifu wa maana katika tafsiri. Alilenga kubainisha jinsi nadharia ya vitendo usemi hufanikisha uibushi wa maana na hivyo kuchangia kusuluhisha matatizo ya ulinganifu katika tafsiri. Alikita uchunguzi wake katika kazi mbili za Barbara Kimenye: *Moses and the Kidnappers* na *Moses and the School Farm* na tafsiri zake za Kiswahili *Musa na Watekanyara* na *Musa na Shamba la Shule*. Matokeo ya uchunguzi wake yalibainisha kuwa tatizo la ulinganifu wa maana lipo na haliwezi kupuuzwa. Kwa mujibu wa Nyangeri (2014), tatizo hili limechochewa na ukosefu wa uelewa wa nia ya mtunzi pamoja na udhaifu wa ala zilizopo za kutumia kuitambua nia yenyewe. Utafiti wa Nyangeri unahusiana na uchunguzi huu kwa baadhi ya vitendo usemi kama vile misemo, istiari na tashbihi ambavyo amevishughulikia pia ni tamathali za usemi ambazo utafiti huu ulichunguza mikakati iliyotumiwa kuzitafsiri ili kuafikia ulinganifu. Utafiti wa Nyangeri na utafiti huu zinatoa mifano kutoka kwa msururu Musa ulioandikwa na Kimenye ila kazi zinazotumika katika tafiti hizi mbili ni tofauti. Uchunguzi huu ni tofauti na uchunguzi wa Nyangeri kwa kuwa Nyangeri alichunguza jinsi nadharia ya vitendo usemi hufanikisha uibushi wa maana nao utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya kuafikia ulinganifu katika tafsiri za kifasihi.

Nzyoka (2014) alichunguza tafsiri na mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi katika tamthilia ya Antigoni. Alilenga kutathmini tafsiri na mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi katika uwasilishaji wa ujumbe kwa walengwa. Utafiti wake uligundua kwamba kuna haja ya kutumia mbinu, mikakati na taratibu mseto katika kutafsiri ili ujumbe uweze kuwasilishwa kwa walengwa ipasavyo. Alibainisha kwamba kuna mikakati inayoweza kutafsiri tamathali za usemi kwa njia wasilifu kuliko mingine. Aidha, aligundua kuwa kuna mikakati ambayo inaweza kuhamisha ujumbe wenye dosari. Uchunguzi wa Nzyoka ulichangia utafiti huu kwa kuwa umeshughulikia mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi; kipengee kilichoshughulikiwa na utafiti huu isipokuwa utafiti huu ulinua kuchunguza ufaafu wa mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ili kuafikia ulinganifu katika tafsiri. Vilevile kazi zilizorejelewa ni tofauti.

### **2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mikakati ya Kutafsiri**

Kulingana na Culler (1976), tatizo kubwa katika kutafsiri ni tofauti iliyopo baina ya lugha moja na nyingine. Ugumu katika kuwasilisha ujumbe kutoka LC hadi LL hulingana na ukubwa wa tofauti baina ya lugha hizi mbili. Mwachano wa kitamaduni pia huchangia ugumu huu. Kwa hivyo, inambidi mtafsiri kuwa na uelewa wa lugha na tamaduni husika ili aweze kuandika tafsiri linganifu. Katika tafsiri ya kifasihi, mtafsiri analazimika kutia maanani sanaa ya lugha (Bassnet, 1988). Hii ni kutohana na sababu kuwa tafsiri ya kifasihi ni mawasiliano ya kisanii baina ya mtunzi, mtafsiri na msomaji lengwa. Kwa hivyo katika mchakato wa kutafsiri, jambo la kimsingi ni uteuzi wa maneno na mikakati mwafaka ya kutafsiri matini. Katika uteuzi huu wa maneno, kuna mikakati ya kutafsiri ambayo humwongoza mtafsiri ili kuunda tafsiri yenye ulinganifu.

Kwa mujibu wa Nida (1943), lugha mbalimbali huwa na miundo tofauti na pia huwa na kaida pamoja na istilahi mbalimbali ambazo ni tofauti na zile za lugha nyingine. Tofauti hizi na nyinginezo huwa changamoto kubwa kwa mtafsiri katika mchakato wa kutafsiri. Mtafsiri kwa hivyo analazimika kutumia mikakati mwafaka ya kutafsiri ili kuweza kuafikia ulinganifu wa maana. Utafiti huu ulichunguza mikakati inayotumiwa ili kuafikia ulinganifu wa maana katika maandishi yaliyotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Nida (1964) anaeleza mikakati ya kutafsiri kama njia anazotumia mtafsiri kushughulikia matatizo ya kutafsiri. Krings (1986) anafafanua mkakati wa kutafsiri kama mpango makusudi wa mtafsiri wa kutatua matatizo mazito ya kutafsiri katika mzingiro wa kazi nzito ya kutafsiri. Anaendelea kusema kuwa mikakati ya kutafsiri ni utaratibu ambao huwa hakikisho la ufanisi mkubwa inapotumiwa kwa mpangilio bora na mtafsiri. Loescher (1991) anaona mkakati wa kutafsiri kuwa mbinu makusudi inayotumiwa kusuluuhisha tatizo analokumbana nalo mtafsiri anapotafsiri matini kutoka lugha moja hadi nyingine. Baker (2005) anaendeleza mawazo haya kwa kusema kuwa mkakati wa kutafsiri ni mbinu ya kutatua tatizo ambalo linamkabili mtafsiri anapotafsiri matini fulani.

Newmark (1988) anafafanua aina mbili za mikakati ya kutafsiri: mbinu za kutafsiri ambazo zinaitwa na baadhi ya watafsiri mikakati ya jumla na taratibu za kutafsiri zinazoitwa na baadhi ya watafsiri mikakati maalum. Anaeleza kuwa mbinu za kutafsiri zinahusu matini nzima nazo taratibu za kutafsiri zinatumika kwa sentensi na vipengee vidogo vya lugha. Umuhimu wa mikakati ya kutafsiri ni kuafikia upeo wa ulinganifu. Baadhi ya mikakati ya kutafsiri inayofafanuliwa na Newmark ni pamoja na tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kiuaminifu, tafsiri ya kisemantiki, tafsiri ya kimawasiliano, tafsiri ya kiutohozi na tafsiri ya kinahau.

Mahmoud (2007) anaeleza aina mbili kuu za mikakati ya kutafsiri: mikakati ya kutafsiri moja kwa moja na tafsiri isiyo wazi. Mikakati ya kutafsiri moja kwa moja inajumlisha ukopaji, kaloki na tafsiri sisisi. Ukopaji unahu kuhamisha neno au mafungu ya maneno moja kwa moja kutoka LC hadi LL (Munday, 2001). Mafungu ya maneno au maneno yaliyokopwa huwa na ushabaha wa kiuamilifu, jambo ambalo hutokea kwa kuwa maana za kimuktadha zinaweza kuafiki utamaduni wa LL. Matumizi ya mkakati huu ni njia bora ya kuleta utamaduni mpya katika LL. Mkakati huu hufanikisha kuleta maana asilia ya ujumbe katika LL. Kaloki ni mkakati wa kukopa kishazi au muundo wa LC kisha kuhamisha kwa tafsiri sisisi. Faida moja ya mkakati huu ni kuwa mtafsiri anaweza kuwasilisha anachomaanisha au anachodokeza msemaji tofauti na anachosema. Tafsiri sisisi inahu kuhamisha neno moja kwa moja kutoka lugha moja hadi nyingine. Mkakati huu unatumika sana pale ambapo lugha za familia moja na utamaduni mmoja zinahusika.

Tafsiri isiyo wazi inajumlisha ubadilishaji, urekebishaji, ulinganifu na utohozi. Ubadilishaji unahu mtafsiri kutumia maneno ya kategoria tofauti na maneno ya MC bila kupotosha ujumbe (Munday, 2001). Kwa mfano MC inaweza kutumia kivumishi nayo ML ichukue kisawe cha kielezi ili kuwasilisha ujumbe wa MC.

Urekebishaji unahu kugeuza umbo la ujumbe kwa kubadili mtazamo. Kwa mujibu wa Newmark (1982), urekebishaji humpatia mtafsiri uhuru wa kueleza jambo kwa kutumia mtazamo tofauti wa kueleza ujumbe wa MC huku akiongozwa na maana ya MC. Kulingana na Munday (2001), katika utaratibu huu neno au mafungu ya maneno hupewa maana za kisemantiki na kipragmantiki ambazo ni za kimuktadha. Ili kuweza kutumia ufundi huu lazima mtafsiri awe na ujuzi wa lugha zote mbili. Ulinganifu

unahu mbinu ya kufafanua hali ile ile kwa kutumia miundo tofauti ili kupata matini linganifu. Mkakati huu huchukuliwa kuwa aina ya urekebishaji unaohusu matumizi ya lugha katika tamaduni tofauti.

Utohozi unahu mbinu inayotumiwa wakati jambo au hali inayoelezwa katika LC haijulikani katika LL; yaani lugha na utamaduni lengwa zinaweza kukosa visawe ambavyo vinapatikana katika LC (Munday, 2001). Newmark (1988) anasema kuwa utohozi hutumiwa pale ambapo mtafsiri hugeuza muundo wa maneno ya LC na kuchukua muundo wa LL. Utohozi huhakikisha uwasilishaji wa maana hata kama visawe vinakosekana katika LL.

Kuhusu tafsiri ya kimawasiliano, Newmark (1988) anasema kuwa mkakati huu unalenga kuhamisha ujumbe wa MC kama ulivyo kwa kuzingatia yaliyomo na kwa kuzingatia maana ya kimuktadha. Hapa ulinganifu, ukubalifu pamoja na wepesi wa kueleweka kwa ML ndio unaotiliwa mkazo. Kwa hivyo matini hutafsiriwa kwa kuzingatia kiwango cha ufahamu wa walengwa. Maneno hubadilishwa na kuchukua visawe vya kiuamilifu kusudi walengwa wapate kuuelewa ujumbe kwa urahisi. Newmark (1988) anasema kuwa mkakati huu ndio ulio na uwezo wa kusababisha athari sawa za MC kwa ML. Kulingana na Munday (2001), mbinu hii ni ya kiufasiri na huzingatia walengwa zaidi ili waweze kuelewa ujumbe. Mkakati huu, kwa mujibu wa Munday (2001), unafaa kwa kazi za kifasihi kwa kuwa unampa mtafsiri uhuru wa kiubunifu na pia unalenga kuwasilisha ujumbe.

Akifafanua tafsiri ya kinahau, Newmark (1988) anasema kuwa mtafsiri hutumia nahau ambazo hazipatikani katika MC kuwasilisha ujumbe katika ML. Katika tafsiri ya kinahau maana ya kileksia kwenye MC hypotea kwa kuwa mtafsiri hutumia visawe kutoka kiwango kingine cha kiplagmantiki (Baker, 1992). Mtafsiri hutumia mkakati huu kutafsiri kazi za kifasihi kwa nia ya kutia mnato katika matini tafsiri ili mlengwa aweze kupata ujumbe kwa njia yenye mvuto.

Newmark (1988), akieleza tafsiri ya kiuaminifu, anasema kuwa mtafsiri hulazimika kutia juhudii zaidi kutoa tafsiri yenye maana sawa na ile ya MC. Mtafsiri huhakikisha kuwa tafsiri yake imezingatia utamaduni wa MC ili iweze kuwasilisha ujumbe kwa

njia iliyo sawa. Mtafsiri hufungwa na mpangilio wa mawazo ya mwandishi kiasi cha kuzuia ubunifu wake kudhihirika katika matini tafsiri. Hii ni kwa sababu analazimika kuhifadhi kiwango cha kisarufi na cha kileksia katika matini tafsiri.

Mawazo ya wataalamu hawa kuhusu mikakati ya kutafsiri yanalingana. Mikakati ya kutafsiri inayoitwa taratibu za kutafsiri na Newmark inalingana na mikakati ya kutafsiri inayoitwa na Mahmoud (2007) mikakati ya kutafsiri moja kwa moja kwa kuwa kulingana nao mikakati hii inahusu vipengee vidogo vya lugha kama vile maneno na sentensi. Nayo mikakati ya kutafsiri inayoitwa na Mahmoud (2007) mikakati ya wazi na ile inayoitwa na Newmark mbinu za kutafsiri inahusu kuhamisha maana ya LC hadi LL. Kwa hivyo kwa namna hii mawazo yao yanalingana. Hata hivyo mawazo yao yanatofautiana kwa kuwa kulingana na Ordudari mikakati ya kutafsiri neno moja kwa moja inahusu kuhamisha neno moja kwa moja kutoka lugha moja hadi nyingine. Kulingana na Newmark (1988), taratibu za kutafsiri na hata mbinu za kutafsiri zinahusu kuhamisha ujumbe wala sio kuhamisha neno au kipengee chochote cha lugha kutoka lugha moja au nyingine.

Mawazo ya wataalamu hawa kuhusu mikakati ya kutafsiri yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa yalimwongoza mtafiti katika kuchunguza mikakati iliyotumiwa na mtafsiri Matundura (2013) kuhakikisha kuwa ujumbe wa MC umewasilishwa kwa walengwa kwa njia isiyoonyesha ugeni kwao. Mtafiti alichunguza kama mikakati iliyotumiwa na mtafsiri ilifanikisha uhamishaji wa ujumbe wa MC kwa njia iliyo asili kwa msomaji lengwa.

#### **2.4 Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi**

Matumizi ya TU katika mawasiliano hulifanya wazo kutokea kwa udhahiri wenye mnato na usahihi. Ni vigumu sana kupata lugha ambayo haitumii TU katika mawasiliano. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza mikakati ya kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri za kifasihi kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, uchambuzi wa mikakati ya kutafsiri TU ulifanywa kwa kiwango cha kufaa lengo hili. TU zilizochunguzwa ni pamoja na nahau, istiari na tashbihi.

#### **2.4.1 Mikakati ya Kutafsiri Nahau**

Tafsiri yoyote bora kama anavyosema Newmark (1988) ni inayoweza kuhamisha ujumbe wa MC kwa ML kwa njia isiyoonyesha ugeni kwa msomaji wa ML. Katika kazi za kifasihi ambapo lugha hutumiwa kisanaa watafsiri hutatizika sana katika kutafuta visawe linganifu kutoka LL. Newmark (1988) anasema kuwa changamoto kubwa inayomkabili mtafsiri si ya kisarufi bali ni ya kileksia. Kwa mfano tafsiri sisisi ya nahau “Eupe kama theluji” inaweza kuonyesha ugeni sana katika lugha ambayo hailinganishi weupe na theluji mathalani iwapo theluji haijulikani katika mazingira husika. Katika sehemu kame kwa mfano nahau hii itaeleweka ikitafsiriwa kama “Eupe kama maziwa”.

Baker (1992) anasema kuwa tatizo kubwa katika kutafsiri nahau ni kuitambua nahau ile na kuifasiri sawasawa. Anasema kuwa tafsiri ya nahau hutegemea maana za kiuamilifu kwa kuwa nahau huwa na maana fiche ambayo mtafsiri anapaswa kuzingatia ili kuelewa alilokusudia mtunzi. Hivyo muktadha wa matumizi humsaidia mtafsiri kung’amua maana iliyokusudiwa na mwandishi ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu kwa walengwa. Baker (1992) anaibuka na mikakati minne ya kutafsiri nahau ambayo ilitumiwa kuchunguza tafsiri za nahau katika tafsiri za Matundura *Musa na Pepo* (2013) na *Musa Mashakani* (2013):

- i. Mtafsiri anaweza kutumia nahau yenyewe usawa wa kimaana na kileksia. Maana hapa ni kuwa nahau iliyokusudiwa na mwandishi ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu kwa walengwa. Hali hii hupatikana kwa nadra sana. Hata hivyo, Baker (1992) anasema kuwa mtafsiri huwa makini kutafsiri nahau kutoka MC hadi ML ili aweze kudumisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.
- ii. Mtafsiri anaweza kutumia nahau yenyewe usawa wa kimaana lakini ikiwa na tofauti za kileksia. Inawezekana kupata nahau katika LL iliyona maana sawa na ile ya nahau katika LC lakini ikiwa na vipengele tofauti vya kileksia. Newmark (1988) anasema kuwa lengo kuu la tafsiri ni kuhamisha ujumbe kutoka LC hadi LL. Kwa kuwa ujumbe unaohamishwa unakusudiwa kuwa na athari sawa kwa mlengwa kama ulivyokuwa kwa msomaji wa MC, mtafsiri anaweza kuteua nahau yenyewe maana sawa na ile ya MC lakini ikitofautiana kileksia ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu kwa walengwa.

- iii. Nahau inaweza kutafsiriwa kwa kutoa ufanuzi wake. Hii ndiyo njia ya kutafsiri nahau inayotumika sana wakati ambapo visawe linganifu vinakosekana katika LL au inapoonekana kuwa lugha ya kinahau haifai katika ML kwa sababu ya tofauti ya kimtindo baina ya LC na LL.
- iv. Kutafsiri nahau kwa kuifutilia mbali. Hali hii hutokea nahau inapokosa kisawe cha karibu katika LL au ikiwa maana yake haiwezi kufafanuliwa kwa urahisi. Kwa mujibu wa Baker (1992), mkakati huu hautumiki sana na hata wataalamu wengi hawautumii kama mkakati mmoja wa kutafsiri nahau.

#### **2.4.2 Mikakati ya Kutafsiri Istiari**

Istiari ni tamathali ya usemi inayotoa ulinganifu fiche baina ya vitu viwili vyenye sifa fulani zinazofanana ila vyenyewe havifanani. Kwa mfano “fulani ni fisi karamuni” ni istiari kwa kuwa yeye si fisi. Hata hivyo ufananisho huu unatumwiwa kulinganisha fisi na mtu huyo. Fisi ni mnyama mlafi na mtu anayeelezwa hapa ana sifa ya ulafi. Hivyo matumizi ya istiari humwezesha msomaji kuuelewa ujumbe kwa kuwa kinachofananishwa kinaelewaka vyema kwake. Hii ndiyo sababu Newmark (1988) anaeleza kuwa istiari hutumiwa na mwandishi kueleza maana iliyokusudiwa kwa njia inayoelewaka bayana. Kwa kuwa istiari hutumiwa kwa njia ya kufananisha dhana inayojulikana na ile ambayo mwandishi anakusudia kuwasilisha, mtafsiri anapaswa kutumia mkakati wa kutafsiri istiari ambao utamwezesha kuwasilisha maana ya istiari hiyo kwa ML bila kutatiza uwasilishaji wa ujumbe. Istiari inatofautiana na tashbihi kwa kuwa istiari haitumii vilinganishi kama vile ‘kama’, ‘mithili’ au ‘ja’.

Kulingana na Newmark (1988), matatizo ambayo humkibili mtafsiri ni ya kileksia na wala sio ya kisarufi. Mathalani mtafsiri anaweza kukosa visawe linganifu vyta istiari husika katika LL au apate istiari yenyе maana sawa lakini yenyе maana tofauti kimuktadha. Kwa hivyo, Newmark (1988) anaendelea kusema kuwa tafsiri ya istiari huwa ya kiuamilifu kwa sababu maneno huwa na maana za kimuktadha. Ifuatayo ni mikakati ya kutafsiri istiari iliyopendekezwa na Newmark (1988) na ambayo imezingatiwa katika utafiti huu:

- i. Istiari inaweza kuhifadhiwa kama LL itaruhusu; yaani kama itaelewaka na waomaji lengwa.
- ii. Kutafsiri istiari kwa istiari yenyе maana sawa katika LL.

- iii. Kutafsiri istiari kwa kisawe cha tashbihi.
- iv. Kutafsiri istiari kwa kisawe cha tashbihi na dhana.
- v. Kutafsiri istiari kwa ufanuzi.
- vi. Kuhifadhi istiari hiyo pamoja na kutoa maelezo ya dhana.
- vii. Kutafsiri istiari kwa kuifutilia mbali.

Kuhusu mkakati wa wa kutafsiri istiari kwa kuihifadhi, Newmark (1988) anasema kuwa mtafsiri anaweza kutumia kisawe cha istiari husika ambacho hakihitilafiani kwa misingi ya kitamaduni ya lugha zote mbili. Ni muhimu kuelewa hapa kwamba istiari inayoteuliwa inaweza kuwa na umbo tofauti na istiari iliyotumika katika MC mradi iwe na ulinganifu wa kiuamilifu. Mtafsiri anapoamua kutumia mkakati huu sharti azingatie tofauti za kitamaduni katika matumizi ya lugha. Jambo hili husaidia kuondoa utata ambao unaweza kusababishwa na tofauti za kitamaduni (Nzyoka, 2014).

Mkakati wa kutafsiri istiari kwa istiari yenye maana sawa katika LL hutumika sana kwa istiari za neno moja kwa kuwa ni rahisi kupata kisawe cha neno moja ambacho hakitaibua maana tatanishi katika muktadha husika. Istiari ambazo hutumiwa kimataifa au na jamii mbalimbali hutafsirika kwa urahisi kwa kuzingatia mkakati huu kwa kuwa inakuwa rahisi kupata visawe vya moja kwa moja. Aidha, kupata visawe linganifu katika ML inakuwa rahisi ikiwa kuna mwingiliano wa kitamaduni.

Mkakati wa kutafsiri istiari kwa kisawe cha tashbihi hutumika aghalabu kwa kuwa istiari na tashbihi zinakaribiana mno kimuundo na kimatumizi (Newmark, 1988). Tafsiri ya istiari kwa kisawe cha tashbihi hutoa maana iliyo wazi kwa kuwa ni ya ufananisho wa moja kwa moja. Kwa mfano, istiari kama “Juma is a rabbit” ikitafsiriwa kwa tashbihi itakuwa “Juma ni mjanja kama sungura.” Tafsiri hii bila shaka itakuwa dhahiri kwa walengwa wa ML.

Kuhusu mkakati wa kutafsiri istiari na dhana, Newmark (1988) anasema kuwa huu ni mkakati wa makubaliano kwa kuwa unahuishisha tafsiri kisemantiki na kimawasiliano. Tafsiri kisemantiki hulenga wapokezi walio na ufahamu wa jambo linalozungumziwa na mtafsiri na hivyo wanaoweza kuelewa ujumbe bila kuongezewa dhana. Tafsiri kimawasiliano huwa ni kwa wale wanaoweza kupotoka ikiwa ufanuzi hautatolewa

katika matini. Kwa mfano, katika mfano uliotolewa hapo juu kuhusu tafsiri ya istiari kwa tashbihi “Juma is a rabbit” tafsiri yake kwa tashbihi na dhana itakuwa “Juma ni mjanja kama sungura, haaminiki.” Dhana ya kutoaminika inatoa ufanuzi unaoufanya ujumbe wa MC kueleweka kwa uwazi zaidi.

Mkakati mwingine uliopendekezwa na Newmark (1982) ni ule wa kutafsiri istiari kwa ufanuzi. Kuna baadhi ya istiari ambazo hazina visawe vya kiistiari. Upungufu huu unasababisha haja ya kutumia mkakati huu ili ujumbe uweze kuhamishwa. Newmark (1988), anasema kuwa ufanuzi unaotolewa kufidia matumizi ya istiari unapaswa kutoa maana na ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Tafsiri ya istiari inapofanywa kwa ufanuzi mtafsiri hana budi kuzingatia muktadha wa matumizi. Vinginevyo ML itakosa ulinganifu na pia itawakanganya walengwa. Toury (1995) anasema kwamba mkakati huu unalenga kuwasilisha ujumbe bila kuzingatia sifa za kisanaa. Hervey na Higgins (1992) wanasema kuwa mkakati huu una dosari kwa sababu matumizi ya lugha kisanaa huwa yamepunguzwa. Hata hivyo ujumbe unapaswa kuzingatiwa zaidi ukilinganishwa na kipengee cha sanaa katika tafsiri (Newmark, 1988).

Kuhusu mkakati wa kuhifadhi istiari pamoja na kutoa maeleo ya dhana, Newmark (1988) anasema mtafsiri anapotumia mkakati huu anaongeza ufanuzi kwa kuwa ikiwa istiari ni ngumu kueleweka, walengwa wanaweza kukosa kuelewa maana iliyokusudiwa. Hata hivyo anashauri kwamba mtafsiri ahakikishe kuwa ufanuzi hauongezei maana na kwamba sio mrefu kiasi cha kupotosha maana.

Istiari inaweza kutafsiriwa kwa kufutiliwa mbali (Newmark, 1988). Newmark anasema kuwa tamathali inaweza kufutiliwa mbali iwapo utendakazi wake unatekelezwa na tamathali nyingine. Tamathali inapokariwa katika matini huwachosha wasomaji wake. Ili kuzuia hali hii mtafsiri huiondoa sehemu nyingine kwenye matini.

#### **2.4.3 Mikakati ya Kutafsiri Tashbihi**

Wills (1983) anafafanua tashbihi kama maeleo ya kiufananisho ambayo yanatumiwa kufananisha dhana moja na nyingine kwa kutumia maneno ya ulinganishi wa moja kwa moja. Matumizi ya kipekee ya maneno ya ulinganishi wa moja kwa moja

humwezesha msomaji au msikilizaji kutambua tashbihi kwa urahisi. Dhana inayofananishwa huwa na sifa ambazo zinaeleweka kwa urahisi na kwa kufananisha dhana moja na nyingine mlengwa huelewa kinachowasilishwa kwa urahisi. Hata hivyo ingawa tashbihi zinatambulika kwa urahisi, kuzitafsiri kunahitaji uangalifu mwingi kwani wakati mwingine kunaweza kuwa changamoto kubwa kwa mtafsiri hasa pale ambapo lugha zinazohusika zinatofautiana sana kiutamaduni. Hii ndiyo sababu Wills (1983) anasema kuwa mtafsiri hana budi kuchagua kwa makini mikakati mwafaka ya kutafsiri tashbihi ili kuweza kuhamisha ujumbe kwa njia ambayo haitatizi mawasiliiano. Pierini (2007) ameibua mikakati sita ya kutafsiri tashbihi. Pierini anasema kuwa mtafsiri hawezi kutumia mkakati bila kuzingatia ufaafu wake. Katika sehemu inayofuata mikakati iliyotumiwa kutafsiri tashbihi imefafanuliwa :

- i. Kuhifadhi tashbihi (Tashbihi kutafsiriwa moja kwa moja bila kufanyiwa mabadiliko yoyote).
- ii. Kutafsiri tashbihi kwa istiari.
- iii. Kutafsiri tashbihi kwa dhana bila kuhifadhi tashbihi.
- iv. Kutafsiri tashbihi kwa tashbihi tofauti lakini yenye maana sawa.
- v. Kuitupilia mbali tashbihi.
- vi. Kutafsiri tashbihi kwa ufanuzi.

Pierini (2007) anasema kwamba mkakati wa kuhifadhi tashbihi unaweza kutumiwa kutafsiri tashbihi katika kazi za kifasihi. Tafsiri za namna hii huwa wazi na kwa hivyo hueleweka kwa urahisi. Kwa mfano, “It is as white as snow.” Tafsiri ya kwa kuzingatia mkakati huu ni, “Ni nyeupe kama theluji.” Hata hivyo tafsiri ya namna hii inaweza kumtatiza mlengwa hasa pale ambapo maana ni ya kimuktadha. Ili kuzuia tatizo kama hili mtafsiri hana budi kuwa mwangalifu ili kuteua visawe linganifu vya tashbihi hasa kwa kuzingatia muktadha husika.

## **2.5 Mikakati ya Kutafsiri Nomino za Pekee**

Nomino za pekee huchukua nafasi muhimu katika kazi za kifasihi na kwa hivyo lazima zitiliwe maanani zinapotafsiriwa katika lugha ngeni. Kuna umuhimu wa kutumia mikakati mwafaka ya kutafsiri nomino hizi ili kuhifadhi ujumbe wa mtunzi na aidha kuandika tafsiri linganifu. Hervey na Higgins (1992) wanaeleza mbinu mbili za kutafsiri nomino za pekee: jina linaweza kuhamishwa moja kwa moja kutoka LC

hadi LL bila kufanyiwa mabadiliko yoyote au linaweza kutohözwa ili kulingana na matamshi au maandishi ya LL. Hata hivyo wanapendekeza njia nyingine ya kutafsiri nomino za pekee kuwa mwatiko wa utamaduni. Hapa, majina ya LC yanabadilishwa kwa majina ya kiasili ya LL ambayo maana yake ya moja kwa moja ni tofauti, ila yanadokeza maana zinazolingana kitamaduni.

Kuhusu tafsiri ya nomino za pekee, Newmark (1988) anasema kuwa majina ya kwanza ya watu yanahamishwa moja kwa moja na kwa hivyo kuweza kuhifadhi uraia. Hili hufanyika pale ambapo inakisiwa kuwa majina yale hayadokezi maana yoyote katika matini. Hata hivyo uhamishaji huu haufai pale ambapo maana inayodokezwa na majina haya ni muhimu.

Leppihalme (1997) anapendekeza kuhifadiwa kwa jina lile kwa kulitumia kama liliyvo; kulitumia jina lile na kisha kutoa mwongozo au kulitumia jina lile halafu kutoa ufanuzi kwa utondoti. Anapendekeza pia kubadilisha jina hilo kwa jina jingine la LL. Vilevile Leppihalme (1997) anasema kuwa jina lile linaweza kutupiliwa mbali lakini maana yake ikahamishwa kwa njia nyingine kama vile kwa kutumia nomino ya kawaida au kwa kutupilia mbali jina na maana yake pamoja.

Mawazo ya wataalamu hawa yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yalimpa mtatifi mwongozo wa kuchunguzia mikakati aliyyotumia mtafsiri katika kutafsiri nomino za pekee. Swali ambalo mtatifi alijiuliza ni kama tafsiri za nomino za pekee zimewasilisha maana ya MC kwa msomaji wa ML kwa njia iliyo asili kwake.

## 2.6 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ulinganifu. Wataalamu mbalimbali kama vile Catford (1965), Nida na Taber (1969), House (1977), Newmark (1981), Baker (1992), Vinay na Darbelnet (1995), na Pym (2010) wameeleza mitazamo mbalimbali ya nadharia ya ularanifu. Wataalamu hawa wamefanua ularanifu kama uhusiano uliopo kati ya MC na ML unaotokana na mikakati ya kutafsiri TU na NP iliyotumiwa na mtafsiri.

Ulingenifu ni mojawapo ya mambo muhimu katika tafsiri. Koller (1979) anasema kuwa kwa kawaida ulinganifu hujengwa kwa misingi ya: 1) maneno ya LC na LL yanayomaanisha kitu kile kile katika ulimwengu halisi, 2) Maneno ya LC na LL yanayoibua maana sawa au maana inayofanana katika fikira za wazungumzaji asili wa lugha zote mbili, 3) Maneno ya LC na LL kuweza kutumika katika miktadha sawa au inayolingana katika lugha husika, na 4) Maneno ya LC na LL kuweza kuwa na athari sawa kwa wasomaji wao. Kufuatia maelezo haya, ulinganifu una maana kwamba lengo la tafsiri ni kuunda ML ilio na maana sawa na MC. Kupitia tafsiri basi Mtafsiri hulenga kuwapa wasiofikia MC nafasi ya kuifurahia kwa namna isiyo na doa wala kuingiliwa kwa vyovyyote (Nyangeri, 2014). Utafiti huu kufuatia mawazo haya ya Koller ulichunguza mikakati iliyotumika kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee kwa lengo la kubainisha mikakati inayofaa zaidi katika kuunda matini tafsiri inayowasilisha maana ya MC.

Kulingana na Hervey na Higgins (1992), ulinganifu ndio unaowezesha tafsiri kuwa na athari sawa kwa wasomaji wake kama ilivyokuwa MC kwa wasomaji wake. Baker (1992), akiendeleza maneno haya, anasema kwamba ulinganifu ni mchakato ambao kwao tamko lililoandikwa katika lugha moja linanuiwa kuwasilisha maana sawa na tamko katika lugha nyingine. Utafiti huu unachunguza tafsiri za tamathali za usemi na nomino za pekee ili kubainisha ulinganifu baina ya MC na ML kwa kuzingatia mawazo haya ya wataalamu hawa.

Nida (1943) anasisitiza kusudi la matini badala ya maneno yaliyotumiwa na mwandishi. Nida anasema kuwa katika tafsiri linganifu mtafsiri huelewa ni hadhira ya aina gani ambayo mwandishi wa MC alikuwa akiandikia. Akiwa na uelewa huu mtafsiri huweza kutoa tafsiri si kwa sababu ya tafsiri tu bali yeye naye huijenga upya kazi ile ili kuweza kuilenga hadhira yake ambayo inaweza kuwa katika muktadha tofauti na ule wa hadhira ya MC. Nida (1943) anasisitiza kwamba yaliyomo ndiyo muhimu sana katika tafsiri yoyote ile. Kulingana na Jakobson (2000), tafsiri linganifu inahusu uhamishaji wa ujumbe wote kutoka lugha moja hadi nyingine wala haihusu kuhamisha sehemu za ujumbe. Mtafsiri kwa hivyo hurekodi ujumbe wote na kisha kuuhamishia LL.

Kulingana na Nida (1964), hakuna vitu viwili ambavyo vinalingana sawasawa na pia hakuna visawe kamili. Anaendelea kusema kuwa kwa tafsiri inahusisha lugha mbili na kwamba kila lugha ina sifa zake mahususi, lazima kila tafsiri ipoteze kiwango fulani cha ujumbe wa MC. Hivyo ni kusema kuwa hatuwezi kupata matini tafsiri iliyo sawasawa na MC. Kwa hivyo kwa mujibu wa Nida (1964), ulinganifu si sawa na usawa bali ni aina ya mfanano. Nyangeri (2014) anaongeza kuwa athari ya kijumla ya tafsiri inaweza kukaribia ile ya MC ila haiwezi kuwa sawa. Hii ni kutohana na ukweli kuwa hakuna lugha mbili zinazofanana mia kwa mia wala ishara zao kupewa maana zinazofanana ama kupangwa kwa mifumo sawa. Hii inaonyesha kwamba kupata ulinganifu kati ya MC na ML ni jambo linalowezekana. Nida (1964) anafafanua aina mbili za ulinganifu: ulinganifu wa kimuundo unaolenga umbo na maudhui ya ujumbe yaani anasema kuwa katika ulinganifu wa kimuundo ML huwiana sana na MC kimuundo na kiyaliyomo. Anaeleza kuwa kuna ulinganifu badilifu unaojikita katika kanuni ya athari linganifu ambapo uhusiano baina ya mpokeaji lengwa na ujumbe unapaswa kuwa sawa na ule wa mpokeaji asili na ujumbe. Kwa hivyo katika ulinganifu badilifu mtafsiri hutia juhudu kuwasilisha maana ya MC katika LL kwa lugha ya kawaida kwa wasomaji wa LL. Nida anashauri kuwa matumizi ya muundo linganifu yanaweza kuathiri pakubwa ML kwa kuwa inaweza kuwa vigumu kwa tafsiri hiyo kuelewaka kwa urahisi na walengwa. Nida na Taber (1969) wanafafanua tafsiri badilifu kama kanuni ya kutafsiri ambayo kwayo mtafsiri hujaribu kuhamisha maana ya MC kwa jinsi ambavyo maneno ya LL yatakuwa na athari sawa kwa wapokeaji katika utamaduni lengwa kama maneno katika maandishi ya awali yalivyokuwa kwa hadhira yake. Ulinganifu badilifu huzingatia utohozi, msamiati na urejeleaji wa kitamaduni ili kupunguza ugeni katika muktadha wa LL. Kulingana na Nida (1964), ujumbe uliotafsiriwa lazima ulenge mahitaji ya kiisimu ya mpokeaji wa matini pamoja na matarajio ya kitamaduni. Ulinganifu badilifu ndio uliozingatiwa katika utafiti huu. Mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ilichunguzwa ili kubainisha ulinganifu kati ya matini tafsiri na MC.

Kwa upande wake, House (1977) anapendelea ulinganifu wa kisemantiki na ule wa kipragmatiki na aidha anahoji kwamba MC na ML hazina budi kushabihiana kiuamilifu. Uamilifu huu kwa mujibu wa House (1977) unaweza kuafikiwa kwa

kutumia njia za ulinganifu wa kipragmatiki. Kulingana na mtaalamu huyu, tafsiri inaweza kuchukuliwa kuwa na ubora wa kutosha kama muundo na uamilifu wake unawiana na ule wa MC. House anafafanua dhana mbili kuhusu tafsiri: tafsiri wazi ambayo hailengi hadhira lengwa kwa kuwa lazima ioneckane kuwa tafsiri na tafsiri fiche ambayo ni ML iliyo na uamilifu sawa na MC kutokana na juhudzi za mtafsiri kushughulikia tofauti za kitamaduni. Utafiti huu unajikita katika tafsiri fiche kwa kuwa ulinganifu ambao unachunguzwa unalenga athari ya ML kwa walengwa.

Newmark (1988) anaeleza aina mbili za ulinganifu: tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Tafsiri ya kisemantiki inalenga maana kwa kuhifadhi sifa za MC ilhali tafsiri ya kimawasiliano inajikita katika athari ya tafsiri. Yaani tafsiri ya kimawasiliano inalenga mahitaji ya walengwa na kujaribu kuwardhisha. Tafsiri ya kisemantiki inasisitiza umuhimu wa mtunzi wa MC nayo tafsiri ya kimawasiliano inalenga kuwafikia wasomaji wengi. Kulingana na Newmark (1988), katika mchakato wa kutafsiri matini za kifasihi, kuna sentensi ambayo huhitaji tafsiri ya kimawasiliano na pia kuna sentensi kutoka kwenye matini hiyo hiyo ambayo huhitaji tafsiri ya kisemantiki. Hitaji la kimsingi kwa aina yoyote ya mawasiliano ni kuhakikisha ya kwamba ujumbe umehamishwa kikamilifu kutoka kwa mwanzilishi wa ujumbe hadi kwa mpokeaji. Vivyo hivyo mtafsiri analazimika kujaribu awezavyo kutoa ujumbe ulio na ulinganifu wa karibu sana na MC katika ML ili msomaji wa ML aweze kuelewa ujumbe wa awali vya kutosha; la sivyo tafsiri kama aina ya mawasiliano itaishia kuanguka.

Baker (1992) anasema kuwa tofauti za miundo ya kisarufi baina ya lugha zinazohusika zinaweza kuathiri sana jinsi ambavyo ujumbe unavyohamishwa na kwa hivyo mtafsiri anaweza kulazimika kutoa au kuongeza ujumbe fulani katika ML kwa kukosa kategoria fulani ya kisarufi katika LL. Mtafsiri huafikia ulinganifu unaoitwa na Baker ulinganifu wa kisarufi. Baker (1992) anafafanua ulinganifu wa kipragmatiki ambao hushughulikia ujumbe uliodokezwa katika matini. Anasema kuwa jukumu la mtafsiri ni kushughulikia maana zilizodokezwa ili kuweza kuhamisha ujumbe wa MC kwa njia iliyo sawa. Lengo la kimsingi kwa mtafsiri ni kubuni ujumbe uliokusudiwa katika LC kwa namna ambavyo itaeleweka na walengwa. Baker (keshatajwa) anaendelea kueleza ulinganifu wa kimatini kama ulinganifu unaoweza kuafikiwa kati

ya MC na ML kulingana na ujumbe na kuchukuana kwa MC na ML. Uamuzi wa mtafsiri kudumisha mchukano kati ya MC na ML hutegemea hadhira lengwa, madhumuni ya tafsiri na aina ya matini. Kufuatia mawazo haya ya Baker (1992), utafiti huu ulichunguza jinsi tofauti baina ya lugha za Kiingereza na ya Kiswahili zilivyoshughulikiwa katika kitafsiri tamathali za usemi na nomino za pekee ili kupata tafsiri linganifu. Utafiti huu umechunguza namna ujumbe uliodokezwa ulivyohamishwa ili kuhakikisha kwamba ujumbe wa MC umewafikia walengwa kwa njia iliyokusudiwa na MC.

Kwa mujibu wa Pym (2010), ulinganifu ni dhana inayokisiwa tu kwa kuwa hakuna ulinganifu kamili baina ya lugha mbalimbali. Anaona kuwa ulinganifu ni uhusiano wa athari sawa baina ya MC na ML na unaweza kupatikana katika kiwango chochote cha kiisimu kuanzia muundo hadi uamilifu. Utafiti huu unalenga kubainisha kama mikakati ya kutafsiri TU na NP imewezesha MC na ML kuwa na athari sawa kwa wasomaji wake.

Kufuatia maelezo ya watetezi wa ulinganifu, ikiwa ujumbe unaweza kutafsirika kwa namna fulani, ina maana kwamba kiasi fulani cha ulinganifu kinaweza kufikiwa katika LL. Kinyume, ikiwa ujumbe hauwezi kutafsirika, ina maana kuwa hakuna ulinganifu wa MC unaoweza kuafikiwa katika lugha lengwa. Upungufu wa tafsiri unasababishwa na umuhimu wa ulinganifu katika tafsiri. Kulingana na Catford (1965), tafsiri isingetafuta ulinganifu, kusingekuwa na udhaifu wa tafsiri, na maandishi yoyote yaliyotafsiriwa yanaweza kuchukuliwa kuwa toleo sahihi la MC. Kwa hivyo, kuwepo kwa upungufu wa tafsiri kunadhihirisha vyema umuhimu wa ulinganifu katika tafsiri. Kadhalika, ugumu wa tafsiri wakati mwengine unatokana na umuhimu wa ulinganifu katika tafsiri. Inakubaliwa kwa jumla kwamba tafsiri ni ngumu kuliko ubunifu asilia na hili linatokana na hitaji la ulinganifu katika tafsiri. Katika ubunifu asilia, msanii hubuni analokusudia kusema na kulisema kwa jinsi anavyopendelea. Hata hivyo, katika tafsiri, mtafsiri hana uhuru huo kwa kuwa inamlazimu kusema kilichosemwa na mtunzi katika MC na kukisema kwa namna sawa na ile iliyofanywa na msanii asilia (Catford, 1965).

Tafsiri inatarajiwa kutoa kwa uaminifu sifa zote muhimu za MC (Nida na Taber, 1969). Baadhi ya wanaisimu pamoja na wahakiki wa fasihi, wanachukulia kwamba dhana ya uaminifu inaweza kuhusishwa na ulinganifu. Hervey na Higgins (1992) anafafanua kwamba kulenga ulinganifu kumedokezwa katika ufanuzi haswa wa tafsiri. Hapa, ulinganifu unamaanisha upeo wa juu iwezekanavyo wa uwiano baina ya MC na ML. Kwa hivyo ulinganifu si usawa bali ni uwiano baina ya MC na ML.

Wataalamu wa ulinganifu wanakubaliana kuwa lazima pawe na uhusiano fulani baina ya MC na ML ili tafsiri iweze kuitwa tafsiri linganifu. Kwa kuzingatia maelezo yao, utafiti huu ulichunguza uwiano kati ya MC na ML kwa kuzingatia mikakati ya kutafsiri TU na NP ili kubainisha iwapo pana ulinganifu baina ya MC na ML.

## **2.7 Hitimisho**

Ulinganifu ni hitaji la kimsingi katika tafsiri yoyote ile. Kulingana na Nida (1964), si jambo rahisi kupata visawe vinavyofanana kitamathali. Tafsiri ya tamathali huenda ikashindwa kuhamisha ujumbe kikamilifu kwa kutumia visawe vya tamathali. Kwa kawaida, maneno mawili kutoka lugha mbili tofauti hayawezi kuwa na maana sawa sawa kabisa. Utafiti huu ulichunguza mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi pamoja na nomino za pekee ili kupata tafsiri linganifu.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Mpango wa Utafiti**

Utafiti huu ni wa kifasihi na kwa hivyo unachukua mwelekeo wa kimaelezo. Matini mbili za Kiingereza zilizoandikwa na Kimenye (1968): *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost* na tafsiri zao za Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* zilisomwa ili kuzielewa na kuchunguza mikakati ya kutafsiri iliyotumiwa kutafsiri TU na NP. Mikakati iliyoyumiwa kutafsiri TU na NP katika juhudini za kuafikia ulinganifu katika matini tafsiri ilichunguzwa ili kubainisha ufaafu wake.

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Kwa kuwa utafiti huu ni wa kiuchambuzi uliegemea vitabu viwili vya Kimenye (1968): *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost* na tafsiri zao za Kiswahili zilizofanywa na Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* kutoka kwenye Msururu wa Musa. Hata hivyo, vitabu vingine katika msururu huu vilirejelewa. Msururu huu umechaguliwa kwa kuwa ndio msururu wa pekee kuwahi kutafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili.

#### **3.2 Idadi Lengwa**

Idadi lengwa kwa ajili ya utafiti ni vitabu ishirini na viwili: kumi na kimoja vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kimenye (1968) na vingine kumi na kimoja ambavyo ni tafsiri zake zilizofanywa kwa lugha ya Kiswahili na Matundura (2013).

#### **3.3 Uteuzi wa Sampuli**

Utafiti huu umezingatia sampuli makusudi. Oduma (2006) anasema kuwa usampulihaji wa aina hii unahuishisha uteuzi wa sehemu fulani kama eneo la utafiti au watu fulani kama wasailiwa. Sehemu hiyo huteuliwa kwa kuzingatia sababu maalum. Kazi mbili za Kimenye (1968) *Moses in Trouble* na *Moses and the Ghost* pamoja na tafsiri zao za Matundura (2013): *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo* ziliteuliwa. Matini hizi ziliteuliwa makusudi kwa kuwa msururu mzima umeandikwa na mwandishi mmoja na wote ukatafsiriwa na mtafsiri mmoja. Wahusika pia ni wale wale na mandhari ni pale pale katika Taasisi ya Elimu ya Mukibi. Kwa hivyo matini

hizi zeliteuliwa makusudi kuwakilisha nyingine kwani kuteua matini zozote kungetupa matokeo yale yale.

### **3.4 Maadili katika Utafiti**

Mtafiti alipata idhini ya utafiti kutoka kwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia iliyomruhusu kwenda nyanjani kukusanya data. Mtafiti alipata ridhaa kutoka kwa mtafsiri ili kuvifanyia utafiti vitabu vyake. Uchanganuzi wote wa data uliongozwa na nadharia ya ulinganifu. Mtafiti alisoma kwa makini matini mbili za Kimenye (1968) zilizoteuliwa pamoja na tafsiri zao katika lugha ya Kiswahili na kuibua data iliyochanganuliwa.

### **3.5 Ukusanyaji wa Data**

Hatua ambazo zilichukuliwa katika ukusanyaji wa data zinaweza kuelezwu kama ifuatavyo: mtafiti alisoma kwa makini kazi za Barbara Kimenye zilizoteuliwa pamoja na tafsiri zao katika Kiswahili. Baada ya kusoma MC, mtafsiri alidondoa tamathali za kiistiasi, kinahau na kitashbihi kutoka kwenye matini za Kiingereza. NP pia zilidondolewa. Kila tamathali husika ilichunguzwa kwa makini kuona jinsi ilivyotafsiriwa katika Kiswahili. Tamathali hizi pamoja na tafsiri zao zililinganishwa kisha mikakati iliyotumiwa kuzitafsiri ilibainishwa na kufafanuliwa. Kwa kuzingatia maoni ya wataalamu wa tafsiri, mtafiti alichunguza mikakati ya kutafsiri iliyotumika pamoja na ufaafu wake katika kuhamisha ujumbe linganifu. Baadaye hitimisho lilifanywa kuhusu mikakati iliyotumiwa kuzihamisha TU na NP kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili.

### **3.6 Uchanganuzi wa Data**

Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kuegemea mihimili ya Nadharia ya Ulinganifu. Uchanganuzi wa data ulifanywa katika viwango viwili: uchanganuzi wa mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi (TU) hasa nahau, tashbihi na istiari na uchanganuzi wa mikakati ya kutafsiri nomino za pekee (NP). Uchanganuzi ulifanywa kwa kuchunguza matini zinazowakilisha kila nahau, tashbihi na istiari zilizoteuliwa na kulinganisha maana zao na maana iliyohamishwa katika matini tafsiri. NP zinazopatikana katika MC pamoja na tafsiri zao katika ML zilidondolewa na maana zao kulinganishwa. Mikakati iliyotumiwa kutafsiri kila nahau, tashbihi au istiari

iliyodondolewa ilibainishwa. Mikakati iliyotumiwa kutafsiri kila NP iliyodondolewa pia ilibainishwa. Tathmini ilifanywa kwa kuchunguza maana katika matini kimuktadha na pia maana kama inavyojitokeza katika tafsiri yenye. Maana kimuktadha zilichunguzwa ili kubainisha ulinganifu wa maana.

Mbinu elezi imetumiwa katika uchanganuzi wa data. Hii ni mbinu ambayo hujaribu kuchanganua data hasa ile ya nathari kwa maelezo. Data ambayo imekusanywa katika utafiti huu imechanganuliwa kwa kueleza mikakati ya kutafsiri ambayo imetumika katika juhudi za kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri.

**SURA YA NNE**  
**MIKAKATI YA KUTAFSIRI TAMATHALI ZA USEMI KATIKA**  
**RIWAYA ZA MUSA NA PEPO NA MUSA MASHAKANI**

**4.1 Muhtasari wa *Musa Mashakani***

Hadithi ya *Musa Mashakani* inahusu Musa na wanafunzi wenzake wa *Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen*. Kwa kuwa wanafunzi hawaridhishwi na chakula wanachopewa shulenii na labda kwa kusudi la kufanya mzaha, wanakusanya mende waliowapata kwenye chakula walichopewa pale shulenii na kukituma kwa Waziri wa Elimu. Jambo hili halijachukuliwa kwa wepesi na mwalimu mkuu Bw Mukibi ambaye si mtu wa kushindwa. Huu ndio unaokuwa mwanzo wa msururu wa mashaka yanayomwandama Musa pamoja na wenzake hasa King Kong.

**4.2 Muhtasari wa *Musa na Pepo***

*Musa na Pepo* ni hadithi inayohusu wanafunzi wa *Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen*. Baadhi ya wanafunzi hawa hasa wale wa Bweni nambari 3 hawaamini kwamba kuna pepo. Hata hivyo kuna 'pepo' anayenyaparanyapara uga wa shule yao akiwa na jembe lililo inuliwa mkononi. Kuna kicheko cha kutisha kinachosikika nje ya mlango wa nyumba ya Bi Namukasa. Aidha madoadoa ya 'damu' yanaonekana madirishani. Yote haya yanatoka wapi? Kwa kuwa naibu wa mwalimu mkuu, Bw Karanja anaamini kuwa ule 'upepo' unaoendelea shulenii ni mzaha wa wavulana wa Bweni nambari 3, huenda wavulana hawa wakajipata matatani. Kwa hivyo kabla ya kujipata katika mashaka ya kutimuliwa shulenii, wavulana hawa wa Bweni nambari 3 hasa Musa, King Kong na wanafunzi wengine wa Bweni nambari 3 wamejitoa mhanga kumnasa 'pepo' huyu msumbu fu.

**4.3 Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi**

Matumizi ya TU katika mawasiliano hulifanya wazo kutokea kwa udhahiri wenye mnato na usahihi. Ni vigumu sana kupata lugha ambayo haitumii TU katika mawasiliano. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza mikakati ya kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri za kifasihi kutoka Kiingereza hadi Kiswahili uchambuzi wa mikakati ya kutafsiri TU ulifanywa kwa kiwango cha kufaa lengo hili. TU zilizochunguzwa ni pamoja na nahau, istiari na tashbihi.

### **4.3.1 Mikakati ya Kutafsiri Nahau**

Tafsiri bora ni tafsiri ambayo inaweza kuhamisha ujumbe wa MC kwa ML kwa njia isiyooonesha ugeni kwa msomaji wa ML. Katika kazi za kifasihi ambapo lugha hutumiwa kisanaa watafsiri hutatizika sana katika kutafuta visawe linganifu kutoka LL. Kwa mfano tafsiri sisisi ya nahau “Eupe kama theluji” inaweza kuonyesha ugeni sana katika lugha ambayo hailinganishi weupe na theluji mathalani iwapo theluji haijulikani katika mazingira husika. Katika sehemu kame kwa mfano nahau hii itaeleweka ikitafsiriwa kama “Eupe kama maziwa”.

### **4.3.2 Mkakati wa Kutumia Nahau Sawa Kimaana na Kileksia**

Maana hapa ni kuwa nahau ilioyoingi na woga aliposikia mgoto uliofua na kicheko cha kutisha mlangoni. Hali hii hupatikana kwa nadra sana. Hata hivyo, mtafsiri analazimika kuwa makini katika kutafsiri nahau kutoka MC hadi ML ili aweze kudumisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.

Katika MC nahau *my blood ran cold* imetumiwa na Bi Namukasa akieleza jinsi alivoingi na woga aliposikia mgoto uliofua na kicheko cha kutisha mlangoni. Matini inasema hivi:

“Practical jokes, indeed!” Miss Namukasa waspishly replied. “As I was saying to Mr Bakole, here, before you came in, *my blood ran cold* when I heard that tapping on my door and that sinister laugh.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 16)

“Mizaha eeh!” Bi Namukasa akajibu kwa kuudhika. Nilivyokuwa nikimwambia Bw Bakole, kabla ya wewe kuja, *damu iliniganda* niliposikia mgoto ule mlangoni mwangu uliofua na kicheko kile cha kutisha.”

(*Musa na Pepo*, uk. 15)

Kisawe cha kinahau kilichotumiwa, *damu iliniganda* kimedumisha maana ya MC, yaani kutishika sana. Kutishika huku ndiko kunakomfanya Bi Namukasa kutaka kuihama Taasisi ya Mukibi kabisa.

Musa anatumia nahau, *my hair stood on end with fright* anapoeleza hali yake hasa alipomwona yule wanayemdhania kuwa pepo. Hapa Musa anaeleza kuwa aligubikwa na hofu kubwa sana. Faraja yake ilikuwa tu katika kuwepo kwa mwenzake King Kong. Musa anasema hivi:

Automatically, I then looked towards the shadowed building housing the object of our guardianship, and as I did so, a figure clad in a ragged kanzu and carrying a jembe seemed to float from around the corner of the building. *My hair stood on end with fright*, and my conviction that the ghost was a Dorm 2 practical joke suddenly left me. King Kong's presence was my only comfort ...

(*Moses and the Ghost*, uk. 22)

Moja kwa moja niligeuka kulitazama jengo lile lililofunikwa na kivuli cha giza na ambalo lilihifadhi mlindwa wetu. Nilipokuwa nikilitazama, gimba lililovalia kanzu iliyochakaa na ambalo lilibeba jembe mkononi lilionekana likielea kutoka kona moja ya jengo hilo. *Nywele zilinisimama kwa woga*, na wazo kuwa suala la pepo lilikuwa mzaha wa Bweni nambari 2 likanitoka mara moja. Faraja yangu ya pekee ilikuwa kuwepo kwa King Kong.

(*Musa na Pepo*, uk. 22)

Tafsiri hii imehifadhi maana ya MC na pia imedumisha sifa ya kisanaa kwa kutumia kisawe cha kitamathali ambacho ni sifa mojawapo ya kazi za kifasihi.

*Their mouth hanging open* ni nahau nyingine katika MC. Nahau hii inaeleza hali ya Sempa na Okot walipokutana na pepo ana kwa ana. Ingawa walikuwa wamekuja kushika doria kuchukua mahali pa Musa na King Kong, Sempa na Okot hawakutarajia kupatana na yule pepo ana kwa ana na aidha vitendo vya pepo mwenyewe viliwashangaza sana hata wasijue la kufanya; wakasimama tu wakitazama kwa mshangao mkubwa. Nahau, *their mouth hanging open* imetumiwa katika MC kuelezea hali hii ya mshtuko mkubwa uliowashika Okot na Sempa kufuatia vitendo vya pepo yule. Tunapata yafuatayo katika matini:

The ghost nearly had a fit. He jiggled for a moment on his feet, not knowing which way to turn, then like lightening made a sideways move

which took us by surprise, nipped neatly between Okot and Sempa, and bolted round another corner.

“After him, you dopes!” I cried, for they were standing *staring with their mouths hanging open*, and once more the chase began.

(*Moses and the Ghost*, uk. 24)

Nusura pepo ashikwe na kifafa. Aliyumbayumba kwa muda, asijue pa kutorokea. Kisha, kwa kasi ya umeme, alisonga ubavuubavu – hatua ambayo hatukutarajia – akajipenyeza katikati ya Okot na Sempa na kupiga kona nyingine.

“Mfuantenteni! Wapumbavu nyie!” nikasema kwa sauti, walipokuwa wamesimama pale wakiwa *wamebaki vinywa wazi!* Kwa mara nyingine tukaanza kulifuata gimba lile.

(*Musa na Pepo*, uk. 24)

Matini ML inaonyesha mshangao mkubwa kwa Sempa na mwenzake Okot kufuatia vitendo vya pepo. Ujumbe wa MC umehamishwa kwa njia wasilifu na iliyo wazi kwa kutumia kisawe cha kinahau, *wamebaki vinywa wazi*. Nahau hii inawakilisha hali sawa na hali inayowakilishwa na nahau katika MC, *mouth hanging open*. Hata hivyo, ujumbe umepunguzwa kwa kiasi fulani kwa kuondoa dhana ya *kukodoa macho* ambayo inapatikana katika MC. MC inasema hivi: *standing staring with their mouths hanging open*. Dhana ya kukodoa macho inayojitokeza katika MC inatilia mkazo mshangao uliowashika Sempa na Okot. Hata hivyo kwa vyovyote vile ujumbe wa MC umehamishwa kwa kuwa tafsiri si usawa bali ni aina ya mfanano.

MC imetumia nahau *kept our eyes open* kuonyesha jinsi Musa na wenzake walivyokuwa makini katika kumtafuta mwenzao Mikono Mirefu. Walihakikisha kwamba wamepekuapekua kila pahali kando ya barabara wasije wakamwacha pale. Tunapata yafuatayo katika matini:

Okot and Ajongo obligingly led Mr Lutu well off the beaten track while the *rest of us kept our eyes open* for Itchy Fingers. We scoured the bushes and ditches at the roadside, thinking he might have seen the school fully light and gone into hiding until things settled down.

(*Moses and the Ghost*, uk. 29)

Okot na Ajongo walimwelekeza Bw Lutu katika eneo tofauti huku sisi tuliosalia *tukiangaza macho* yetu kumtafuta Mikono Mirefu. Tulipekuapekua kwenye vichaka na mitaro tukifikiri kuwa huenda aliona taa zimewaka kote shulenii na kuamua kujificha hadi mambo yatakapotulia.

(*Musa na Pepo*, uk. 29-30)

Matini tafsiri inasawiri hali hiyo hiyo inayosawiriwa na MC kwa kutumia nahau: *tukiangaza macho* kama kisawe cha nahau: *kept our eyes open* katika MC. Yaani zinasisitiza kumakinika kwa kina Musa katika kumtafuta Mikono Mirefu.

Kufuatia mambo ambayo yamekuwa yakiendelea katika Taasisi ya Mukibi kuhusu pepo na hasa yaliyotokea usiku uliotangulia, wavulana wa Bweni nambari ya 3 walijua kwamba kesi yao na naibu wa mwalimu mkuu haikuwa imekamilika. Kwa hivyo, wanasikiza kwa makini wakati naibu wa mwalimu mkuu anapoanza kuieleza shule yote kuhusu tishio la Bi Namukasa kuondoka na kupoteza fahamu kwa Mikono Mirefu. Walisikiza kwa makini kwa sababu hawakutaka kuitwa na chochote ambacho kingesemwa na Bw Karanja kwa kuwa walifahamu kuwa lazima kingewahusu. Kule kusikiliza kwa makini kunaonyeshwa kwa njia ya kitamathali na nahau: *We pricked our ears* katika MC. Katika ML, nahau hii imehamishwa kwa kisawe cha kinahau, *tulitega masikio yetu ndi*. Nahau hii imehamisha maana ya MC kwa njia wazi isiyotatiza mawasiliano. Matini zinasema hivi:

Even when he told all the boys in our dorm to stand while he let the rest of the school to know, in nasty scathing tones, exactly what a lot of rotters we were, we didn't feel too bad.

*We pricked our ears*, however, when he pointed out that because of what he termed our ‘thoughtlessness’, Miss Namukasa was threatening to leave, and ‘one particularly sensitive boy has failed to bear the strain imposed by the ghost story nonsense, and consequently is suffering from loss of memory.’

(*Moses and the ghost*, uk. 34)

Hata pale alipoamuru wavulana wote wa bweni letu wasimame, kisha akaifahamisha shule nzima, kwa sauti iliyojaa dharau, jinsi tulivyokuwa watu waovu, hatukuhisi vibaya sana.

*Tulitega masikio yetu ndi*, hata hivyo, wakati aliposema kwamba kwa sababu ya kile alichokitaja kuwa, ‘kukosa akili kwetu’, Bi Namukasa alikuwa anatishia kuondoka, na kwamba ‘mvulana mmoja dhaifu ameshindwa kuhimili vishindo vilivvosababishwa na kadhia hii ya kipumbavu kuhusu pepo na kwa hivyo amepoteza fahamu’.

(*Musa na Pepo*, uk. 34)

*Get lost* ni nahau ambayo imetumiwa na Musa katika MC. Musa ameitumia nahau hii kumwamuru mvulana mgeni shulenii kumwondokea anapomjia Musa kumweleza uzushi kwamba pepo aliyekamatwa alitambuliwa kuwa Mzee Mukibi na kwamba kwa wakati huu amelazwa katika hospitali ya watu wenye akili punguani. Bila shaka Musa alihusika katika kumkamata yule pepo na kwa hivyo ilikuwa vigumu kwake kustahimili uongo kama ule. Kwa hivyo akamwamuru yule mvulana kumwondokea.

Katika matini tafsiri, nahau, *get lost* imetafsiriwa kwa nahau *potelea mbali* katika lugha ya Kiswahili. Nahau hii imehamisha ujumbe wasilifu wa MC kwa ML. Katika muktadha huu, ni chukizo kwa Musa kisikiza uongo wa yule mvulana kwa kuwa akiwa mmoja wa waliomsaka na kumkamata pepo, alijua kwa kina yote yaliyomhusu pepo aliyekamatwa. Ili kujiondolea kero anamwamuru kumwondokea kwa kutumia nahau, *potelea mbali*. Tunapata yafuatayo katika matini:

The story of how dorm 3 laid the ghost provided an endless source of interest and, naturally, was subjected to gross distortion.

One short sighted new boy came to me with the version that the ghost had been revealed as Old Mukibi who has since been admitted to a mental home. I told him to *get lost*.

(*Moses and the Ghost*, uk. 87)

Kisa cha jinsi wavulana wa Bweni nambari ya 3 walivyomnasa ‘pepo’ kilinoga shulenii. Ingawa kiliwavutia watu wengi, kilivurugwa na kutiwa chumvi mno.

Mvulana mmoja mgeni mwenye shida ya kuona alinijia na fasiri tofauti ya kisa hicho. Alisema kwamba pepo huyo alikuwa ametambuliwa kuwa ni Mzee Mukibi ambaye, tangu ugunduzi huo, alikuwa amelazwa katika hospitali ya watu wenyewe punguani. Nilimwambia *apotelee mbali*.

(*Musa na Pepo*, uk. 87).

#### **4.3.3 Mkakati wa Kutumia Nahau Tofauti lakini yenyenye Maana Sawa**

Inawezekana kupata nahau katika LL iliyo na maana sawa na ile ya nahau katika LC lakini ikiwa na vipengele tofauti vya kileksia. Itakumbukwa kuwa lengo kuu la tafsiri ni kuhamisha ujumbe kutoka LC hadi LL. Kwa kuwa ujumbe unaohamishwa unakusudiwa kuwa na athari sawa kwa walengwa kama ulivyokuwa kwa wasomaji wa MC, mtafsiri anaweza kuteua nahau yenyenye maana sawa na ile ya MC lakini ikitofautiana kileksia ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu kwa walengwa.

Tunapata nahau, *laughing their heads off* katika MC. Nahau hii imetumiwa na Musa akieleza maoni yake kuwa wavulana wa Bweni nambari ya 2 walikuwa na msisimko na furaha kubwa hasa kwa kujua kwamba wavulana wa Bweni nambari ya 3 ndio ambao wangelaumiwa kufuatia kadhia ya pepo kumsumbu Bi Namukasa ambaye sasa anatishia kuihama Taasisi ya Mukibi. Musa anatumia nahau hii, *laughing their heads off* kumaanisha kuwa wavulana wa Bweni nambari 2 lazima wanacheka sana kufuatia masaibu yaliyowapata wavulana wa Bweni nambari ya 3. Matini tafsiri imehamisha nahau hii kwa kisawe cha nahau tafauti lakini inayowasilisha ujumbe wa MC kwa ML. Nahau iliyotumiwa katika ML ni, *nina hakika wanavunjika mbavu kwa vicheko*. Nahau hii inaeleza kuwa wavulana wa Bweni nambari 2 walicheka kupita kiasi kwa kufurahia masaibu yaliyowapata wavulana wa Bweni nambari 3. Tafsiri hii imeuhamisha ujumbe wa MC kwa ML kwa lugha iliyio wazi kwa walengwa. Tunapata yafuatayo katika matini:

“... I bet anything it was Dorm 2! If Husseini did see the figure with the jembe, how come it’s taken so long for him to tell anybody about it?”

“*I bet they are laughing their heads off* at the thought of our dorm getting the blame,” I said bitterly.

Rukia nodded, “Yes, I noticed this morning how they were as much amused as interested in what happened to us.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 16-17)

“... Bila shaka ilikuwa ni Bweni nambari 2! Ikiwa ni kweli Husseini alilionga gimba hilo lenye jembe, iweje imemchukua muda mrefu hivi kumwelezea yeyote kulihu?”

*Nina hakika wanavunjika mbavu kwa vicheko* kuona kuwa bweni letu ndilo lililoelekezwa lawama,” nikasema kwa uchungu.

“Ndio. Leo asubuhi, niliona jinsi walivyofurahishwa na masaibu yaliyotupata,” Rukia alikubaliana nami.

(*Musa na Pepo*, uk. 17)

Tunapata nahau *red-handed* katika MC. Wanafunzi wamekuwa wakisumbuliwa na pepo ambaye wamegundua sasa kwamba ana ushirika na wanaume wawili. Ugunduzi huu bila shaka umeiongeza shaku yao kwamba yule pepo hakuwa pepo hasa bali alikuwa binadamu. Kwa hivyo wanatafuta mbinu ya kuwawezesha kumshika ‘pepo’ pamoja na washiriki wake bila ya wao kutarajia. Tunapata yafuatayo katika matini:

What set us back, of course, was that we didn’t know when the ghost and his two friends intended to visit us again. It wasn’t until after lunch that we hit upon the idea of posting scouts near the spot where the strange car had been concealed. We knew it wouldn’t be easy to give the alarm from there, but we could think of no other way of ensuring *we would catch the men red-handed*.

(*Moses and the Ghost*, uk. 64)

Kilichoturudisha nyuma, bila shaka, ni kule kutojua ni lini huyo pepo na marafiki zake wawili waliniua kurudi kutusumbua tena. Hatukuwa na suluhu yoyote hadi baada ya chakula cha mchana tulipopata wazo la kuwatuma maskauti karibu na eneo ambapo gari lile lisilokuwa la kawaida lilikuwa limefichwa. Tulifahamu kuwa haingekuwa rahisi kwao kututahadharisha kutoka mahali hapo, lakini hatukuwa na mbinu nyingine ya kuhakikisha kwamba *tumewafumania wanaume hao peupe* wakitekeleza njama yao.

(*Musa na Pepo*, uk. 64-65)

Katika matini tafsiri, nahau *red-handed* imetafsiriwa kwa nahau, *fumania peupe*. ML inasema: ...kuhakikisha kwamba *tumewafumania wanaume hao peupe wakitekeleza njama yao*. Maana inayojitokeza katika muktadha huu ni ile ya kuwakamata ghafla bila wao kutarajia. Tafsiri hii imehamisha ujumbe wa MC kwa njia ya kitamathali inayoipa mnato wa kisanaa. Neno *fumania* katika ML limedokezwa katika MC katika ile dhana ya *kushika bila kutarajia*.

Nahau, *life had reached its lowest ebb* imetumiwa katika MC na Musa kuelezea magumu ambayo yamewapata yeye na rafikiye King Kong. Katika kipindi chote cha wiki moja ambacho kimekuwa zamu ya Bweni nambari 2 kuwa wapishi, Musa na King wamekuwa wakipewa nusu ya chakula walichokuwa wakipewa wengine. Kama inavyoeliza katika matini, katika siku ya mwisho ya upishi wa wanafunzi wa Bweni nambari 2, Musa na King Kong walikuwa wanakaribia kufa njaa. Wakiwa katika hali hii ya kudhoofika kutokana na makali ya njaa, wananyimwa chakula kwa kuchelewa kufika bwaloni. Yanayofuata ni kwamba kunazuka vita baina ya King Kong na Ssali (kiranja wa Bweni nambari 2). Kufuatia vita hivi naibu wa mwalimu mkuu Bw Karanja anasikiza tu maelezo ya wavulana wa Bweni nambari 2 na kukataa kuyasikiliza maelezo ya Musa na King Kong kwamba wapishi wa Bweni nambari 2 walikuwa wakiwaua kwa njaa. Bw Karanja anawaachilia wapishi wa Bweni nambari 2 kurudi jikoni. Licha ya Musa na King Kong kudhihakiwa na wavulana hao wa Bweni nambari 2 walipokuwa wakiondoka kuelekea jikoni, walichapwa kinyama na Bw Karanja. Musa na King Kong wanatamauka na kuona kama maisha yao yamefikia kikomo. Ndipo Musa anaposema katika MC kuwa, *life had reached its lowest ebb so far as King Kong and I were concerned*. Matini zinasema hivi:

Everything was over in a few minutes, but the stinging pain of the strokes he gave us lingered on for the rest of the afternoon. Life had reached *its lowest ebb* so far as King Kong and I were concerned.

(*Moses in Trouble*, uk. 18)

Kila kitu kilikwisha baada ya dakika chache, isipokuwa uchungu wa viboko tulivyocharazwa uliobaki nasi alasiri nzima. Mimi na King Kong tulihisi kwamba maisha yalikuwa *yametuendea tenge*.

(*Musa Mashakani*, uk. 19)

Katika matini tafsiri, Musa anaeleza kuwa yeye na King Kong walihisi kuwa maisha yalikuwa yamewaharibikia. Musa anasema haya kwa tamathali ya kinahau, *mimi na King Kong tulihisi kwamba maisha yalikuwa yametuendea tengé*. Nahau hii inasawiri hali ya Musa na rafikiye kukata tamaa sawa na hali inayosawiriwa na nahau, *life had reached its lowest ebb* katika MC. Tafsiri hii kwa hivyo imewasilisha maana ya MC kwa njia isiyotatiza mawasiliano na yenye mvuto wa kisanaa.

Katika MC tunapata nahau *to face the music*. Ni baada ya Musa kurusha kipande cha paipai kilichompata Bi Nagendo usoni. Kutokana na tendo hili wavulana wanapomwona naibu wa mwalimu mkuu akiingia katika bwalo, wanaweza kukisia kilichomwalika pale. Kila mvulana ananyamaza kimya. Wale wa Bweni nambari 2 wanajifanya kuwa na kazi nyingi jikoni. MC inatuambia kuwa waliwaacha Rukia, King Kong na Musa *to face the music*, yaani kupata adhabu kali.

Nahau hii imetafsiriwa kwa nahau katika LL, *kukiona cha mtema kuni* katika ML. Katika muktadha huu, wavulana wa Bweni nambari 2 waliwaacha Rukia, King Kong na Musa kupokea adhabu kali sana kutoka kwa naibu wa mwalimu mkuu. Dhana hii ya adhabu kali ndiyo inayobainishwa na nahau, *kukiona cha mtema kuni*. Kwa hivyo hii ni tafsiri wasilifu ya ujumbe wa MC kwa ML. Matini zinasema hivi:

There was no time to argue, though, because at that moment Mr Karanja came striding towards us, and an expectant hush fell over the dining hall. As soon as they saw him coming, our fellow cooks took themselves off and pretended to be busy in the kitchen, leaving Rukia, King King and Me *to face the music*. The deputy head came straight to the point.

“I have just seen Miss Nagendo in a very distressed state,” he said. “She tells me that Moses Kibaya threw some fruit at her.”

(*Moses in Trouble*, uk. 32-34)

Hakukuwepo muda wa ubishi, kwa sababu wakati huohuo, Bw Karanja alifika bwaloni na kuelekea tulipokuwa. Kimya cha kaburi kikajiri ghafla kwenye bwalo. Wapishi wenzetu walitoweka pindi walipomwona akija, na kujifanya walikuwa na shughuli nyingi jikoni. Wakaniacha mimi, Rukia na King Kong *kukiona cha mtema kuni*. Naibu wa mwalimu mkuu naye akaweka wazi nia ya mjo wake. “Nimemwona Bi Nagendo katika hali

mbaya ya kimawazo,” akasema. “Ameniambia kuwa Musa Kibaya alimrushia tunda.”

(*Musa Mashakani*, uk. 34)

#### **4.3.4 Mkakati wa Kutafsiri Nahau kwa Ufafanuzi**

Hii ndiyo njia ya kutafsiri nahau inayotumika sana wakati ambapo visawe linganifu vinakosekana katika LL au inapoonekana kuwa lugha ya kinahau haifai katika ML kwa sababu ya tofauti ya kimtindo baina ya LC na LL.

Nahau: *paused for effect* imetumiwa katika MC. Mikono Mirefu anapowatajia wanafunzi wenzake kuwa shule yao ina pepo, bila shaka wanafunzi wanakuwa na hamu kubwa ya kujua kuhusu madai hayo. Mikono Mirefu anaanza kuwaeleza chanzo cha uvumi huo kuwa ajuza wanayemfahamu – ajuza ambaye hufanya biashara ya chupa tupu sokoni. Mikono Mirefu anawaeleza kuwa ajuza huyu ndiye aliywuliza iwapo amewahi kuona chochote kisichokuwa cha kawaida katika Taasisi ya Mukibi. Baada ya maelezo hayo Mikono Mirefu alinyamaza ili wenzake wapate nafasi ya kutafakari aliyosema. MC inasema, he *paused for effect*. Kisawe cha kiufafanuzi kimetumiwa kuuwasilisha ujumbe huu katika matini tafsiri. ML inasema, *alisita kidogo na kuiacha kauli yake ituingie akilini, ...* Ujumbe unaowasilishwa kwa maelezo haya katika LL ni ule ule ulio katika MC ila mtafsiri ameuunda upya katika ML kwa njia ya maelezo. Tunapata yafuatayo katika matini:

“I’ve just been to the village to fetch some *waragi* for Kigali, and there was an old woman in the bar – you know, the one who deals in empty bottles in the market. Well, she started asking me if I’d ever noticed anything odd about Mukibi’s Educational Institute, and ...” here he *paused for effect, ...*

(*Moses and the Ghost*, uk. 2)

“Nimetoka kijijini muda mfupi uliopita kumletea Kigali pombe yake ya waragi, na kulikuwa na ajuza mmoja kwenye baa hiyo – ushafahamu, yule anayefanya biashara ya chupa tupu sokoni, naam, alianza kuniuliza iwapo nimewahi kuona kitu chochote kisichokuwa cha kawaida katika Taasisi ya Elimu ya Mukibi, na ...” hapo, *alisita kidogo na kuiacha kauli yake ituingie akilini, kisha akaendelea, ...*

(*Musa na Pepo*, uk. 1-2)

Ili kuweza kuiwasilisha maana ya muktadha huu kwa njia wasilifu zaidi maneno:  
*kisha akaendelea* yameongezwa.

Katika MC nahau *dig in the ribs* imetumiwa kuonyesha jinsi King Kong anavyomhimiza Mikono Mirefu kuendelea kuwaeleza kuhusu shule yao kuwa na pepo. Matini inatuambia hivi:

Itchy Fingers shook his head. “No. Listen. I naturally wanted to hear the details, so I asked her what she meant, and she told me the most gruesome story.”

*King Kong dug him in the ribs.* “OK. Go on, the tell us.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 2)

Mikono Mirefu alitikisa kichwa chake. “Hapana! Sikiliza. Nilitaka anisimulie habari hizo kwa undani, kwa hivyo nikamwomba afafanue alichomaanisha. Hapo ndipo aliposimulia kisa cha kuogofya sana.”

“Sawa basi, endelea. Tueleze.” *King Kong akamhimiza.*

(*Musa na Pepo*, uk. 2)

Maana ya kimuktadha inayojitokeza katika nahau *dig in the ribs* ni ile ya kutia mtu moyo kuendelea na shughuli fulani. Kwa hivyo maana ya MC imehamishwa kwa njia iliyowasilifu.

Katika MC Itchy Fingers hapendezwi na wavulana wenzake wa Bweni nambari 3 kwa ubishi wao anapowaeleza kuhusu shule yao kuwa na pepo. Kwa hivyo anawaondokea na kwenda kujitafutia hadhira mpya katika Bweni nambari 2 ambayo anafikiria labda ingemsikiza. Nahau iliyotumiwa katika MC kueleza namna Mikono Mirefu alivyoondoka ni: *Itchy Fingers took himself off in a huff ...* Matini zinasema hivi:

*Itchy Fingers took himself off in a huff* to find a new audience in Dorm 2, and after he had gone, we quietened down enough to relate ghost stories we had heard back in our respective villages.

(*Moses and the ghost*, uk. 4)

Mikono Mirefu *alijiondoa haraka katika kundi letu* ili kwenda kujitafutia hadhira mpya katika Bweni nambari 2. Baada ya yeye kuondoka tulitulia kidogo ili kusimuliana visa vingine kuhusu pepo, ambavyo tulikuwa tumevisikia katika viji viyetu.

(*Musa na Pepo*, uk. 4)

Mikono Mirefu anajiondoa haraka kwa hasira kwa kuwa wenzake wanaonekana kutokubaliana naye kuhusu shule kuwa na pepo. Hali ya Mikono Mirefu kwenda kujitafutia hadhira nyingine kwa kuudhiwa imeondolewa katika matini tafsiri na kwa hivyo kupotosha ingawa kwa kiasi kidogo ujumbe wa MC. Hata hivyo ujumbe kwamba alijitafutia hadhira nyingine umehamishwa. Itakumbukwa kuwa kulingana na nadharia ya ulinganifu, hatuwezi kuwa na ulinganifu kamili. Kinachohitajika katika tafsiri yoyote wasilifu ni aina ya uwiano.

Nahau nyingine ambayo imetumika katika MC ni *shivers down my back*. Nahau hii imetumiwa kuelezea athari ya kisa kuhusu pepo kilichosimuliwa na Rukia kwa wenzake. Kisa hiki kiliogofya sana. Hali hii ya kuogofya ndiyo inayoelezwa na nahau hii: *that sent shivers down my back*. Matini zinasema hivi:

Rukia told a really horrible tale that *sent shivers down my back*, and I was glad when the talk turned to ways and means of getting rid of ghosts.

(*Moses and the Ghost*, uk. 4)

Rukia alisimulia kisa cha kutisha *ambacho kiliniogofya sana*. Hata hivyo nilifurahi wakati masimulizi hayo yalibadilika na kuangazia njia za kuwafukuzia pepo.

(*Musa na Pepo*, uk. 4)

Ufafanuzi ambao umetolewa katika ML umewasilisha maana ya MC kwa njia iliyo wazi isiyomatizwa mlengwa.

Katika MC tunapata nahau, *I should have known you would be at the bottom of this, ...*" Musa aliingiwa na hofu nyingi alipomwona mwanamume anayedhaniwa na wanafunzi kuwa pepo aliyesimuliwa na Mikono Mirefu dirishani. Kutokana na hofu

hii alipiga unyende ambao uliwaamsha wanafunzi wote. Kelele za wanafunzi zinamwalika Bw Karanja ambaye alitaka maelezo kuhusu kilichokuwa kikiendelea. Katika maelezo yanayotolewa na baadhi ya wanafunzi, jina la Musa linatajwa mara kadhaa. Kuhusika huku kwa Musa ndiko kunakomwelekeza Bw Karanja kutumia nahau hii: *I should have known you would be at the bottom of this*, kuwasiliana na Musa.

Katika muktadha huu, Bw Karanja anamlaumu Musa kwa kuwa chanzo cha vurugu iliyotokea bwenini usiku huo. Nahau *be at the bottom* hapa inamaanisha kuwa Musa ndiye aliyechukua nafasi kubwa zaidi katika yale yaliyotokea kuliko wanafunzi wengine. Kisawe cha kiufafanuzi kinachotumiwa katika ML ni *Mhusika*. Tafsiri hii imepunguza ujumbe wa MC katika ML. Ikiwa Musa ni mhusika lazima pana wahusika wengine katika kadhia hii. Mtafsiri labda angeongeza kivumishi *mkuu* ili kumtofautisha Musa na wahusika wengine tafsiri ikawa, *mhusika mkuu*. Hata hivyo ubunifu wa mtafsiri umejidhihirisha pale anapoongeza sehemu ya Musa kujieleza kwa naibu wa mwalimu mkuu: sehemu ambayo haiko katika MC. Ni kutokana na muktadha huu ambapo naibu wa mwalimu mkuu anamwambia Musa kuwa hakujuu ni kwa nini hakubahatisha kuwa Musa alikuwa mhusika katika kadhia ile. Matini zinasema hivi:

Mr Karanja, the deputy head, stopped the flow of wild stories after my name had recurred several times, and he turned, grim-faced furious, in my direction.

He said, “I should have known you would be *at the bottom of this*. I’ll see you in my office before class in the morning.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 8-9)

Bw Karanja, naibu wa mwalimu mkuu, alikomesha msururu wa hadithi zao za kubuni kuhusu pepo, baada ya jina langu kutajwa mara kadhaa. Alinigeukia huku uso wake ukiashiria ghadhabu kana kwamba alitaka kunimeza mzimamzima.

Nilimweleza kile nilichokuwa nimekiona. Hata hivyo maelezo yangu hayakuwa na uzito hasa baada ya yale yaliyotiwa chumvi ambayo alikuwa amesimuliwa na wenzangu.

“Sijui kwa nini sikubahatisha kwamba ulikuwa *mhusika* katika kadhia hii,” Bw Karanja alisema. “Uje unione ofisini mwangu kabla ya kwenda darasani asubuhi.”

(*Musa na Pepo*, uk. 9-10)

*Benefit of doubt* ni nahau ambayo imetumiwa katika MC na Bw Karanja. Baada ya Musa kutetewa na King Kong kwa kuonyesha ‘damu’ kwenye kishubaka cha dirisha na Bw Karanja mwenyewe kugusa kitu kinachofikiriwa na wanafunzi kuwa damu, kwenye dirisha, anaamua kuamini yanayosemwa na Musa kuhusu pepo usiku huo ingawa anamshuku Musa. Katika kueleza haya Bw Karanja anasema: *I'll give Kibaya the benefit of doubt this time.*

Katika ML, tunapata kisawe cha kiufafanuzi kuwa: *Nitaikubali kauli ya Kibaya kwa leo.* Kauli ambayo Bw Karanja anairejelea hapa haipatikani kamwe katika MC. Ni kauli inayotolewa na Musa katika ML anaposema: *Nilimweleza kile nilichokuwa nimekiona.* Kisawe cha kiufafanuzi kinachotolewa kinatokana na sehemu iliyobuniwa na mtafsiri anapoonyesha yaliyosemwa na Musa katika kujitetea. Matini zinasema yafuatayo:

Mr Karanja wiped his finger clean on a handkerchief and let his gaze travel slowly over us. “*I'll give Kibaya the benefit of doubt this time,*” he said. You can all report to me before class tomorrow. If there is a practical joker in the dormitory, I intend to find out who he is.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 9)

Bw Karanja alipangusa kidole chake kwenye hanchifu kisha akatutazama kwa Muda. “*Nitaikubali kauli ya Kibaya kwa leo,*” akasema. “Nyote mje ofisini mwangu kabla ya kwenda darasani hapo kesho. Iwapo kuna mtu anayejaribu kucheza shere katika bweni hili, ninataka kubainisha ni nani.”

(*Musa na Pepo*, uk. 10)

Tafsiri hii ya nahau *I'll give Kibaya benefit of doubt* kuwa *nitaikubali kauli ya Kibaya kwa leo* imepotosha maana ya MC. Kulingana na muktadha huu, tafsiri ya nahau hii labda ingekuwa: *Ingawa ninamshuku Kibaya nitamsamehe kwa leo.*

*Made a silent appeal to the heavens* ni nahau nyingine ambayo imetumika katika MC. Katika harakati za kumsaka pepo shuleni inagunduliwa kuwa mwanafunzi mmoja – Mikono Mirefu ametoweka. Makundi ya wanafunzi yamepangwa ili kumtafuta kwa kuwa Bwana Karanja anashuku kuwa Mikono Mirefu ni mmoja wa wanafunzi wanaojifanya pepo. Anapopatikana katika nyumba ya Kigali, inawalazimu marafiki zake kubuni namna ya kumnusuru. Marafiki hawa (Musa na wenzake) wanamshauri Mikono Mirefu kujifanya kwamba amepoteza fahamu na kwa hivyo hawezi kusema chochote.

Nahau *made a silent appeal to heavens*, imetumiwa pale ambapo Itchy Fingers anaonekana kushindwa kuiga hali aliyoshauriwa kuiiga ili kujiondoa katika shida inayomkabili. Badala ya kunyamaza kama alivyoshauriwa na wenzake ikiwa ishara kwamba amepoteza fahamu, anapoulizwa na Bw Lutu alikokuwa, anajibu kuwa hakumbuki. Baada ya Mikono Mirefu kuonyesha ishara za kushindwa kutekeleza ushauri, ndipo nahau *made a silent appeal to the heavens* inapotumiwa. Katika muktadha huu, Mutagubya anamwita Mwenyezi Mungu kuingilia kati. Ombi hili linafanywa kimoyomoyo.

Katika matini tafsiri kisawe cha nahau hii kinachotolewa ni *kuomba kimoyomoyo*. Mutagubya anaomba kimoyomoyo ili kumwita Mungu aingilie kati. Ufafanuzi huu umehamisha maana ya MC kwa njia wasilifu. Tunapata yafuatayo katika Matini:

We got him out of Kigali's house and called the others. Mr Lutu came panting to the scene. "Where have you been?" he shouted at Itchy Fingers.  
"You're in big trouble, my boy ..."

Itchy Fingers passed a stiff hand across his eyes and muttered woodenly,  
"I can't remember ..."

Mutagubya nudged me and made *a silent appeal to the heavens*. We both realized that as far as the acting went, Itchy Fingers would never make it to an Oscar.

(*Moses and the Ghost*, uk. 33)

Tulimtoa nyumbani kwa Kigali na kuwaita wenzetu. Bw Lutu alifika hapo akiwa anahema. “Umetoka wapi muda huu wote?” alimkemea Mikono Mirefu. “Umejitia mashakani, kijana wangu ...”

Mikono Mirefu alipitisha mikono mbele ya macho yake na kusema kwa uthabiti, na kwa sauti ya chini, “Sikumbuki ...”

Mutagubya alinipiga kikumbo *na kuomba kimoyomoyo*. Sote tuligundua kwamba kutokana na uigizaji wake mbaya, Mikono Mirefu kamwe hawezi kushiriki katika mashindano ya kuwania tuzo ya uigizaji bora ya Oscar.

(*Musa na Pepo*, uk. 33)

Katika MC tunapata nahau: *made a mess of him*. Nahau hii imetumiwa kumrejelea King Kong. King Kong alikuwa amefunikwa na siafu mwili wote wakamwumiza vibaya sana. Hali hii ndiyo inayoelezwa katika MC kwa nahau: *Those ants had really made a mess of him*. Katika ML nahau hii imehamishwa kwa ufanuzi: Siafu wale walikuwa *wamemdhuru vibaya*. Matini zinasema hivi:

About King Kong, not a word was said, but not long after we had made our beds and settled down in glum silence to the work we had been given to do, he came limping in to join us. Those ants had really *made a mess of him*. He was covered in tiny scabs where they had bitten and hung on long enough to draw blood ...

(*Moses and the Ghost*, uk. 35)

Hakuna hata neno moja lililosemwa kumhusu King Kong. Hata hivyo muda mfupi tu baada ya sisi kutandika vitanda vyetu na kukaa kimya tukifanya kazi tuliyokuwa tumepewa, alifika huku akichechemea, na kujiunga nasi. Siafu wale walikuwa *wamemdhuru vibaya*. Alikuwa amelemewa na vipele vidogo vidogo kwenye sehemu ya ngozi ambako siafu hao walimuumma na kumkwamilia na kumfanya avuje damu.

(*Musa na Pepo*, uk. 35)

*Tear ourselves* ni nahau nyingine ambayo imetumiwa katika MC kuelezea kuachana kwa wanafunzi kila mmoja wao akienda kukaa katika dawati lake Bi Nagendo alipojитома darasani. Katika muktadha huu, nahau hii, *we had to tear ourselves*

inaonyesha kwamba ilikuwa vigumu kwao kuachana ila tu ni kwa vile lisilobudi hutendwa. Nahau hii inatafsiriwa katika matini tafsiri kuwa: tulilazimika kujiepusha. Matini zinasema hivi:

“Man, we’ve felt it! You and King Kong were wise to give the dining hall a miss at lunchtime. The rest of us sat down to bread and water – plus a soul-stirring talk by Karanja on how to make the best of things in an emergency!”

“Well, he did give everybody an orange afterwards,” another boy grudgingly conceded. “An orange!” Rukia grimaced. “It would have served him right if we’d thrown them at him!”

Miss Nagendo, the only woman member of staff bustled into the classroom at that moment, so we had to *tear ourselves* from this fascinating conversation and settle at our desks.

(*Moses in Trouble*, uk. 7)

“Aisee, tumekipata! Wewe na King Kong mlikuwa werevu kulikwepa bwalo wakati wa chamcha. Tumekula mkate na maji – pamoja na mashauri ya Bw Karanja kuhusu namna ya kuishi vyema wakati wa dharura! “

“Naam, baadaye, alimpa kila mtu chungwa,” mvulana mwingine akakiri shingo upande.

“Chungwa!” Rukia akasema kwa hasira. “Ingefaa zaidi kama tungemrushia machungwa hayo!”

Bi Nagendo, mwalimu pekee wa kike katika shule yetu, alijitoma darasani wakati huo. *Tulilazimika kujiepusha* na mazungumzo hayo ya kuvutia na kutulia kwenye madawati yetu.

(*Musa Mashakani*, uk. 7)

Kulingana na muktadha huu hii ni tafsiri wasilifu ya MC. Kwa kuwa mazungumzo yao yalikuwa yanawavutia sana, hawakuwa tayari kuachana lakini kuingia kwa mwalimu kuliwalazimu kuachana.

Katika MC tunapata nahau *his nose in the air*. Nahau hii inaeleza kuhusu Gekonyo ambaye ni kiranja wa Bweni nambari 1. Baada ya Gikonyo kuambiwa na Musa kuwa chai iliyopikwa na bweni lake haikuwa nzuri, analalama kwamba kuna watu wasioridhika na kisha anatoka kwenye meza ya akina Musa kwa jinsi inayoelezwa na MC kuwa *with his nose in the air*. Matini zinasema hivi:

“Well, I hope he keeps his cloves and ginger to himself in future,” I said.

“Some people are never satisfied ...” Gekonyo drifted away from our table *with his nose in the air*. I think at that moment he imagined himself to be the head waiter of some expensive hotel.

(*Moses in Trouble*, uk. 9)

“Natumai atajihifadhia karafuu na tangawizi zake katika siku zijazo,” nikasema. “Watu wengine hawaridhiki kamwe ...” Gekonyo akagura meza yetu *huku akijishaua*. Ninadhani kwa wakati huo, alijiona kuwa kiongozi wa wahudumu katika hoteli ya kifahari.

(*Musa Mashakani*, uk. 10)

Katika muktadha huu, tunaelezwa kuwa Gekonyo alijiona kama kiongozi wa wahudumu katika hoteli ya kifahari. Kwa hivyo, alikuwa na majitwazo kwa kujiona kuwa juu ya wengine. Katika matini kuhamishwa kwa nahau, *with his nose in the air* kuwa, *huku akijishaua* kumewasilisha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC kuwa Gikonyo aliondoka akijigamba.

Katika MC Musa anawakumbusha wenzake kuwa kwake Bi Nagendo *is a pain in the neck*. Musa alikuwa akiwalalamikia wenzake kwa kumnyima chakula kwa madai kwamba alisusia kazi akampeleka nje rafikiye wa kike ambaye ni Bi Nagendo. Katika sura ya nne, Musa aliporusha kipande cha paipai na kwa bahati mbaya kikampata Bi Nagendo usoni, Musa mwenyewe anasema kuwa shauku yake ya siri kwamba Bi Nagendo hakuwa akimpenda ilidhihirika. Shauku hii ilidhihirika kwa namna ambavyo Musa alikaripiwa na kutusiwa na Bi Nagendo ambaye alikataa katakata kusikiza Musa alipomwomba msamaha. Musa anawakumbusha ukweli wanaoufahamu kwamba kwake Bi Nagendo *is a pain in the neck*. Hapa Musa anawakumbusha kuwa Bi Nagendo kwake si rafiki bali maudhi, ni usumbufu na ni machukizo.

Ujumbe huu unajidhihirisha katika matini tafsiri inaposema, mnajua wazi kwamba, kwangu mimi, Bi Nagendo ni kero na bughudha tele! Tafsiri hii imewasilisha ujumbe wa MC kwa njia iliyowazi na isiyotatiza kuelewaka kwa ujumbe. Tunapata yafuatayo katika matini:

“Never mind what you all thought – where is my supper?” I shouted.  
“That’s the point,” Rukia shouted back. “We never saved you any because we thought you had walked off the job with your lady friend!”  
“Well, of all the ... You know as far as I’m concerned *old Nagendo is a pain in the neck!*”

(*Moses in Trouble*, uk. 57)

“Usijali kuhusu mllichofikiria nyinyi. Chajio changu ki wapi?” niliuliza kwa sauti. “Huo ndio ukweli,” Rukia naye akajibu kwa sauti.  
“Hatukukusazia chakula chochote. Tulifikiri kwamba ulikuwa umesusia kazi na badala yake kujiendea zako pamoja na rafiki yako wa kike!”

“Mhh, kati ya wote ... Mnajua wazi kwamba, kwangu mimi, Bi Nagendo *ni kero na bughudha tele!*”

(*Musa Mashakani*, uk. 57-58)

#### **4.3.5 Mkakati wa Kuifutilia mbali Nahau**

Hali hii hutokea nahau inapokosa kisawe cha karibu katika LL au ikiwa maana yake haiwezi kufafanuliwa kwa urahisi. Mkakati huu hautumiki sana na hata wataalamu wengi hawautumii kama mkakati mmoja wa kutafsiri nahau.

Katika matini zote mbili ambazo zimetumiwa katika utafiti huu: *Musa Mashakani* na *Musa na Pepo*, nahau zote zimatafsiriwa, yaani hakuna nahau iliyofutwa katika matini tafsiri na hivyo ni kumaanisha kwamba hakuna ujumbe wa MC uliopotezwa kwa kuifutilia mbali nahau kwa kukosa kisawe cha karibi katika LL.

#### **4.4 Mikakati ya Kutafsiri Istiari**

Matatizo ambayo humkabili mtafsiri katika kutafsiri istiari ni ya kileksia na wala sio ya kisarufi (Newmark, 1988). Mathalani mtafsiri anaweza kukosa visawe linganifu vyta istiari husika katika LL au apate istiari yenye maana sawa lakini yenye maana

tofauti kimuktadha. Kwa hivyo, tafsiri ya istiari huwa ya kiuamilifu kwa sababu maneno huwa na maana za kimuktadha. Katika sehemu inayofuata, tathmini ya tafsiri ya istiari kutoka MC hadi ML imefanywa. Mikakati iliyotumiwa kuhamisha istiari mbalimbali pia imebainishwa.

#### **4.4.1 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Kuzihifadhi**

Katika MC istiari: *near the look of a cat that has lately digested a large mouse* imetumiwa kueleza taswira ya sura ya Mikono Mirefu baada ya kutoweka kwa saa ya kijana mmoja kutoka Bweni nambari 1. Taswira hii ambayo inafahamika vyema na Rukia wakiwa na Musa iliwafafanulia wazi kwamba Mikono Mirefu alikuwa mwenye hatia. Katika matini tafsiri, istiari hii imehamishwa moja kwa moja bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Kuhifadhi istiari hii kumemwezesha mtafsiri kuwasilisha ujumbe wa MC kwa ML kwa njia isiyotatiza. Matini zinasema hivi:

We, three, simply looked at each other, and on Itchy Fingers' face was the expression we had learnt to read all too well. It's too had to describe. I can only say *it is near the look of a cat that has lately digested a large mouse.*

(*Moses and the Ghost*, uk. 12)

Sisi watatu kimsingi tuliangaliana, na kwenye uso wa Mikono Mirefu kulikuwa na ishara ambayo tulikuwa tumejifunza kuitafsiri vizuri sana. Ingawa ni vigumu kuielezea ishara hiyo, ninaweza kusema tu kwamba *inakaribiana na taswira ya uso wa paka ambaye amemmeza panya mkubwa.*

(*Musa na Pepo*, uk. 13)

Maneno *old scarecrow* yametumika katika MC kama istiari kueleza hali ya kudhoofika kiafya kwa Bwana Mukibi. Mzee Mukibi alikuwa mwenye Taasisi ya Elimu ya Mukibi pia mwalimu mkuu. Hapo awali Mzee Mukibi alikuwa mkali sana. Aliwaonyesha cha mtema kuni wanafunzi watundu kwa kuwacharaza vibaya sana. Hata hivyo kutohana na hali yake mbaya ya kiafya, Mzee Mukibi hawezi kuwaadhibu wanafunzi watundu ila kuwatishia tu. Katika muktadha huu, Mzee Mukibi anaitwa na wanafunzi *scarecrow* kumaanisha kwamba hakuna chochote anachoweza kuwafanyia wanafunzi ila kuwaogofya.

Katika ML istiari hii imehifadhiwa. Kisawe hiki, *Sanamu mzee* kimetumiwa kuwasilisha ujumbe wa MC kwa wasomaji lengwa kwa kuwa kama *scarecrow*, *sanamu* hutumiwa hasa na wakulima kuwingia ndege na wanyama waharibifu. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), ya Oxford *Sanamu* ni kitu kilichoundwa, kufinyangwa au kuchongwa katika umbo la viumbe k.v. samaki, ndege, binadamu au wanyama. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) ya Longhorn inaeleza *sanamu* kuwa kitu mfano wa binadamu, ndege, mnyama au samaki kilichotengenezwa kwa kifinyangwa au kuchongwa ili aghalabu kuwakilisha kilicho hai, kinachodhaniwa kuwa hai au kilichokufa lakini kinakumbukiwa na kuenziwa. Kufuatia maelezo haya neno *sanamu* limefaa kuwasilisha ujumbe linganifu kutoka MC hadi ML. Tunapata yafuatayo katika matini:

Hussein of Dorm 2, who had said had seen a figure with a jembe creeping about the school one night, stuck to his story until King Kong threatened to bash him if he didn't tell the truth. He then admitted that what he saw could have been that *old scarecrow*, Mr Mukibi the headmaster, on the snoop.

(*Moses and the Ghost*, uk. 18-19)

Husseini, kutoka Bweni nambari 2, ambaye awali alikuwa amedai kuwa alilionga gimba lenye jembe likinyapanyapa shulenii usiku mmoja, alishikilia hadithi hiyo hadi pale King Kong alipotishia kumpiga endapo hangesema ukweli. Ndipo akakiri kuwa alichokiona huenda kikawa ni yule *sanamu mzee*, Bw Mukibi, mkuu wa shule akiwa katika udukuzi wake.

(*Musa na Pepo*, uk. 18-19)

Neno *worms* limetumiwa kama istiari katika MC. Neno hili limetumiwa na King Kong kuwataja wavulana wa Bweni nambari 2. Badala ya kuwaita *Dorm 2 boys* anawaita *Dorm 2 worms*. Tunaona kwamba istiari hii imetumiwa na King Kong kuonyesha namna alivyowadunisha wale wavulana wa Bweni nambari ya 2 kiasi cha kuwafananisha na wadudu.

Katika ML istiari hii imehifadhiwa. Kisawe kilichotumiwa ni *wadudu* na kwa hivyo tafsiri ya *Dorm 2 worms* ikawa *wadudu wa Bweni nambari 2*. Watu ni tofauti sana na wadudu; wadudu ni viumbe dhaifu sana wakilinganishwa na binadamu. Kwa jinsi King Kong anavyowadunisha wavulana wa Bweni nambari ya pili, anaona kuwa anaweza kuwapiga wote akiwa peke yake. Yafuatayo ndiyo tunayopata kwenye matini:

To add to the general confusion, King Kong kept jumping up and down on his bed, beating his chest and roaring, “Me King Kong! Me go punch those *Dorm 2 worms*!”

(*Moses and the Ghost*, uk. 19-20)

Kama kutia msumari moto kwenye kidonda, King Kong alirukaruka kitandani mwake, akijigongagonga kifuani na kunguruma, “Mimi King Kong! Ninaenda kuwapiga hao *wadudu wa Bweni nambari ya 2!*”

(*Musa na Pepo*, uk. 19-20)

Bila shaka King Kong hamaanishi wavulana wa Bweni nambari 2 ni wadudu bali anawaona kuwa wanyonge kama walivyo wadudu.

Istiari nyininge katika MC ni *rabbits*. Istiari hii ilitumiwa na Rukia kuwasuta wavulana wa Bweni nambari ya 2 aliodai kuwa walitumia ujanja katika mchezo waliochezea katika Bweni nambari 3. Aidha, istiari hii imetumiwa na Ssali, kiranya wa Bweni nambari 2 akimjibu Rukia kwa kumwonyesha kwamba wanaotumia ujanja kushinda ni wavulana wa Bweni nambari ya 3, yaani bweni la kina Rukia. Matini zinasema hivi:

Ssali, the Dorm 2 prefect, looked at us suspiciously. “OK,” he said. “We don’t mind accepting the challenge if you come to play in our dorm. Last time we played in Dorm 3 there were too many peculiar coincidences.” “What you mean!”King Kong bellowed, jumping to his feet.”Come outside if you say we crooked you!” “Crooked us!” Mimicked Ssali. “If you want the truth, I think it was bare-faced robbery...”“I’ll ...” King Kong began, but Rukia quickly put an end to what promised to be an interesting brawl, with, “Oh, never mind, KK. If they don’t want to play, we’ll leave them alone. They are *rabbits* in any case. ”Stung by the insult,

Ssali retorted, “You come for a couple of games to our dorm and we’ll show you who are *rabbits*!”

(*Moses and the Ghost*, uk. 45-46)

Ssali, kiranja wa Bweni nambari 2, alitutazama kwa kututilia shaka “Sawa,” akasema. Tutakubali hiyo changamoto iwapo mtakuja kuchezea kwenye bweni letu. Wakati uliopita, tulipocheza katika Bweni nambari ya 3 kulizuka visa vingi sana vya kiajabuajabu.” “Unaamaanisha nini?” King Kong akanguruma, huku akisimama. “Tokeni nje ikiwa mnahisi tuliwachezea shere.” “Kutuchezea shere!” akaiga Ssali. “Acha niwaambie ukweli. Huo wenu ulikuwa wizi dhahiri!” “Nita...” King Kong akaanza, lakini Rukia akakomesha haraka ugomvi huo ambaao ulikuwa unatokota. “Usijali KK. Ikiwa hawataki kuchenza, tutaaachana nao. Hata hivyo wao ni *sungura*,” Rukia alimwambia. Kwa kukerwa na matusi hayo, Ssali alijibu, “Njoni mcheze nasi katika bweni letu. Tutawadhihirishia ni kina nani walio *sungura* zaidi.

(*Musa na Pepo*, uk. 45-46)

Ili kudhihirisha ujanja huo uliotekelizwa na wavulana wa Bweni nambari 3, Ssali anasema kuwa katika mchezo waliocheza na Bweni nambari 3 wakati uliopita, MC inasema ...*there were too many peculiar coincidences.*’ Katika Kiswahili, tafsiri ingekuwa kulizuka visa vingi sana vya sadfa za kiajabuajabu. Ila tunaona kuwa mtafsiri amedondosha neno sadfa ili kurahisisha uwasilishaji wa ujumbe wa MC kwa ML bila kupotosha maana.

*Old vulture* ni istiari katika MC iliyotumiwa kumrejelea Bwana Mukibi aliye Mwalimu mkuu wa shule. Kulingana na *Oxford Advanced Learner’s Dictionary* (2010), maana ya neno *vulture* ni mtu ambaye hunua kunufaika kutokana na masaibu au mateso ya watu wengine. Maana nyingine ni ndege mkubwa asiyé na manyoya kichwani au shingoni anayekula mizoga. Katika matini tafsiri, istiari hii imehamishwa moja kwa moja kuwa *tai* ambaye kulingana na *Kamusí ya Kiswahili Sanifu* (2004) ya Oxford, ni ndege mkubwa mwenye makucha marefu na makali ambaye chakula chake kikuu ni mizoga. Kwa hivyo istiari hii imetafsiriwa kwa kuihifadhi.

Kutokana na maelezo haya, ndege huyu hufaidi jasho la wengine. Wanafunzi wanamlinganisha Bwana Mukibi na *tai* kwa kuwa wanafunzi wanaendelea kuteseka katika taasisi yake ila yeye anaendelea kufaidika kutokana na karo zinazolipwa na wazazi wao. Aidha Bwana Mukibi hashughuliki kuona kwamba wanafunzi wamepata elimu bora. Wapishi pamoja na wafanyakazi wote wa jikoni wanapogoma wakidai nyongeza ya mshahara, Bwana Mukibi anawalazimisha wanafunzi kufanya kazi zote za jikoni. Wanafunzi hawa hawakufanya kazi tu mbali walizalimika kutafuta chakula ambacho wangewapikia wenzao.

There was no need for Mr Karanja, the deputy head, to rap sharply on the table for silence, since we all stopped eating and talking the moment the *old vulture* darkened the doorway. We stared like frightened rabbits...

(*Moses in Trouble*, uk. 1-2)

Hapakuwa na haja ya Bwana Karanja, naibu wa mwalimu mkuu, kugongagonga meza ili kunyamazisha. Sote tulisitisha kula na kuzungumza pindi *tu tai yule mkongwe* alipozuru pale. Tuliakodoa macho kama sungura waliotishwa...

(*Musa Mashakani*, uk. 1)

Katika MC tunapata *brainless idiot* kama istiari. Imetumiwa kumaanisha yejote asiyenye na akili. Mwalimu mkuu anawataka wavulana waliotuma kifurushi cha wadudu waliokufa kwa Waziri wa Elimu kuinua mikono yao juu. Tayari tumeelezwa katika MC kwamba mwalimu mkuu alipoingia alionekana mwenye hasira sana kiasi kwamba angehatarisha maisha yake kwa kibarua cha kumcharaza viboko kila mvulana mahali pale. Katika hali hii basi ingechukua mvulana mjinga kukiri kwamba yeye ndiye aliyekitekeleza kitendo kile cha hatari.

Istiari hii imetafsiriwa kwa kuhifadhiwa katika matini tafsiri. Katika matini tafsiri tunapata maelezo yafuatayo: *Mwalimu mkuu alisubiri kwa muda wa dakika moja ili yejote asiyekuwa na akili akiri*. Istiari *asiyekuwa na akili* imehamisha maana linganifu ya istiari *brainless idiot*. Matini zinasema:

The headmaster waited a full minute for *some brainless idiot* to confess, and when it eventually dawned on him that nobody was that stupid,...

(*Moses in Trouble*, uk. 2)

Mwalimu mkuu alisubiri kwa muda wa dakika moja ili *yeyote asiye na akili* akiri. Alipobaini kwamba hapakuwa na yeyote mjinga kiasi hicho,...

(*Musa Mashakani* uk. 3)

*Prison fare* ni istiari ilitotumiwa katika MC. Kulingana na *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (2010) *fare* ni chakula kilichotolewa kama mlo. Kwa hivyo chakula kilichopikwa siku ile kilikuwa kibovu kiasi cha kulinganishwa na chakula kinacholiwa na wafungwa. Istiari hii imefafanuliwa kama *chakula cha wafungwa* katika ML. Jamii kwa kawaida hukichukulia chakula cha wafungwa kuwa kibovu na kwa hivyo Rukia anapokilinganisha chakula kilichopikwa na wavulana wa Bweni nambari 1 na chakula kilichipikiwa wafungwa basi inamsaidia msomaji kuwa na taswira kamili ya hali ya chakula kile.

“*Real prison fare!*” Rukia, our dorm prefect, was loudly proclaiming, as we entered. Dangerous criminals are better fed than we are! And if the cooks hadn’t left some bread when they went on strike, we should all have starved.

(*Moses in Trouble*, uk. 6)

“*Hakika kilikuwa chakula cha wafungwa!*” Rukia, kiranja wetu wa bweni, alikuwa akitangaza tulipokuwa tukiingia darasani. “Wahalifu sugu hulishwa vizuri kutushinda! Wapishi wasingalibakisha mkate walipogoma, sote tungalikufa njaa!”

(*Musa Mashakani*, uk. 7)

Tunaelezwa katika MC kuwa wavulana wawili walikimbizwa zahanatini walipozirai ghafla matumbo yao yalipodinda kustahimili takataka kila siku. Yafuatayo ni maelezo hayo:

Gekonyo then threatened the rest of us with all sorts of tortures if we did not eat everything on our plates at every meal. Two boys whose atomachs refused to take so much daily *rubbish*, collapsed suddenly,...

(*Moses in Trouble*, uk. 11)

Baadaye, Gekonyo akatishia kututesa kwa njia mbalimbali ikiwa tungekosa kumaliza chakula ambacho tungepakuliwa katika kila kipindi cha kula. Wavulana wawili, ambao matumbo yao yalidinda kustahimili *takataka* hiyo kila siku, walizirai ghafla...

(*Musa na Pepo*, uk. 12)

Katika muktadha huu, neno *rubbish* ni istiari iliyotumiwa kuonyesha hali mbaya ya chakula kilicholiwa na wanafunzi. Chakula hiki kinalinganishwa na uchafu. Chakula hiki ni kibovu kiasi cha kuweza kutoa uhai badala ya kuhifadhi maisha. Istiari hii imehifadhiwa katika matini tafsiri kama *takataka* na kwa kufanya hivi maana ya MC imehifadhiwa.

#### **4.4.2 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Istiari**

Mkakati wa kutafsiri istiari kwa istiari yenye maana sawa katika LL hutumika sana kwa istiari za neno moja kwa kuwa ni rahisi kupata kisawe cha neno moja ambacho hakitaibua maana tatanishi katika muktadha husika. Istiari ambazo hutumiwa kimataifa au na jamii mbalimbali hutafsirika kwa urahisi kwa kuzingatia mkakati huu kwa kuwa inakuwa rahisi kupata visawe vya moja kwa moja. Aidha, kupata visawe linganifu katika ML inakuwa rahisi ikiwa kuna mwingiliano wa kitamaduni.

Tunapata istiari *owners nose* katika MC. Ni vigumu kitu kuchukuliwa kutoka chini ya pua la mtu bila mtu huyo kuona. Hata hivyo hii ndiyo iliyokuwa tabia ya Mikono Mirefu. Ikiwa tafsiri ya neno kwa neno ingefanywa kisawe cha *owners nose* kingekuwa *chini ya pua la mwenyewe*. Tasiri hii ingekosa mnato wa kifasihi. Ili kupata mnato huo kisawe cha kitamathali kilitumiwa: *machoni pa mwenyewe*. Tunapata yafuatayo katika matini:

(On the one occasion that a group of us were taken to the Animal orphanage at Entebbe, he arrived back at school with a baby crocodile in his pocket. How we got rid of it without the staff finding out is something I haven't time to relate here.) Frankly, though, King Kong and I admire his skill. He can take practically anything from directly under the *owner's nose* without being detected.

(*Moses and the Ghost*, uk. 11)

(Katika hafla moja ambapo baadhi yetu tulipelekwa kuzuru makao ya wanyama yatima mjini Entebbe, alirudi shulenii akiwa na mwana wa mamba mfukoni. Jinsi tulivyomwondoa mwanamamba huyo bila ya walimu kugundua ni jambo ambalo sina muda wa kulisimulia hapa.) Hata hivyo, ukweli ni kuwa mimi na King Kong hupendezwa na ujuzi wake. Kimsingi, anaweza kunyakua kitu chochote kutoka *machoni pa mwenyewe* bila yeye kugunduliwa.

(*Musa na Pepo*, uk. 12)

Tunaambiwa kwenye MC kwamba Bw Karanja anapoingia kwenye bwalo kimya kikuu kilitanda. Istiari inayotumiwa kuelezea hali hii ni *an expectant hush*. Istiari hii inaonyesha kwamba kama anavyokuwa na matarajio mwanamke aliye na mimba ndivyo kilivyokuwa kimya cha wanafunzi. Kuna mengi au makubwa waliyoyatarajia hasa kutokana na kupigwa kwa Bi Nagendo kwa kipande cha paipai kilichorushwa na Musa.

Katika matini tafsiri, kisawe cha kiistiari kimetumiwa. Kimya kilichotanda anapoingia Bw Karanja kinalinganishwa na kimya kinachoshuhudiwa makaburini ambapo ni mahali pa wafu wasiokuwa na sauti. Istiari inayotumiwa katika ML ni *kimya cha kaburi*. Kutumia istiari *kimya cha kaburi* kumedondosha dhana ya matarajio ambayo inasawiriwa na neno *expectant* katika MC na kwa hivyo kupunguza ujumbe wa MC. Hata hivyo kwa kuwa tafsiri si usawa bali ni aina ya ulingano, kwa kutumia istiari *kimya cha kaburi* katika ML kumeweza kuhamisha ujumbe wasilifu kwa ML. Yafuatayo ndiyo tunayopata katika matini:

Rukia turned angrily upon me. “Now you really have got us into a mess,” he said. “Why did you start chucking things about?” “But I didn’t start it!” I replied. King Kong backed me up by saying, “No, he didn’t. One of these dorm 2 fools started the throwing.” There was no time to argue, though, because at that moment Mr Karanja came striding towards us, and an *expectant hush* fell over the dining hall.

(*Moses in Trouble*, uk. 32)

Rukia alinigeukia kwa hasira. “Sasa, kwa hakika umetutia taabuni,” alisema. “Mbona ulianza kutupa vitu kiholela?” “Lakini, si mimi niliyeyaanza!” nikajibu. “Ndiyo hakuanza. Ni mmoja wa mabaradhuli hawa wa Bweni nambari ya 2 aliyeanza kurusha,” King Kong akaniunga mkono. Hakukuwepo muda wa ubishi, kwa sababu wakati huohuo Bw Karanja alifika bwaloni na kuelekea tulipokuwa. *Kimya cha kaburi* kikajiri ghafla kwenye bwalo.

(*Musa Mashakani*, uk. 34)

Istiari: *extra large rat hole* imetumiwa katika MC kunena kuhusu jiko la shule. Jiko la shule linalinganishwa na maficho ya panya. Tunaelezwa hivi katika matini:

“Oh,” she cried, clasping her hands together, “Why didn’t you report to the Sanatorium? The whole school will be down with flu if you, boys in the kitchen, are spreading germs!” From the way she spoke, a stranger might have thought that the school kitchen was a model of hygiene, instead of the *extra large rat hole* that it really was.

(*Moses in Trouble*, uk. 41-42)

“Ala,” alisema, akishikanisha pamoja mikono yake. “Mbona hamkwenda kwa zahanati? Shule nzima itaathiriwa na homa iwapo nyie wapishi mnasambaza vijidudu vyahoma hiyo!” Kutokana na jinsi alivyozungumza, mgeni angefikiria jiko la shule lilikuwa ni kielelezo cha usafi. Kinyume ni kuwa, kwa hakika, lilikuwa *pango la panya*.

(*Musa Mashakani*, uk. 42)

Katika ML istiari inayotumiwa kulitaja jiko la shule ni *pango la panya*. Katika MC maelezo *extra large rat hole* yanaibua dhana ya ukubwa wa mahali pale (ambapo ni makao ya panya) katika mawazo ya msomaji. Kwa hivyo istiari *pango la panya* katika ML ni tafsiri wasilifu ya istiari *extra large rat hole* katika MC. Kulingana na nadharia ya ulinganifu, tafsiri si sawa na usawa bali ni aina ya mfanano.

#### **4.4.3 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Kisawe cha Tashbihi**

Mkakati wa kutafsiri istiari kwa kisawe cha tashbihi hutumika aghalabu kwa kuwa istiari na tashbihi zinakaribiana mno kimuundo na kimatumizi (Newmark, 1988). Tafsiri ya istiari kwa kisawe cha tashbihi hutoa maana iliyo wazi kwa kuwa ni ya ufananisho wa moja kwa moja. Kwa mfano, istiari kama *Juma is a rabbit* ikitafsiriwa kwa tashbihi itakuwa *Juma ni mjanja kama sungura*. Tafsiri hii bila shaka itakuwa dhahiri kwa walengwa wa ML.

*Quivering jelly* ni istiari iliyotumiwa katika MC kueleza woga uliomwingia Mikono Mirefu alipoelezwa kuhusu jinsi alivyotafutwa alipokuwa nje ya shule. Istiari hii imetafsiriwa kwa kisawe cha tashbihi. Kulingana na Newmark (1988), tafsiri ya istiari kwa kisawe cha tashbihi hutoa maana iliyo wazi kwa kuwa ufananisho ni wa moja kwa moja. Katika ML tashbihi iliyotumika kama kisawe cha istiari *he was reduced to a quivering jelly* ni *alianza kutetemeka kwa woga kama jani kwenye upepo mkali*. Ulinganishi wa woga aliokuwa nao Mikono Mirefu na kutingishika kwa majani kwenye upepo mkali kunabainisha maana ya MC kwa walengwa kwa njia iliyo wazi kabisa.

Because he is even dumber than King Kong, we had to spell it out for him,

and when he got the message *he was reduced to a quivering jelly*.

(*Moses and the Ghost*, uk. 32)

Kwa kuwa Mikono Mirefu alikuwa na tatizo kubwa zaidi la kuelewa kuliko King Kong, tulilazimika kumfafanulia bayana yaliyojiri. Alipouelewa ujumbe wetu hatimaye, *alianza kutetemeka kwa woga kama jani kwenye upepo mkali*.

(*Musa na Pepo* uk. 32)

Kwa mzaha tu na akiwa na nia ya kumkera Rukia, Musa anaomba mkate wa kila siku kutoka kwa Maulana. Kwa njia ambayo wanafunzi wa Bweni nambari ya 3 wanaona kama ni kujibiwa kwa dua ya Musa, lori moja linaangusha masanduku mawili: moja likiwa na maziwa ya unga na jingine mikebe ya mchuzi; bidhaa ambazo walikuwa wakizisaka. Tukio hili linawastaajabisha wanafunzi lakini wengi wanakataa kuamini.

Wanafunzi ambao wanakataa kuamini wanalinganishwa na mwanafunzi wa Yesu Kristo katika Biblia ambaye alikataa kuamini habari kuhusu kufufuka kwa Yesu akisema kuwa angeamini habari hizo ikiwa Yesu angejidhihirisha kwake. Katika MC, istiari inayotumiwa kueleza hali hii ni *Doubting Thomases*. Katika istiari hii dhana ya kutilia shaka jambo fulani inajitokeza. Dhana hii imedondoshwa katika matini tafsiri inapohamishwa kuwa *sawa na Tomaso wa Biblia*. Kama mkakati wa kiufafanuzi ungetumiwa, *sawa na Tomaso wa Biblia aliyeamini kwa kuona*. Ufafanuzi huu unahamisha ujumbe linganifu kwa njia iliyo wazi zaidi.

Tafsiri ya kitashbih: *sawa na Tomaso wa Biblia* hata hivyo imeongeza kipengee cha *Biblia*, jambo ambalo linawasaidia wasomaji wanaomfahamu *Tomaso wa Biblia* kuuelewa ujumbe kwa njia rahisi. Tunapata yafuatayo katika matini:

Of course, the tale spread throughout the dining hall when the rest of the school appeared for breakfast, although, through constant telling, it became distorted to the extent that my prayers had brought the tins raining down from Heaven there were several *Doubting Thomases* among the boys, but they quickly shut up when they received their mugs of steaming tea, thick with good, sweetened milk, which we were not afraid to use extravagantly.

(*Moses in Trouble*, uk. 69-70)

Bila shaka, hadithi hiyo ilienea kote kwenye bwalo wakati wanafunzi wengine shuleni walipofika ili kupata kiamshakinywa. Kwa kusimuliwa tena na tena, hata hivyo, iligeuzwa na kudaiwa kwamba maombi yangu yaliisababisha mikebe ile kutona kutoka mbinguni. Kulikuwa na wavulana wengi ambao, *sawa na Tomaso wa Biblia*, walikataa kuamini. Iliwabidi kufyata ndimi zao pindi walipopokea makopo yao ya chai moto na yenye maziwa ya kutosha. Hatukuwa na woga wa kuyatumia maziwa hayo kwa kubadhiri.

(*Musa Mashakani*, uk. 70-71)

#### **4.4.4 Mkakati wa Kutafsiri Istiari kwa Ufafanuzi**

Kuna baadhi ya istiari ambazo hazina visawe vya kiistiari (Broeck, 1981). Upungufu huu unasababisha haja ya kutumia mkakati huu ili ujumbe uweze kuhamishwa.

Ufafanuzi unaotolewa kufidia matumizi ya istiari unapaswa kutoa maana na ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Tafsiri ya istiari inapofanywa kwa ufanuzi mtafsiri hana budi kuzingatia muktadha wa matumizi. Vinginevyo ML itakosa ulinganifu na pia itawakanganya walengwa. Mkakati huu hulenga kuwasilisha ujumbe bila kuzingatia sifa za kisanaa. Ingawa baadhi ya wataalamu kama vile Hervey na Higgins (1992) wanasema kuwa mkakati huu una dosari kwa sababu matumizi ya lugha kisanaa huwa yamepunguzwa, ujumbe wa MC unapaswa kuzingatiwa zaidi ikilinganishwa na kipengee cha sanaa katika tafsiri (Newmark, 1988).

Tunaelezwa katika MC kwamba, kiranja wa bweni lao, Rukia aliyejitia ustaarabu tangu alipoanza kumchumbia msichana aliyeitwa Clarissa, alimshauri Mikono Mirefu kuongea baada ya kukimeza chakula kilichokuwa kinywani. Inaendelea kusema kuwa Rukia aliona ugumu kuketi kwenye meza moja na hao wavulana wengine wasiostaarabika.

Rukia, our dormitory prefect, had a thing about good manners now that he was writing regularly to a girl called Clarissa and planned to become engaged to her next holidays. He found it painful to sit at the table with us, whom he described as *ignorant peasants*

(*Moses and the Ghost*, uk. 1)

Rukia, kiranja wa bweni letu, alijitia ustaarabu tangu alipoanza kumwandikia barua msichana aliyeitwa Clarisa, ambaye alipanga kumchumbia wakati wa likizo iliyofuata. Alikereka sana kuketi kwenye meza moja nasi ambaa alituona kuwa *hatujastaarabika*.

(*Musa na Pepo*, uk. 1)

Maneno *ignorant peasants* yametumiwa katika MC kama istiari. Tafsiri ya maneno haya kama yalitafsiriwa nje ya muktadha ingekuwa *wakulima wadogo wasiofahamu chochote*. Hata hivyo, tafsiri ya kiufafanuzi ilizingatiwa ili kuhamisha ujumbe linganifu katika matini tafsiri. Tafsiri ya istiari *ignorant peasants* kuwa *sisi ambaa alituona kuwa hatujastaarabika* imetokana na hali ya Mikono Mirefu kuzungumza chakula kikiwa kimejaa kinywani; jambo lililo kinyume cha ustaarabu. Rukia amejifunza ustaarabu kutokana na msichana Clarisa.

Maneno *one of his days* katika MC yametumika kama istiari kumaanisha nafasi nzuri kwa Mikono Mirefu kutumia kuendeleza tabia yake ya wizi. Neno *day* katika kamusi ya, *English – Swahili Dictionary (2010)* ya TUKI toleo la tatu limetafsiriwa kuwa *siku*. Kama mtafsiri angezingatia maana hii basi maana ya *his days* ingekuwa *siku zake* na hivyo kupoteza maana ya kimuktadha. Ili kuhamisha ujumbe linganifu kutoka MC hadi ML, tafsiri ya kiufafanuzi ilitumika. Tafsiri ya: Itchy Fingers was going to have *one of his days* ikawa: Mikono Mirefu *alikuwa anatumia fursa hiyo kufanya kile ambacho hupenda kukifanya zaidi*.

...and, to make matters worse, it was soon apparent that Itchy Fingers was going to have *one of his days*. Elsewhere I think I have mentioned that he acquired his nickname from his uncontrollable habit of picking up other people's property.

(*Moses and the Ghost*, uk. 11)

La kuudhi zaidi ni kwamba ilibainika punde kuwa Mikono Mirefu *alikuwa anatumia fursa hiyo kufanya kile ambacho hupenda kukifanya zaidi*. Kwingineko nadhani nilikuwa nimekwisha kutaja kwamba alipewa jina hilo kutohana na hulka yake isiyodhibitika ya kuiba mali ya wenzake.

(*Musa na Pepo*, uk. 12)

Istiari *teacher's pet* imetumiwa na Okot ambaye aliamini kuwa Musa alipendelewa na naibu wa mwalimu mkuu. Kwa hivyo istiari hii imetafsiriwa kuwa *kipenzi cha mwalimu* ili kupata uwiano wa kimaana baina ya MC na ML.

“That's a laugh!” Okot sneered as soon as the deputy head had gone.

“There's a practical joker here all right, and it's Holy Moses. Only old old Karanja will do anything to take the blame off him. That's what happens when you're *teacher's pet!*”

(*Moses and the Ghost*, uk. 9)

“Hicho ni kichekesho!” Okot alisonya pindi tu naibu wa mwalimu mkuu alipoondoka. “Ni kweli kuna mtu anayetuchazea shere hapa, naye ni Musa Mtakatifu. Hata hivyo, mzee Karanja atafanya lolote kumwondolea Musa

Mtakatifu lawama. Hivyo ndivyo inavyokuwa wakati wewe ni *kipenzi cha mwalimu!*"

(*Musa na Pepo*, uk. 11)

Neno *woodenly* ni istiari iliyotumiwa katika MC kuonyesha uthabiti wa sauti ya Mikono Mirefu alipokuwa akimjibu Bwana Lutu kuhusu alikokuwa kwa muda wote aliokuwa akitafutwa. Itakumbukwa kuwa mpango wa kujifanya kuwa amepoteza fahamu na kujifanya mpumbavu haukuwa wazo lake bali alishauriwa na wenzake kufanya hivyo ili kujitoa matatani. Hivyo basi lazima angefanya kila juhudui kuwaridhisha wenzake.

Katika ML istiari hii imefafanuliwa. Ufafanuzi wenyewe ni, ...na *kusema kwa uthabiti* , na kwa sauti ya chini. Ufafanuzi huu pia umeongezea istiari hii; na kwa sauti ya chini. Maneno haya yameongezwa ili kuhamisha ujumbe linganifu kati ya MC na ML kwa kudhihirisha hofu aliyokuwa nayo Mikono Mirefu alipokuwa anamjibu mwalimu.

Itchy Fingers passed a stiff hand across his eyes and muttered *woodenly*, “I can’t remember...”

(*Moses and the Ghost*, uk. 33)

Mikono Mirefu alipitisha mikono mbele ya macho yake na *kusema kwa uthabiti*, na kwa sauti ya chini, “Sikumbuki...”

(*Musa na Pepo*, uk. 33)

MC imetumia istiari *purer souls* kuwarejelea wanafunzi wengine ambao hawajachafuliwa na uovu wa Musa na wenzake wa Bweni nambari ya 2. Istiari hii imetafsiriwa kwa kisawe cha istiari katika LL. Istiari yenyewe ni *malaika*. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (2004) ya Oxford malaika ni kiumbe kisichoonekana ambacho kinasadikiwa kuwa kimeumbwa na Mungu kwa nuru. Inaaminiwa kuwa kiumbe huyu ambaye ni mjumbe wa Mungu ni mtakatifu na wala hana hatia.

Istiari hii ingehifadhiwa kwa tafsiri ya neno kwa neno kuwa *roho safi*. Tukizingatia muktadha wa matumizi ya istiari hii katika MC, tafsiri hii ingepotosha ujumbe wa MC

kwa hivyo kumtatiza msomaji wa ML. Kipengee cha usanii kingepotea na tafsiri ikapoteza mnato wa kifasihi.

Meanwhile, we were to remain completely segregated from the rest of the school (incase, I imagine, some of our rottenness rubbed off on to *purer souls*), studying and having our meals in the dormitory.

(*Moses and the Ghost*, uk. 35)

Wakati huohuo, iliamuliwa kwamba tutatengwa na wanafunzi wengine (nadhani kwa sababu ilidhaniwa kuwa tungewaambukiza *malaika hao uovu wetu*). Tulipaswa kusoma na kulia chakula chetu kwenye bweni.

(*Musa na Pepo*, uk. 35)

*Picture of guilt* ni istiari iliyotumiwa kueleza alivyoonekana King Kong mbele ya Musa na naibu wa mwalimu mkuu Bwana Karanja. King Kong alikuwa amewagonganisha vichwa wale wanaume wawili wakapoteza fahamu. Wanaume hawa walikuwa wameandamana na Joe (ambaye alikuwa pepo) na wao ndio waliokuwa wamempa Joe kazi ya kuisumbua shule akiwa pepo mpaka wanafunzi wawaombe wazazi wao wawaondoe katika shule hiyo. Walikuwa na azma ya kuinunua shule hiyo na kwa hivyo walikuwa wanatafuta mbinu yoyote ambayo ingewawezesha kuuziwa shule hiyo.

Kitendo cha kuwagoganisha vichwa wale wanaume kilifanyika nje ya uga wa shule. Hapo awali Bwana Karanja alikuwa amewaonya wanafunzi dhidi ya kumgusa ye yote nje ya uga wa shule. Hii ndiyo sababu King King hakuweza kuficha dalili za mtu mwenye hatia.

Istiari, *picture of guilt* imetafsiriwa kwa kisawe cha kiufafanuzi ambacho ni *Uso wa King Kong ulionyesha ishara ya mtu mwenye hatia*. Ufafanuzi huu umewezesha kuwasilisha ujumbe wa MC kwa ML ingawa ufundi wa kisanaa amba ni sifa mojawapo ya kazi za kifasihi umepotea. Itakumbukwa kuwa kazi ya kimsingi ya mtafsiri ni kuwasilisha ujumbe wa MC kwa ML (Newmark, 1988). Hivi ndivyo matini zinavyosema:

The bundles were the two men, and if they weren't exactly unconscious, they were certainly stupefied. "Gosh! What on earth are you doing?" I

cried. and behind me, Mr Karanja called, “What’s going on here?” King Kong was the *picture of guilt*. He looked at Itchy Fingers who, of course, was reduced to a jelly. However, it was Itchy Fingers who answered.

(*Moses and the Ghost*, uk. 80- 82)

Vifurushi hivyo vilikuwa wanaume wale wawili. Kama hawakuwa Wamepoteza fahamu, bila shaka walikuwa wameduwaa kuduwa. “Salaale! Mnafanya nini?” nikauliza kwa mshangao. Nyuma yangu, Bw Karanja naye akasaili, “Ni nini kinaendelea hapa?” *Uso wa King Kong ulionesha ishara ya mtu mwenye hatia*. Alimtazama Mikono Mirefu ambaye, bila shaka alikuwa ameganda kwa woga. Hata hivyo, Mikono Mirefu ndiye aliyejibu.

(*Musa na Pepo*, uk. 80-82)

Istiari nyingine katika MC ni *reduced to a jelly* iliyotumiwa kuelezea hali ya woga aliokuwa nao Mikono Mirefu kutokana na kugonganishwa vichwa na kuumizwa kwa wale wanaume wawili nje ya uga wa shule na King Kong. Istiari hii imefafanuliwa katika matini tafsiri kuwa *ganda kwa woga*. Ufafanuzi huu umeweza kuhamisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa MC kutegemea muktadha husika. Tunapata yafuatayo katika matini:

“Gosh! What on earth are you doing?” I cried. And behind me, Mr Karanja called, “what’s going on here?” King Kong was the picture of guilt. He looked at Itchy Fingers who, of cause , was reduced to *a jelly*. However it was Itchy Fingers who answered.

(*Moses and the Ghost*, uk. 80 -82)

“Salaale! Mnafanya nini?” nikauliza kwa mshangao. Nyuma yangu Bw Karanja naye akasaili, “Ni nini kinaendelea hapa? *Uso wa King Kong ulionesha ishara ya mtu mwenye hatia*. Alimtazama Mikono Mirefu ambaye, bila shaka alikuwa *ameganda kwa woga*. Hata hivyo, Mikono Mirefu ndiye aliyejibu.

(*Musa na Pepo*, uk. 80- 82)

Tunapata katika MC kuwa Rukia alipoulizwa na Musa kama alikuwa na habari kuhusu mgomo wa wapishi, aliyazungusha macho yake na kutazama angani. Yafuatayo ndiyo yaliyosemwa:

“Oh, so you know about the strike,” I said. “Know about it?” Rukia rolled his eyes towards *heaven*. “Man, we’ve felt it! You and King Kong were wise to give the dining hall a miss at lunchtime. The rest of us sat down to bread and water – plus a soul-stirring talk by Mr Karanja on how to make the best of things in an emergency!”

(*Moses in Trouble*, uk. 6)

“Ahaa, kwa hivyo unajua habari za mgomo,” nilisema. “Kujua kuuhusu?” Rukia aliyazungusha macho yake na *kuangalia juu*. “Aisee tumekipata! Wewe na King Kong mlikuwa werevu kulikwepa bwalo wakati wa chamcha. Tumekula mkate na maji – pamoja na mashauri ya Bw Karanja kuhusu namna ya kuishi vyema wakati wa dharura!”

(*Musa Mashakani*, uk. 7)

Maneno *towards heaven* yametumika katika MC kama istiari kuonyesha hali ya kutamauka kwa Rukia kutokana na chakula yeye na wanafunzi wenzake walichokula na kile wanachotarajia kula kufuatia hali ilivyo shulenii. Neno *heaven* linamaanisha mbinguni ambapo ni makao yake Mwenyezi Mungu. Kuangalia mbinguni kwa Rukia ni kama ishara ya kuomba rehema zake Mungu. Istiari hii imehifadhiwa kwa kuhamishwa kutoka MC hadi ML kuwa *kuangalia juu*. Ingawa neno *juu* limehamisha ujumbe wa MC kwa ML, kwa kiwango fulani limepunguza ujumbe wa MC kwa kupoteza uzito wa *heaven* katika MC. Tafsiri ya moja kwa moja ingefaa zaidi katika muktadha huu. Hata hivyo, kwa kuwa kazi ya mtafsiri ni kuhamisha ujumbe linganifu wa MC kwa ML, tafsiri hii imefaulu kwani kuna uwiano mkubwa baina ya MC na ML. Itakumbukwa kuwa ulinganifu si sawa na usawa bali ni aina ya uwiano.

*Top dogs* ni istiari katika MC. Imetumiwa na Musa kueleza namna ambavyo wavulana wa Bweni nambari 3 wangetia fora katika upishi pale shulenii kama King Kong angekumbuka mambo aliyofunzwa kuhusu upishi alipokuwa amejiriwa kama mfanyakazi wa jikoni. Istiari *top dogs* imetafsiriwa kwa ufanuzi kuwa *kuwa mabingwa*. Ingawa kipengee cha sanaa kimedidimia, ujumbe wa MC kwamba vijana

wa Bweni nambari ya 3 wangetambulika shulenii kuwa wapishi bora zaidi umehifadhiwa. Hivi ndivyo alivyosema Musa:

“Well, if you must know, I once ran away from home and took a job as a kitchen boy. At the end of a month of washing dishes and scrubbing floors, I decided that life was more comfortable in my father’ house. Still the cook at the house where I worked taught me plenty of useful things, and I don’t think I’ve forgotten all of them.” “Try to remember everything,” I cried, “Won’t we be *top dogs* in the school if our dorm prove to be the best cooks!”

(*Moses in Trouble*, uk. 13)

“Kwa taarifa yako, niliwahi kutoroka nyumbani wakati mmoja, nikaajiriwa kama mfanyakazi wa jikoni. Baada ya kuosha vyombo na kusugua sakafu mwezi mmoja, niliamua kuwa maisha yalikuwa bora zaidi nyumbani kwa babangu. Hata hivyo, aliyekuwa mpishi katika nyumba niliyokuwa nikifanya kazi alinifunza mambo mengi muhimu, na sidhani kama nimeyasahau yote.” “Jaribu kukumbuka kila kitu,” nilimsihi. “Huoni tutakuwa *mabingwa* shulenii iwapo bweni letu litathibitisha kuwa na wapishi bora zaidi?”

(*Musa Mashakani*, uk. 14)

Katika MC *stinging pain* ni istiari. Istiari hii imetumiwa kutilia mkazo maumivu waliyopata Musa na King Kong kutokana na viboko walivyocharazwa na Bwana Karanja. Wanasema hivi:

Everything was over in a few minutes, but the *stinging pain* of the strokes he gave us lingered on for the rest of the afternoon.

(*Moses in Trouble*, uk. 18)

Kila kitu kilikwisha baada ya dakika chache, isipokuwa *uchungu wa viboko* tulivyocharazwa uliobaki nasi alasiri nzima.

(*Musa Mashakani*, uk. 18)

#### **4.4.5 Mkakati wa Kuifutilia Mbali Istiari**

Istiari inaweza kutafsiriwa kwa kufutiliwa mbali iwapo utendakazi wake unatekelezwa na tamathali nyingine. Tamathali inapokaririwa katika matini huwachosha wasomaji wake. Ili kuzuia hali hii, mtafsiri huiondoa sehemu nyingine kwenye matini. Mkakati huu haujatumika katika tafsiri za *Musa na Pepo* (2013) na *Musa Mashakani* (2013).

Kwa kuwa mtafsiri ni msanii, anaweza kuibua mikakati mpya ambayo inamfaa katika kuhamisha baadhi ya istiari. Kwa mfano: Istiari ‘fish face’ imetumiwa katika MC. Istiari hii imetumiwa na King Kong wakati wanafunzi hasa Musa, Mutagubya, Rukia na King Kong walipokuwa wakimhoji Joe kuhusu yeye (joe) kuiga pepo. Ni baada ya King Kong kumjuza Joe kuwa alittambua sauti yake walipokuwa wakibishana na Kintu na Mulabi. Yafuatayo ndiyo yaliyosemwa katika matini:

“Anyway, Joe, I recognized your voice while you were arguing with those two men on the night we caught you,” King Kong said. At least, I knew I had heard it before. I bet I would have put a name to it if Holy Moses hadn’t rushed me so.” “**Oh jug it, fish face,**” I told him, and asked Joe how he was getting on in his new job.

(*Moses and the Ghost*, uk. 90)

“Hata hivyo, Joe, niliitambua sauti yako ulipokuwa ukibishana na wale wanaume wawili usiku ule tuliokekamata,” King Kong akasema. “Nilijua kwamba nilikuwa nimewahi kuisikia sauti hiyo awali. Nina hakika kwamba ningelitaja jina lako iwapo Musa Mtakatifu hangeniharakisha.” “*Oh, jug it, fish face!*” nikamwambia kasha nikamwuliza Joe kuhusu kazi yake mpya.

(*Musa na Pepo*, uk. 92)

Istiari *fish face* imehamishwa bila kutafsiriwa ila imeandikwa kwa herufi za mlazo. Maana ya istiari hii haijulikani katika muktadha huu na labda hii ndiyo sababu yake kukosa kutafsiriwa. Aidha, kutotafsiri istiari hii kimakusudi na mtafsiri kumeiwezesha ML kuibua athari sawa kwa msomaji wake na ile ya MC kwa msomaji wake.

## **4.5 Mikakati ya Kutafsiri Tashbihi**

Mtafsiri hana budi kuchagua kwa makini mikakati mwafaka ya kutafsiri tashbihi ili kuweza kuhamisha ujumbe kwa njia ambayo haitatizi mawasiliano. Katika sehemu inayofuata mikakati iliyotumiwa kutafsiri tashbihi imefafanuliwa :

### **4.5.1 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Kuzihifadhi**

Musa alikuwa na mawazo mengi kufuatia kisa kilichosimuliwa na Mikono Mirefu kuhusu shule yao kuwa na pepo. Kwa hivyo, ye ye pamoja na wawulana wenzake wanapoingia vitandani kulala usingizi unampaa. Tashbihi *for what seemed like centuries* imetumika kulinganisha urefu wa muda aliokaa Musa bila kupata usingizi na karne kadha. Karne ni kipindi kirefu cha miaka mia moja. Tashbihi hii imetumiwa kusisitiza urefu wa muda aliokaa Musa bila kuiwa na usingizi.

Tashbihi hii imetafsiriwa kuwa *kwa muda mrefu niliouona kuwa mrefu sawa na karne*. Ingawa dhana ya *karne nyngi* kama inavyojitokeza katika MC imepunguzwa kuwa *karne moja*, ujumbe linganifu umehamishwa kutoka MC hadi ML bila utata wowote. Ulingenifu si sawa na usawa bali ni aina ya mfanano (Nida, 1964). Anasema hivi:

Nevertheless, sleep didn't come as easily as I expected. I was more wide awake than I had been all day. Every night noise was sharp and clear. The insects tinkling away outside, the rustle of lizards, in the thatched roof, the creak of beds as some of the others moved in their sleep, their breathing, and King Kongs rattling snore. *For what seemed like centuries*, I tossed and turned, and even smoked the cigarette stub I had meant to save until Saturday afternoon.

(*Moses and the Ghost*, uk. 6)

Hata hivyo, usingizi haukunijia haraka kama nilivyotarajia. Nilikaa macho zaidi kuliko nilivyokuwa mchana kutwa. Kelele yoyote hata ile ndogo kabisa ilisikika bayana usiku huo. Niliweza kusikia milio ya wadudu nje na michakato ya mijusi kwenye paa la nyasi la bweni letu. mkerezo wa vitanda pia ulisikika wakati baadhi ya wale waliokuwa usingizini walijigeuza kutoka ubavu mmoja hadi mwengine. Niliweza kusikia pia

mipumuo yao pamoja na mkoromo wa King Kong uliosikika kama ule wa chura. Nilijigeuza kitandani kwa muda mrefu *niliouona kuwa mrefu sawa na karne*. Hata ikanibidi kukivuta kile kibiri nilichodhamiria kukihifadhi hadi alasiri ya Jumamosi.

(*Musa na Pepo*, uk. 6)

Musa anaona kana kwamba wanafunzi wengine wote walikuwa katika usingizi wa pono. Yeye tu ndiye aliyekuwa macho wakati Bw Lutu alipofika kufanya ukaguzi wa bweni usiku huo. Tashbihi *I still lay there feeling like the only living person in the world* imetumiwa kudhihirisha hali hii. Tashbihi hii imehifadhiwa katika matini tafsiri kuwa ... *huku nimejilaza hapo nikihisi kana kwamba ndimi pekee niliyekuwa hai duniani*. Kuhifadhiwa kwa tashbihi hii kumewezesha uwasilishaji wa ujumbe wa MC kwa ML kwa jinsi iliyo wazi na isiyomtatiza msomaji wa ML. MC inasema hivi:

Mr Lutu came and went on his nightly dormitory check, and *I still lay there feeling like the only living person in the world*.

(*Moses and the Ghost*, uk. 6)

Bw Lutu alifika na kufanya ukaguzi wa bweni usiku huo, ilivyokuwa kawaida yake, huku *nimejilaza hapo nikihisi kana kwamba ndimi pekee niliyekuwa hai duniani*.

(*Musa na Pepo*, uk. 6)

*...he could run like the wind* ni tashbihi ambayo imetumiwa katika MC. Tashbihi hii imetumiwa kueleza mwendo wa yule pepo aliyekuwa akiwasumbua wanafunzi na shule nzima. Kasi ya yule pepo inalinganishwa na kasi ya upepo. Upopo huenda kwa kasi sana na kwa hivyo kufananisha mwendo wa pepo na mwendo wa upepo kunatoa picha halisi ya namna pepo yule alivyotimua. Tunaambiwa katika MC kwamba pepo lilikimbia kwa njia ambayo haikulidhihirisha kuwa pepo likatoweke. Hivi ndivyo MC inavyosema:

He raced straight at the ghostly figure who turned for a second to stare at King Kong, dropped the jembe, grabbed the flowing folds of his kanzu and sprinted in a most unghostly fashion past the San and out of sight. I chased after him, leaving King Kong to do a wild war-dance across the

main compound and ignoring the screeches now issuing from Miss Namukasa's room. One thing I will say for that ghost, *he could run like the wind* when the spirit moved him. It was only after I had passed the San and was crossing the bit of spare ground separating it from the kitchen store that I again caught sight of him in full flight.

(*Moses and the Ghost*, uk. 22-24)

King Kong alikimbia kuelekea lilikokuwa gimba lile ambalo leligeuka kwa muda wa sekunde moja kumwangalia King Kong. Halafu, lilidondosha jembe, likashikilia mapindo ya kanzu yake yaliyokuwa yakielea, na kwa namna isiyoonyesha 'upepo' wowote, likakimbia kuelekea kwenyezahanati na kutoweka machoni petu. Nilifuata na kumwacha King Kong afanye sarakasi zake kwenye uga wote wa shule pamoja na kupuuza kamsa zilizokuwa zikitoka chumbani mwa Bi Namukasa. Jambo moja ninaloweza kusema kumhusu pepo huyo ni kwamba, *aliweza kukimbia kwa kasi ya upepo uvumao wakati wa kimbunga*. Ni baada ya kuipita zahanati huku likivuka uwanja ulioitenga na ghal ya shule ambapo niliweza kuliona tena gimba lile likitimua mbio kama farasi.

(*Musa na Pepo*, uk. 22-24)

Katika matini tafsiri, istiari *he could run like the wind* imetafsiriwa kuwa *aliweza kukimbia kwa kasi ya upepo uvumao wakati wa kimbunga*. Tafsiri hii imehamisha ujumbe wasilifu wa MC kwa ML. Aidha ubunifu wa mtafsiri umejidhihirisha anapoiongezea tashbihi hii maneno, *uvumao wakati wa kimbunga*. Kimbunga huwa upepo ulio mkali sana na unaoenda kwa kasi sana. Kwa hivyo kuongezea maneno haya kumechangia kuweka wazi zaidi ujumbe wa MC kwamba pepo huyo alienda kwa kasi sana.

Katika kutilia mkazo kasi aliyogeuka nayo yule pepo, tashbihi, *like lightning* imetumiwa katika MC. Tunapata katika MC:

The ghost nearly had a fit. He jiggled for a moment on his feet, not knowing, which way to turn, then *like lightning* made a sideways move

which took us by surprise, nipped neatly between Okot and Sempa, and bolted round another corner.

(*Moses and the Ghost*, uk. 24)

Nusura pepo huyo ashikwe na kifafa. Aliyumbayumba kwa muda, asijue pa kutorokea. Kisha, *kwa kasi ya umeme*, alisonga ubavuubavu-hatua ambayo hatukuitarajia –akajipenyeza katikati ya Okot na Sempa na kupiga kona nyingine.

(*Musa na Pepo*, uk. 24)

Kasi ya umeme haiwezi kulinganishwa na kasi yoyote ile. Kasi ya pepo yule inapofananishwa kasi ya umeme inatuwezesha kupata picha kamili ya namna ambavyo huyo pepo alivyogeuka bila ya kutarajiwa na Musa na wenzake. Kwa hivyo kuhifadhi tashbihi hii kumehamisha ujumbe linganifu wa MC.

Wanafunzi wa Taasisi ya Mukibi wamekuwa pamoja katika shule hii kwa muda. Wamezoeana sana hivi kwamba wanalionna jambo gumu sana kwao kupata shule nyingine ambayo ingewachukua wote na kwa pamoja ikiwa Taasisi ya Mukibi ingeuzwa. Kusikia kwamba shule hiyo ilikuwa inauzwa kuliwasononesha sana. Tashbihi like *orphans in a storm* imetumiwa kuelezea hali hii. Tunapata katika MC:

There's no denying that Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen is a wretched place, yet in a way I suppose it means more to us than we ever realize. To learn so suddenly that it was being sold over our heads left us *feeling like orphans in a storm*. Nobody can claim to have any love for Old Mukibi himself, and indeed there is very little exchange of loyalties.

(*Moses and the Ghost*, uk. 38)

Sikatai kwamba *Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen* ni pahali pasipopendeza, lakini kwa namna fulani nadhani ni pahali muhimu sana kwetu kuliko tunavyopatambua. Kusikia ghafla hivyo kwamba shule hii ilikuwa inauzwa bila ya sisi kujua, kulituacha *tukisononeka na kujihisi kama mayatima katika dhoruba kali ya maisha*.

Hakuna aliyezeza kudai kumpenda Mzee Mukibi mwenyewe, na kwa hakika kulikuwa na kiwango kidogo sana cha uaminifu baina yetu na yeye.

(*Musa na Pepo*, uk 38)

Wanafunzi wanahisi kwamba ikiwa shule yao ingeuzwa wangeachwa bila yejote wa kuegemea wala kumtegemea kama mtoto anavyoachwa anapoondokewa na wazazi. Ingawa shule yenyewe haipendeki uhusiano wao ni muhimu sana kwao. Tashbihi hii imehifadhiwa katika ML kuwa *tukisononeka na kujihisi kama mayatima katika dhoruba kali ya maisha*. Ujumbe wa MC umezidishwa kwa kuongezea tashbihi hii neno *kusononeka*. Hata hivyo neno *kusononeka* linaongezea uzito magumu wanayopitia watoto wanapoachwa bila wazazi; jambo ambalo linatilia mkazo ujumbe wa MC na pia kudhihirisha ubunifu wa mtafsiri katika kuhamisha ujumbe wa MC. Kuuzwa kwa Taasisi ya Mukibi kungewaacha wanafunzi wake katika hali ngumu sana. Wanaona kwamba ingekuwa vigumu sana kwao kusoma pamoja na wanafunzi ambao hawajapitia magumu kama vile kutimuliwa kutoka shule moja hadi nyingine na wanaodaiwa kuwa waitiifu.

*As flat as a pancake* ni tashbihi ambayo imetumiwa katika MC. Tunaelezwa katika MC kwamba gari lilikuwa mahali ambapo lilikuwa limeegeshwa lakini lilikuwa limejiinamia. Sababu ya kujiinamia huku ni kwamba magurudumu yalikuwa yametolewa pumzi yakawa bapa kabisa hivi kwamba gari halingeweza kuondoka mahali pale. Ubapa wa magurudumu unalinganishwa na *Pancake* katika MC. Pancake na chapati husawiana sana kwa umbo. Tofauti iliyoko tu ni jinsi ya kutengeneza. Katika ML tashbihi *as flat as a pancake* imetafsiriwa kuwa *bapa mithili ya chapati*. Mwandishi wa MC anatumia tashbihi hii kusisitiza jinsi ilivyokuwa vigumu kwa lile gari kuondoka mahali lilipokuwa limeegeshwa. Kutafsiri tashbihi kwa kuihifadhi kumewasilisha ujumbe huu kwa ML kwa njia nzuri isiyomtatiza msomaji wa ML.

He hobbled along behind, while we hurried as fast as we could to the place where the men had parked the car. It was still standing where King Kong and I had last seen it, only it seemed lower and squatter. I soon realized why. Each of its four tyres was *as flat as a pancake*. Mr Karanja frowned

and said, “I hope these flat tyres are an Act of God, and not the work of an overenthusiastic boy.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 80)

Gari hilo bado lilikuwa limeegeshwa mahali ambapo mimi na King Kong tulikuwa tumeliona mara ya mwisho, ila tu lilionekana limejiinamia. Hatimaye nilijua sababu; magurudumu yake yote *yalikuwa bapa mithili ya chapati*. Bw Karanja alikunja uso na kusema, “Ninatumai ubapa wa magurudumu hayo umetokana na kitendo cha Mungu, wala si kazi ya mvulana mwenye msisimko uliopita mipaka.

(*Musa na Pepo*, uk. 80)

Tunapata katika MC tashbihi *We stared like frightened rabbits* ambayo imehifadhiwa katika ML kuwa *Tuliyakodoa macho kama sungura waliotishwa*. Bw Mukibi hakuwa na mazoea ya kulizuru bwalo la shule. Wanafunzi wanapomwona akiingia bwaloni wanajua lazima kuna jambo. Aidha maumbile ya mwalimu mkuu kama yanavyofafanuliwa katika matini yanatisha. Kila mwanafunzi ana hamu ya kujuu kilichomleta mwalimu mkuu na kwa hivyo hakuna haja ya kuwanyamazisha; kila mtu alikomesha alichokuwa akifanya na kusubiri kwa hamu kuu kusikia yaliyojiri. Kiwewe walichokuwa nacho wanafunzi ndicho kinachofananishwa na wasiwasi wanaokuwa nao sungura waliotishwa. Ujumbe huu umewasilishwa kwa njia wazi katika ML kwa kuihifadhi tashbihi. Matini zinasema hivi:

Then one morning our headmaster, Mr Mukibi made one of his rare appearances in the school dinning hall. There was no need for Mr Karanja, our deputy head, to rap sharply on the table for silence, since we all stopped eating and talking the moment the old vulture darkened the doorway. *We stared like frightened rabbits* at the tall, gaunt figure with hooded eyes, wrinkled, sagging cheeks, and a tight, cruel mouth, to whose care our loving families had so willingly entrusted us.

(*Moses in Trouble*, uk. 1-2)

Asubuhi moja, mwalimu mkuu wetu, Bw Mukibi, alifanya mojawapo ya ziara zake za nadra katika bwalo. Hapakuwa na haja ya Bw Karanja, naibu wa mwalimu mkuu, kugongagonga meza ili kunyamazisha. Sote tulisitisha

kula na kuzungumza pindi tu tai yule mkongwe alipozuru pale. *Tuliyakodoa macho kama sungura waliotishwa tukiyatazama maumbile ya kutisha ya yule mzee.* Alikuwa kifyefye, mrefu, mweusi, mwenye macho makubwa na mashavu yaliyoning'inia kwa sababu ya makunyanzi mbali na kuwa na kinywa kilichotoa maneno makali.

(*Musa Mashakani*, uk. 1)

Tashbihi *like whirlwind* imetumiwa katika MC. Tashbihi hii imetumiwa kufafanua namna ambavyo King King alivyokuwa akizunguka ndani ya kile chumba walimokuwa wavulana wa Bweni nambari 2 akiwa na hasira kubwa. Kulingana na Oxford *Learner's Dictionary* (2010), Whirlwind ni upopo wenyewe nguvu unaovuma kwa kuzungukazunguka kwa kasi ambao husababisha madhara. Katika matini tafsiri, tashbihi hii imetafsiriwa kuwa *kama chamchela*. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) ya Oxford chamchela ni upopo mkali unaovuma na kuleta maafa. Maana za tashbihi hizi zinawiana katika MC na ML. Tunapata katika MC:

“Look here, King Kong, you’d better leave us alone!” Ssali, the dorm 2 prefect, cried, but King Kong was in no mood to listen to threats. He charged round the small room *like whirlwind*, knocking plates out of hands whenever he failed to empty them on somebody. In a matter of seconds, the storeroom looked like the inside of a dustbin, and all of us, including King Kong himself, were either plastered or splashed with sweet potato, gravy and meat.

(*Moses in Trouble*, uk. 14)

“Sikiliza, King Kong, Tunaomba utukome!” Ssali, kiranja wa Bweni nambari ya pili, akasema. Hata hivyo, King Kong alitia masikio yake nta na kupuuza vitisho vyake. Alikizunguka chumba kile kidogo kwa *fujo kama chamchela* huku akigonga na kuangusha sahani kutoka mikononi mwao pale alipokosa kumwagia mtu chakula. Katika sekunde chache ghalia ile ilionekana kama jaa. Sote, akiwemo King Kong, ama tulikuwa tumepakwa viazi vitamu au kumwagikiwa na mchuzi wa nyama na hata nyama zenyewe.

(*Musa Mashakani*, uk. 15)

Kuhifadhi tashbihi hii, kumerahisisha uelewaji wa ujumbe wa MC katika ML kwa kuwa tashbihi hizi mbili zina athari sawa kwa wasomaji wake.

*Swift as an arrow* ni tashbihi ambayo imetumiwa katika MC kuelezea namna Musa alivyokimbia ili kujinusuru kutoka kwa wale wanaume waliokuwa wakimwandama. Tashbihi hii imehifadhiwa katika ML kuwa kasi kama mshale. MC inasema hivi:

As he shouted, I broke free from his grasp and took to my heels. The noise of the two hungry people following me was enough to send me flying through the shamba, *swift as an arrow*. I bumped into trees, I tripped over stones and plants, but I still kept on running, even when I was convinced my lungs would burst.

(*Moses in Trouble*, uk. 27)

Alipokuwa akiongea kwa sauti, nilijinasua kutoka mikononi mwake na kutoroka. Kelele za watu wawili waliokuwa na hasira, ambao walikuwa wakiniandama, zilitosha kunifanya nikimbie *kwa kasi kama mshale* shambani pale. Licha ya kuwa niligonga miti na kujikwaa kwenye mawe na mimea, au hata nilipokuwa na hakika ya mapafu yangu kupasuka, bado niliendelea kukimbia.

(*Musa Mashakani*, uk. 27)

Tafsiri hii imehamisha ujumbe wa MC kwa njia rahisi na ambayo haimtatizi msomaji wa ML.

Katika MC tunapata tashbihi *I slept like a log*. Katika ML tashbihi hii imetafsiriwa kuwa *nililala kama gogo*. Tafsiri hii imehamisha ujumbe ulio wazi kwa ML kwamba Musa alilala usingizi wa pono licha ya furaha na njaa aliyokuwa nayo kwa muda mrefu. Matini zinasema hivi:

The four of us were still in this subdued state when we said ‘goodnight’ and climbed thankfully into our beds. The other boys were already fast asleep, but I noticed a heap of tired-looking sugarcane behind the door. Despite so much excitement and my constant hunger, *I slept like a log*.

(*Moses in Trouble*, uk. 69)

Sote wanne tulikuwa tungali katika hali hiyo ya kimya tulipoambiana ‘Alamsiki’ na kuingia vitandani mwetu. Wale wavulana wengine tayari walikuwa wamelala fofofu, ingawa nilikiona kitita cha miwa nyuma ya mlango. Licha ya furaha kuu na njaa ya muda mrefu niliyokuwa nayo, *nililala kama gogo*.

(*Musa Mashakani*, uk. 70)

#### **4.5.2 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Dhana**

Mkakati huu unaweza kutumiwa na mtafsiri pale ambapo kisawe cha kitashbihi kinapokosekana. Hata hivyo mtafsiri hana budi kuzingatia maana ya kimuktadha. Dhana inayotumika lazima idhihirishe maana ya tashbihi inayotafsiriwa. Kwa mfano, “It’s body was as cold as ice”. Tashbihi hii ikitafsiriwa kwa dhana itakuwa “Mwili wake ulikuwa baridi sana.” Mkakati wa kutafsiri tashbihi kwa dhana hutumiwa mtafsiri anapokosa kisawe cha tashbihi ambacho kinaoana na muktadha.

Tashbihi *as much amused as interested* imetumiwa katika MC. Tashbihi hii imetumiwa kufafanua hisia za wavulana wa Bweni nambari 2 kuhusu masaibu yaliyowapata wavulana wa Bweni nambari ya 3. Masaibu ambayo yamewakumba wavulana wa Bweni nambari ya 3 yamewasisimua sana wavulana wa Bweni nambari ya 2. Hii ni kwa mujibu wa wavulana wa Bweni nambari ya 3. Matini zinasema hivi:

“I bet they are laughing their heads off at the thought of our dorm getting the blame,” I said bitterly. Rukia nodded, “Yes, I noticed this morning *how they were as much amused as interested* in what happened to us.”

(*Moses and the Ghost*, uk. 17)

“Nina hakika wanavunjika mbavu kwa vicheko kuona kuwa bweni letu ndilo liliolekezwa lawama,” nikasema kwa uchungu. “Ndio. Leo asubuhi, *nilionna jinsi walivyofurahishwa* na masaibu yaliyotupata,” Rukia alikubaliana nami.

(*Musa na Pepo*, uk. 17)

Katika tafsiri hii, ujumbe linganifu wa MC umehamishwa kwa njia nyepesi na rahisi kueleweka kwa msomaji wa ML. Hata hivyo kukosa kuitafsiri tashbihi hii kwa kisawe cha kitamathali kumepunguza kwa kiwango fulani ladha ya kisanaa ambayo ni muhimu katika kazi za kifasihi.

Katika MC, tunapata maelezo ya Musa kumhusu pepo kuwa tashbihi; *the Ghost is about as ghostly as I am*. MC inasema hivi:

“It was horrible,” Itchy Fingers repeated. I was coming back from the Village, taking the Sneaker’s Path off the main road – and it was there – the ghost! It suddenly sprang out of some bushes and dashed straight past me!” “Is that all?” Considering past events, I thought this a very feeble tale. “Well, we’ve got news for you. *The ghost is about as ghostly as I am* and can run faster and,

(*Moses and the Ghost*, uk. 30- 32)

“Alikuwa anaogofya,” Mikono Mirefu alikariri. “Nilikuwa ninarudi shulen i kutoka kijijini, kupitia Ujia wa Wahepaji kando ya barabara kuu – naye alikuwa hapo – yule pepo! Aliruka ghafla kutoka vichakani na kunipita mbio! “Ni hayo tu?” nilimuuliza. Kwa kurejelea matukio ya hivi karibuni, masimulizi hayo hayakuwa ya kutilia maanani. “Mmmh tuna jambo la kukuarifu. *Pepo huyo ni binadamu jinsi nilivyo na ana uwezo wa kukimbia kwa kasi zaidi, lakini la mno ni kwamba,...*”

(*Musa na Pepo*, uk. 32)

Katika muktadha huu, pepo analinganishwa na binadamu, kumaanisha kwamba ubinadamu alio nao huyu pepo umeupiku ‘upepo’ alio nao. Kwa hivyo yeye ni kama binadamu wa kawaida. Tafsiri hii kwa kisawe cha kidhana imehamisha ujumbe wa MC ila sifa ya kisanaa imepotea. Nia ya kimsingi ya tafsiri ni kuhamisha ujumbe linganifu kutoka MC hadi ML (Nida, 1964).

Katika MC, muda baina ya kuonekana kwa wale wanaume wawili waliokuwa na wasiwasi mwingi na kuja kwa mwanamume wa tatu ulionekana kama kwamba

ulikuwa mrefu sana kwa wavulana waliokuwa wakiwavizia. Tunapata yafuatayo katika MC:

...The footsteps came nearer, and a few yards away from us, two men came and stood as though they were waiting for somebody. They spoke to each other in undertones and we failed to recognize them, but they were obviously very agitated because they frequently glanced at the luminous dials of their watches. *After what seemed like hours*, there was a further sound of footsteps, this time hurried, and panting up the hill between the bushes came a tall man holding up the hem of his trailing kanzu with one hand and carrying a jembe in another.

(*Moses and the Ghost*, uk. 61-62)

...Michakato hiyo ilikaribia, wanaume wawili wakatokezea na kusimama kama ambao walikuwa wanamsubiri mtu fulani. Waliongea kwa sauti ya chini kiasi kwamba tulishindwa kuwatambua. Hata hivyo, walionekana kughadhabishwa na jambo fulani kwa namna walivyokuwa wakizitazama saa zao za mikononi. *Baada ya kipindi kilichoonekana kirefu*, kulikuwa na michakato zaidi, wakati huu ya harakaharaka iliyoandamana na kuhema kwa haraka kwa mtu aliyekuwa anakwea mlima. Punde alitokea mwanamume mrefu kama mlingoti ambaye alishikilia mpindo wa kanzu yake kwa mkono mmoja na kubeba jembe kwa mkono mwengine.

(*Moses and the Ghost*, uk. 61-62)

Tashbihi, *like hours* imehamishwa kwa dhana kuwa *kipindi kilichokuwa kirefu*. Tafsiri hii imehamisha ujumbe wa MC kwa ML kwa njia wasilifu kulingana na muktadha huu.

Bw Mukibi analalama kuhusu yeye kuachwa katika nyumba ambamo amefungiwa Joe kwenye stoo. Joe amekuwa pepo ambalo limekuwa likisumbua Taasisi ya Mukibi. Kwa kuwa kuna wavulana wawili ambao wamepotea katika harakati za kulisaka pepo, Bw Karanja anamhakikishia mwalimu mkuu kwamba ilibidi kuwatafuta wavulana wale. Katika hali hii, kulingana na Bw Karanja, lazima Bw Mukibi angeachwa

kwenye ile nyumba. *Bw Karanja alishikilia* ni dhana katika ML ambayo imetumiwa kutafsiri tashbihi, Mr Karanja was *crisp and businesslike*. Matini inasema:

“You’re are not leaving a sick old man in the house with that murderer locked in the store!” the headmaster quavered trying to look pathetic and only succeeding in being more revolting than usual.“There is no alternative I’m afraid, Sir,” *Mr Karanja was crisp and businesslike*. “It’s important that we find those boys.

(*Moses and the Ghost*, uk. 79)

“Hivi mnaniacha hapa nilivyo mgonjwa, tena na yule muuaji akiwa amefungiwa kwenye stoo?” mwalimu mkuu aliuliza. Ingawa alitaka kuonewa huruma aliishia kuonekana mwasi zaidi kuliko ilivyokuwa kawaida yake. “Samahani, Sir, hakuna njia nyingine, ”*Bw Karanja alishikilia*. “Ni muhimu tuwatafute wavulana hao.

(*Musa na Pepo*, uk. 79)

Wanafunzi wanapoanza kazi za jikoni, Musa na King Kong wanaamua kulikwepa bwalo wakati wa chakula cha mchana na kufululiza hadi kwa Mzee Kigali ili kumuarifu kuhusu yaliyokuwa yametokea shuleni. Wanampata Kigali akiwa na mengi ya kuwajuza hasa kuhusu mgomo wa wapishi. Tunapata yafuatayo katika MC:

At lunchtime, King Kong I avoided the dining hall and raced to the main entrance of the school to tell our great friend, Kigali, the old gatekeeper, what had happened. *We found Kigali as full of gossip as we were*. He almost dragged us inside his tinny grass hut,...

(*Moses in Trouble*, uk. 4)

Wakati wa chakula cha mchana, mimi na King Kong tuliliepuka bwalo na kufululiza hadi kwenye lango kuu la shule ili kumwarifu rafiki yetu mkuu, Kigali, yule bawabu mzee, kilichokuwa kimetokea. *Tulimkuta Kigali akiwa mwingi wa porojo na uvumi jinsi tulivyokuwa sisi*. Nusura atuvute ili kutuingiza ndani ya nyumba yake ya msonge.

(*Musa Mashakani*, uk 4-5)

Tafsiri hii ya kidhana imeuhamisha ujumbe wa MC kwa njia iliyowasilifu. Porojo aliyokuwa nayo Kigali ndiyo inayomfanya kutaka kuwawuta King Kong na Musa ndani ili aweze kupata nafasi ya kuwaeleza aliyokuwa nayo.

#### **4.5.3 Mkakati wa kutafsiri Tashbihi kwa Istiari**

Hii ni tafsiri ya kitamathali ambayo ikiwa itatumwa vizuri na mtafsiri hasa kwa kuzingatia maana ya kimuktadha inaipa lugha ladha ya kisanii. Mtafsiri hulazimika kutafuta kisawe cha kiistiari ambacho kinawasilisha maana ya tashbihi husika.

MC inafananisha namna ambavyo wavulana wa Bweni nambari ya 3 hasa Rukia, King Kong na Musa watakavyowachunguza wavulana wa Bweni nambari ya 2 na jinsi ambavyo mwewe huchunguza windo lake. Tashbihi katika MC inasema; *Tonight we'll watch them like hawks.* Tashbihi hii imetafsiriwa kwa kisawe cha kiistiari; *Leo usiku tutawapa jicho pevu* kumaanisha kwamba wangewachunguza kwa macho makali ambayo hayakosi kuona chochote. Tafsiri hii imewasilisha maana linganifu ya MC katika ML. Taswira inayowasilishwa katika MC ya jinsi wavulana wa Bweni nambari 2 wangechunguzwa inajitokeza katika ML katika istiari inayofananisha namna watakavyochunguzwa wavulana wa Bweni nambari 2 na kutazamwa kwa jicho pevu. Tunapata yafuatayo katika matini:

Rukia agreed with me. He thought it would be silly to pick a fight with them when we hadn't a shred of evidence.

"Anyway," he added, "we'll not take any risks. *Tonight we'll watch them like hawks.* If they are up to something, we'll soon find out what it is – then we'll have them!"

(*Moses and the Ghost*, uk. 17)

Rukia aliniunga mkono. Aliona kuwa ni upumbavu kuzozana nao bila ya kuwa na hata chembe ya ushahidi.

"Haidhuru, "akaongeza, "ni muhimu tuchukue tahadhari. *Leo usiku tutawapa jicho pevu.* Iwapo kuna jambo wanalodhamiria kulifanya tutaligundua hivi karibuni – na tutakuwa tumewanasa.

(*Musa na Pepo*, uk. 17)

Kunaswa kwa wavulana wa Bweni nambari 2 na wavulana wa Bweni nambari 3 kutatokana na kutazamwa kwa macho makali yasiyokosa, jambo ambalo linawasilisha maana ya MC kwa njia ya kitamathali.

Usiku ambao wavulana wa Bweni nambari 3 walilivamia shamba la mwalimu mkuu ulikuwa na giza totoro. MC inasema: but *the night was as black as ink*. Wanachuma matunda gizani bila ya kuonekana mpaka pale Musa anapoangukia majani ya minanasi yenyе miiba akapiga unyende. Hata mwanamume anayemkimbiza Musa anamgonga kwa kuwa hamwoni kutokana na giza. Istiari anayowasilisha maana ya tashbihi: *but the night was as black as ink* imetumiwa katika matini tafsiri. Istiari ambayo imetumiwa katika ML ni: lakini usiku huo ulikuwa *wenye giza la kaniki*. Istiari hii inaleta mnato wa kisanii katika ML pamoja na kuhamisha maana linganifu ya MC kwa njia yenyе mnato. Tunapata yafuatayo katika matini:

As he spoke we heard the pounding of feet and a warbled cry of alarm shrilled through the night. Picking up the prize pawpaw, I hastily followed my two friends as they made their getaway. I heard them crashing on ahead of me, and did my best to catch up with them, *but the night was as black as ink*. I wasn't at all familiar with Mr Mukibi's  
shamba ...

*(Moses in trouble, uk. 25)*

Alipokuwa akizungumza, tulisikia michakato na ukwenzi mkubwa uliotatiza kimya cha usiku ule. Huku nikiliokota papai lile la kipekee, niliwafuata kwa kasi marafiki zangu wawili waliokuwa wakitoroka.

Niliwasikia wakichuana na majani makavu mbele yangu. Nikajitahidi kadri ya uwezo wangu kuwafikia, *lakini usiku huo ulikuwa wenye giza la kaniki*, nami sikulifahamu vyema shamba la Bw Mukibi.

*(Musa Mashakani, uk. 26)*

#### **4.5.4 Mkakati wa Kutafsiri Tashbihi kwa Tashbihi yenyе maana sawa**

Tashbihi inaweza kutafsiriwa kwa tashbihi tofauti inayobeba maana ya kimuktadha. Tafsiri hii ya kitamathali huibua taswira bayana ya ujumbe uliokusudiwa na MC

katika mawazo ya msomaji wa ML kwa kutumia tashbihi inayooana na mazingira au utamaduni wake.

Tunapata katika MC tashbihi: *working like mad*. King Kong na Musa wanajaribu kwa uwezo wao wote kuwasukuma wanaume wawili ambao wamegonganishwa vichwa na King Kong wakapoteza fahamu ili wapate kuwaingiza ndani ya uga wa shule. Inawabidi kuwaingiza ndani ya uga wa shule kwa kuwa ilikuwa haramu kwao kuwapiga ua kuwakamata watu hao nje ya uga wa shule kwa mujibu wa Bw Karanja. Tashbihi: *working like mad* imehamishwa kwa tashbihi tofauti katika LL lakini inayowasilisha maana ya kimuktadha ya tashbihi hii. Tashbihi iliyotumiwa katika ML: *wakijitahidi kwa bidii ya mchwa inaibua picha dhahiri ya bidii ambayo King Kong na Mikono Mirefu walikuwa katika ile shughuli ya kuwavusha wanaume wale wawili*. Tunapata yafuatayo katika matini:

I raced down the track, following the sound of his voice, and everybody chased after me. Eventually I came to a little known part of the school boundary, the only portion fenced with barbed wire. King Kong and Itchy Fingers crouched there, *working like mad* to push through two bulky bundles. The bundles were the two men, and if they weren't exactly unconscious, they were certainly stupefied.

(*Moses and the Ghost*, uk 80)

Nilikimbia upande huo, nikifuata sauti yake. Kila mtu alinifuata nyuma. Hatimaye nilifika katika sehemu ya mpaka wa shule isiyofahamika sana. Ilikuwa sehemu ya pekee iliyozingirwa kwa seng'eng'e ambayo ilikuwa imeshika kutu. King Kong na Mikono Mirefu walikuwa wameinama hapo, *wakijitahidi kwa bidii ya mchwa kusukuma vifurushi viwili vikubwa ili kuvivusha hadi upande wa pili*.

Vifurushi hivyo vilikuwa wanaume wale wawili. Kama hawakuwa wamepoteza fahamu, bila shaka walikuwa wameduwaa kuduwaan.

(*Musa na Pepo*, uk 80).

Tashbihi: *The rats disappeared like magic* imetumiwa katika MC kuelezea kuwa panya hao walitoweka kwa njia ya kustaajabisha wakati Rukia, King Kong na Musa

walipoingia ghalani; yaani kufumba na kufumbua panya wote walikuwa wametoweka. Kutoweka huku kunafananishwa na kufanyika kwa jambo la kustaajabisha. Katika matini tafsiri kutoweka kwa panya hao kunalinganishwa na kutoweka kwa moshi wakati wa kimbunga. Ni muhali kwa moshi kuonekana kukiwa na kimbunga. Matini tafsiri inasema: *Panya walitoweka kama moshi kwenye upepo mkali*. Tafsiri hii inasawiri picha inayosawiriwa na MC kuhusu jinsi wale panya walivyotoweka. Tafuatayo yanapatikana katika matini:

I think the storeroom looked far worse by daylight than it looked at night, because darkness did a lot to hide its sagging thatched roof and crumbling walls. Aunt Damali would have fainted if anybody had suggested that she store her food in such a hole. We walked around it and soon realized that the only items in any quantity were rats and onion. *The rats disappeared like magic* when we entered, but the onions were spread out along the side of one wall.

(*Moses in Trouble*, uk. 36 - 37)

Nafikiri ghalia ilionekana bora zaidi mchana kuliko ilivyoonekana usiku. Giza lilisitiri mengi – paa lake lilijiinamia huku kuta zikiwa na nyufa. Shangazi yangu, Damali, angelizirai iwapo mtu angelimpendekezea ahifadhi chakula chake kwenye pango kama hilo. Tulizunguka ndani ya ghalia hiyo na punde tukagundua kwamba bidhaa pekee zilizokuwemo kwa idadi kubwa walikuwa ni panya na vitunguu. *Panya walitoweka kama moshi kwenye upepo mkali* wakati tulipoingia, ila vitunguu vilikuwa vimetapakazwa kando ya upande mmoja wa ukuta.

(*Musa na Pepo*, uk 37)

#### 4.6 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi (tashbihi, nahau na istiari). Katika tathmini ya mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali za usemi, ilibainika kuwa mikakati mbalimbali ilitumiwa kutafsiri kila mojawapo wa TU zilizoshughulikiwa.

Katika tafsiri ya nahau, ilibainika kuwa nahau nyingi zilihamishwa kupertia mkakati wa kiufafanuzi. Nahau nyingi ambazo zilitafsiriwa kwa mkakati huu zilihamisha ujumbe wa MC kwa njia wazi. Ni nahau chache mno ambazo zilitafsiriwa kwa kutumia mkakati huu ambazo hazikuhamisha ujumbe kwa njia iliyo wazi. Imebainika pia kwamba ni nahau chache zilitafsiriwa kwa mkakati wa kutafsiri nahau kwa nahau yenyе maana sawa lakini ikiwa tofauti kileksia. Nahau zote zilizotafsiriwa kwa mkakati huu zilihamisha maana ya MC kwa njia wasilifu.

Kuna nahau ambazo zilitafsiriwa kwa mkakati wa kutafsiri nahau kwa nahau zenye usawa wa kimaana na kileksia. Nahau ambazo zilitafsiriwa kwa mkakati huu hazikuwa nyingi. Nahau ambazo zilitafsiriwa kwa mkakati huu zilihamisha ujumbe kwa njia wazi. Hata hivyo, kuna tafsiri ambazo zilipunguza ujumbe wa MC kwa kiasi fulani. Ilibainika kuwa hakuna nahau ambayo haikutafsiriwa. yaani nahau zote zilitafsiriwa.

Katika kutathmini mikakati iliyotumiwa kutafsiri tashbihi, ilibainika kuwa tashbihi nyingi zilitafsiriwa kwa kuzihifadhi. Baadhi ya tashbihi zilizotafsiriwa kwa mkakati huu zilihamisha ujumbe wa MC kwa walengwa ingawa kuna zile ambazo zilitatiza uwasilishaji wa ujumbe. Kuna tashbihi ambazo zilitafsiriwa kwa dhana. Tafsiri zilizofanywa kwa mkakati huu zilihamisha ujumbe kwa njia wazi isiyotatiza ujumbe. Aidha, tashbihi zilizotafsiriwa kwa mkakati ziliweza kuhifadhi sifa za kifasihi. Tashbihi ambazo zilitafsiriwa kwa istiari ziliwasilisha ujumbe wa MC kwa ML. Tafsiri za kiistri pia ziliipa matini tafsiri sifa za kisanaa. Katika tafsiri za tashbihi kwa tashbihi yenyе maana sawa katika LL, ilibainika kuwa tashbihi zilizotafsiriwa kupertia mkakati huu ziliwasilisha ujumbe kwa njia wazi isiyotatiza mawasiliano.Tashbihi zilizotafsiriwa kupertia mkakati huu hazikuwa nyingi. Ilibainika pia kuwa hakuna tashbihi ambayo haikutafsiriwa.

Katika uchunguzi wa mikakati ya kutafsiri iliyotumika kutafsiri istiari, ilibainika kuwa mkakati wa kiufafanuzi ulitumika kwa kiwango kikubwa. Istiari ambazo zilitafsiriwa kwa mkakati huu ziliwasilisha maana ya MC kwa njia wazi. Hata hivyo baadhi ya tafsiri hizi zilipoteza sifa za kifasihi. Baadhi ya istiari zilitafsiriwa kwa mkakati wa kuhifadhi istiari. Tafsiri ambazo zilifanywa kupertia mkakati huu vile vile

zilihamisha ujumbe wa MC kwa njia isiyopotosha maana. Kuna istiari ambazo zilitafsiriwa kwa istiari yenyeye maana sawa. Tafsiri ambazo zilifanywa kwa mkakati huu zilihamisha ujumbe wa MC bila kuutatiza. Ilibainika pia kuwa istiari ambazo zilitafsiriwa kwa kisawe cha tashbihi ziliwasilsha ujumbe wa MC kwa njia wasilifu. Istiari moja ilihamishwa bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Ingawa maana ya istiari hii haifahamiki, athari yake kwa walengwa ni sawa na ile iliyokuwa nayo kwa wasomaji wa MC.

**SURA YA TANO**  
**MIKAKATI YA KUTAFSIRI NOMINO ZA PEKEE KATIKA MUSA**  
***MASHAKANI NA MUSA NA PEPO***

**5.1 Mkakati wa Kuhamisha Jina Moja kwa Moja**

Mkakati huu hutumiwa pale ambapo inakisiwa kuwa majina hayo hayadokezi maana yoyote katika matini (Newmark, 1988). Hivyo mkakati huu haufai pale ambapo maana inayodokezwa na majina haya ni muhimu. Katika tafsiri za Matundura (2013), *Musa Mashakani na Musa na Pepo*, NP nyingi zinazowakilisha majina ya watu zilihamishwa kwa kuzingatia mkakati huu. Kwa kuwa watusi binadamu wote ni wale wale katika matini mbili tunazotumia, majina yametajwa tu bila kutaja jina hilo linapatikana katika matini ipi. Katika matini za Kiingereza, majina kama Mukibi, Karanja, King Kong, Gekonyo, Nagendo, Rukia, Lutu, Namukasa, Bakole, Bilha, Joe, Okot, Sempa, Muwanga, Husseini, Sebastian Mulutu, Kigali, Mutagubya, nk ni baadhi ya majina yaliyotumiwa. Katika matini za Kiswahili majina haya ni yale yale; hayakufanyiwa mabadiliko yoyote. Newmark (1988) anasema kwamba mtafsiri anaweza kufanya hivi makusudi ili kuhifadhi uraia. Aidha, majina haya hayaashirii maana yoyote kimuktadha na kwa hivyo uhamishaji wa namna hii umewezesha uhamishaji wa ujumbe wa MC kwa ML.

**5.2 Mkakati wa Kulitoho Jina**

Jina linaweza kutoholewa ili kulingana na matamshi au maandishi ya LL. Katika tafsiri za Matundura (2013), ni majina machache yaliyotafsiriwa kwa mkakati huu. Jina Moses limetafsiriwa kuwa *Musa* nalo jina *America* likatfsiriwa kuwa *Marekani*. Tafsiri hizi zimeziwezesha ML kuonekana kuwa kazi asilia kwa kuzuia ugeni hivyo kumwezesha mtafsiri kuhamisha ujumbe linganifu kutoka MC` hadi ML kwa njia isiyotatiza uwasilishaji wa ujumbe.

**5.3 Mkakati wa Mwatiko wa Utamaduni**

Majina ya LC yanabadilishwa kwa majina ya kiasili ya LL ambayo maana yake ya moja kwa moja ni tofauti lakini yanadokeza maana zinazolingana kitamaduni. Kwa mfano NP *Itchy Fingers* ingetafsiriwa kama *Vidole Vinavyowasha* katika matini tafsiri. Hata hivyo badala ya *Vidole Vinavyowasha* mtafsiri amemwita Mikono

Mirefu. Maana za *Itchy Fingers* na *Mikono Mirefu* ni tofauti sana ikiwa maana ya moja kwa moja itazingatiwa. Barbara Kimenye aliye mtunzi wa MC amearifu kuwa kijana huyu alipewa jina *Itchy Fingers* kutokana na hulka yake isiyodhibitika ya kuiba vitu vya wenzake. Kwa hivyo *Vidole Vinavyowasha* ingechukuliwa kuwa tafsiri ya *Itchy Fingers* basi tafsiri hii ingepotosha maana ya MC kwa kupoteza ile dhana ya tabia ya wizi iliyodokezwa katika MC na hivyo ulinganifu wa maana usingepatikana.

Anasema:

Katika hafla moja ambapo baadhi yetu wanafunzi tulipelekwa kuzuru makao ya wanyama yatima mjini Entebbe, *alirudi shulen i akiwa na mwana wa mamba mfukoni*.

(*Musa na Pepo*, uk. 12).

Katika lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo LL, mtu mwenye tabia ya wizi husemwa kuwa na mikono mirefu. Jina *Mikono Mirefu* basi linafaa sana kama tafsiri ya *Itchy Fingers* kwa kuwa linabeba maana maalum kimuktadha. Kwa hivyo maana potovu ingehamishwa iwapo jina hili lilitafsiriwa moja kwa moja pasipo kuzingatia muktadha.

#### 5.4 Mikakati Mingine

Mtafsiri anaweza kutumia mikakati yoyote ya kutafsiri bora imfae katika kuhamisha ujumbe wa MC kwa ML. Katika kutafsiri majina ya mahali, mikakati mbalimbali imetumiwa kimwingiliano. Katika matini zote, matukio hutendeka katika shule inayoitwa *Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen*. Kwa kuwa matukio mengi hutendeka katika taasisi hii mahali hapa pamerejelewa mara nyingi katika matini. Aidha, majina mbalimbali yametumika katika MC kumaanisha mahali pale. Yafuatayo ni baadhi ya majina ambayo yametumiwa na Kimenye (1968) katika matini zote kurejelea taasisi hii:

- i. Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen
- ii. Mukibi's Educational Institute
- iii. Mukibi's

Jina *Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen* limetumika mara tano katika matini ya *Moses and the Ghost* (uk. 1, 18, 38, 55 na 62), na mara nne

katika *Moses in Trouble* (uk. 1, 9, 43 na 63). Katika matini tafsiri, mtafsiri ametumia mkakati uliopendekezwa na Hervey na Higgins (1992) wa kulihamisha jina moja kwa moja bila kulifanyia marekebisho yoyote. Tofauti ya jina hilo katika matini tafsiri na MC ni kwamba limeandikwa kwa herufi za mlazo (*Mukibi's Educational Institute for Sons of African Gentlemen*). Kama jina hili lilitafsiriwa lingekuwa: *Taasisi ya Elimu ya Mukibi kwa Watoto wa Kiume wa Wangwana wa Kiafrika*. Tafsiri hii ingekosa uasilia. Vile vile ingepoteza ladha ya kisanaa. Kulihamisha jina hili bila kulifanyia marekebisho kumewezesha mtafsiri kuwasilisha ujumbe wa MC kwa walengwa bila utata unaochosha akili ya msomaji wa ML. Kulingana na Venuti (1998), tafsiri ya kifasihi haipaswi kuonekana kama tafsiri bali kama kazi asilia kwa kuwa kutafsiri kazi ya kifasihi ni sawa na kuiandika upya. Kulihamisha jina hili bila mabadiliko kumesaidia katika kuibua athari sawa kwa walengwa kama ilivyokuwa kwa wasomaji wa MC.

Jina *Mukibi's Educational Institute*, limetafsiriwa kwa njia mbili:

- i. Jina hili limehamishwa kwa tafsiri sisisi ambapo limetafsiriwa kuwa *Taasisi ya Elimu ya Mukibi (Moses and the Ghost*, uk 2, *Musa na Pepo* uk. Tafsiri hii imehamisha ujumbe linganifu wa MC kwa ML kwa njia inayoleweka kwa urahisi bila utata wowote.
- ii. Mkakati mwingine ambao umetumiwa ni ule wa kulihamisha jina kama lilivyo bila kulibadilisha kwa vyovyote. Hata hivyo mtafsiri ametumia ubunifu wake akaongezea mkakati wa kuliandika jina hilo kwa herufi za mlazo kuwa *Mukibi's Educational Institute. (Moses and the Ghost* uk. 39, *Musa na Pepo* uk. 39). Kwa kutumia mkakati huu, ujumbe wa MC umewasilishwa kwa ML kwa njia wasilifu isiyopotosha maana.

Mtafsiri amelihamisha jina *Mukibi's* kwa namna sita:

- i. Taasisi ya Mukibi.

Kwa mfano:

Can anybody recall how many years Mukibi's has been here?

(*Moses and the Ghost*, uk. 6).

Kunaye anaweza kukumbuka *Taasisi ya Mukibi* imekuwepo hapa kwa miaka mingapi?

(*Musa na Pepo*, uk. 6).

For the first time in my life at *Mukibi*'s, I welcomed the bell and was up, washing and dressing while the others were still struggling to open their eyes. (*Moses and the Ghost*, uk. 44).

Kwa mara ya kwanza kabisa katika *Taasisi ya Mukibi*, nilifurahia sana kengele hiyo. Niliamka mara moja, nikaoga na kuanza kuvalia nguo wakati wengine bado walikuwa waking'ang'ana kufumbua macho yao.  
(*Musa na Pepo*, uk. 44).

As soon as they heard that Itchy Fingers had recognized him as one of the people interested in buying *Mukibi*'s, they instantly brightened.  
(*Moses and the Ghost* uk. 54).

Punde tu waliposikia kwamba Mikono Mirefu alikuwa amemtambua kuwa mmoja kati ya watu wale walionuia kununua *Taasisi ya Mukibi*, walichangamka mara moja.  
(*Musa na Pepo*, uk. 54).

Katika tafsiri hizi tatu, jina *Mukibi*'s lingetafsiriwa kama *Kwa Mukibi*. Hata hivyo, tafsiri hii isingefaa kwa kuwa ingekuwa potovu. Ingekuwa tatanishi kwa kuwa *Kwa Mukibi* kunaweza pia kumaanisha mahali anapoishi au anapomiliki *Mukibi*. Utata huu ulizuiliwa na mtafsiri kwa kulitafsiri jina hili kuwa *Taasisi ya Mukibi*.

## ii. *Mukibi*'s

Kwa mfano:

The shutters of a window (there are no glass panes at *Mukibi*'s except in the headmasters own house) were thrown wide open, ...

(*Moses and the Ghost*, uk. 14).

Madirisha ya mbao (hakuna vioo kwenye madirisha ya *Mukibi*'s isipokuwa katika nyumba ya mwalimu mkuu mwenyewe) yalikuwa wazi.  
(*Musa na Pepo*, uk. 15).

Tafsiri hii haijaathiri maana bali imehamisha ujumbe wa MC kwa ML bila utatanishi.

iii. Shule ya Mukibi

Kwa mfano:

Mr Burega was noted for his bad memory. Once during my second term at *Mukibi's*, he forgot where he had put his graduated tax ticket, (*Moses in Trouble*, uk. 51).

Bw Berega alifahamika kwa usahafulifu. Wakati mmoja, katika muhula wangu wa pili katika *Shule ya Mukibi*, alisahau mahali alipokuwa ameiweka tiketi yake ya ushuru. (*Musa Mashakani*, uk. 52)

Katika sehemu hii, mtafsiri ameiweka maana wazi kwa kutafsiri Mukibi's kama *Shule ya Mukibi* kwa kuwa Mukibi's inamaanisha mahali wanaposomea wale watoto. Kwa kufanya hivi mtafsiri ameweza kuwasilisha ujumbe linganifu kwa ML.

iv. Kwa Mukibi

Kwa mfano:

And before we reach *Mukibi's*, Itchy Fingers, you'd better say how much you're Giving Holy Moses and me for walking all this way with you. (*Moses and the Ghost*, uk 48).

Na kabla hatujafika *kwa Mukibi* ni vyema Mikono Mirefu useme utatupa mimi na Musa Mtakatifu pesa ngapi kwa kutembea masafa haya yote kukusindikiza.

(*Musa na Pepo*, uk 48).

Tafsiri hii ni tafsiri sisisi ambayo imetatiza uwasilishaji wa maana ya MC kwa ML. *Kwa Mukibi* inamaanisha anapoishi Mukibi au panapomilikiwa na Mukibi. Maana ya MC ni mahali pale wanaposomea Musa na wenzake wala haimaanishi kitu kingine chochote kile.

v. Taasisi ya Elimu ya Mukibi

Kwa mfano:

We couldn't imagine being separated and sent to study with so-called

respectable students who had never known what it is like to be expelled from other places, and, let's face it, *Mukibi*'s specializes in such cases. (*Moses and the Ghost*, uk. 38).

Ilikuwa vigumu kwetu kuwazia kutenganishwa na kupelekwa kusoma pamoja na wanafunzi wanaodaiwa kuwa watifu na ambao hawajui ni nini maana ya kutimuliwa kutoka shule nyingine. Ukweli ni kwamba, *Taasisi ya Elimu ya Mukibi* ndiyo kitovu cha wanafunzi wa sampuli yetu! (*Musa na Pepo*, uk 38)

Jina *Mukibi*'s katika MC linadokeza tu jina la mahali walipokuwa wakisomea Moses na wenzake. Mahali pale ndipo *Taasisi ya Elimu ya Mukibi* na kwa hivyo tafsiri hii imehakikisha ulinganifu kati ya MC na ML.

vi.        **Mukibi**

Kwa mfano:

Everybody cheered, and he added, "so we'll be on our own again, and we will pull together to make *Mukibi*'s a school to be proud off!"

(*Moses and the Ghost*, uk 90)

Kila mtu aliangalia, na akaongeza, "Kwa hivyo tutakuwa peke yetu tena, na tutashirikiana kuifanya *Mukibi* kuwa shule ya kuonewa fahari!"

(*Musa na Pepo*, uk 90).

Katika tafsiri hii kiwakilishi **I** katika neno kuifanya pamoja na maneno *kuwa shule* yametumiwa makusudi ili kuondoa utata wa kimaana ambao ungekuwepo kama hayakutumiwa. Kutokana na matumizi haya kinachodokezwa kinaeleweka moja kwa moja na hivyo kuonyesha kuwa tafsiri imefaulu katika kuhamisha ujumbe linganifu.

Baadhi ya nomino zimetafsiriwa kwa kutumia mkakati wa kutafsiri neno kwa neno uliopendekezwa na Newmark (1988). Ifuatayo ni mifano ya nomino hizo pamoja na tafsiri zao:

- i.        Tafsiri za matini mbili zinazohusika: *Moses ni Trouble*  
Kuwa *Musa Mashakani* na *Moses and the Ghost* kuwa  
*Musa na Pepo*.

- ii. Minister for Education (*Moses in Trouble*, uk.1)  
Wizara ya Elimu. (*Musa Mashakani*, uk.1)

Tafsiri hii ni potovu kwa kuwa *Wizara ya Elimu* kwa Kiingereza ni *Ministry of Education*. Tafsiri sahihi ingekuwa *Waziri wa Elimu*. Jina lili hili limetafsiriwa kama Wizara ya Elimu katika (*Musa Mashakani*, uk. 3).

- iii. On the one occasion that a group of us were taken to the *Animal Orphanage at Entebbe* he arrived back to school with A baby crocodile in his pocket.  
(*Moses and the Ghost*, uk. 11).

Katika hafla moja ambapo baadhi yetu wanafunzi tulipelekwa kuzuru “*makao ya wanyama yatima mjini Entebbe*”, alirudi shuleni akiwa na mwana wa mamba mfukoni.  
(*Musa na Pepo*, uk. 12).

- iv. They turned into *Sneaker’s Path* as casually as if walking into their own shambas’ and from there took the main road.  
(*Moses and the Ghost*, uk. 63)

Walishika *Ujia wa Wahepaji* kana kwamba walitembea kwenye mashamba yao, na kutoka hapo wakafuata barabara kuu. (*Musa na Pepo* uk. 63).

- v. Katika matini zote jina *Holy Moses* limetafsiriwa kuwa *Musa Mtakatifu*.

Katika tafsiri hizi mtafsiri amefaulu kuhamisha maana ya MC kwa ML kwa njia inayoeleweka kwa urahisi. “*Animal Orphanage*” ni mahali wanapotunziwa wanyama walio mayatima. Kwa hivyo kutafsiri *Animal orphanage at Entebbe* kuwa *makao ya wanyama yatima mjini Entebbe* ni tafsiri iliyofaulu kuhamisha ujumbe usio na kasoro. Kutafsiri *Sneaker’s Path* kuwa *Ujia wa Wahepaji* pia kumemwesha mtafsiri

kuhamisha ujumbe wa MC kwa njia isiyotatiza msomaji wa ML. *Holy Moses* lilikuwa jina la utani alilobandikwa Moses alipojiunga na *Taasisi ya Elimu ya Mukibi*. Jina *holy* lina maana sawa na *takatifu*. *Musa Mtakatifu* ni tafsiri inayowasilisha maana linganifu na *Holy Moses* katika MC.

Baadhi ya NP zimetafsiriwa kwa dhana ili kuweza kuwasilisha ujumbe linganifu kwa ML. Ifuatayo ni mifano ya tafsiri za NP kwa dhana:

OK, *Mother Cook!* I yelled at Gekonyo, and King Kong and I sullenly turned back to our own dormitory.

*(Moses in Trouble, uk 8)*

Ni sawa, *Mpishi Mkuu!* Nikamjibu Gekonyo kwa sauti ya juu, kisha mimi na King Kong tukarudi katika bweni letu tukiwa na hasira nyingi.

Kusudi la Musa kumwita Gekonyo *Mother Cook* lilikuwa ni kumkejeli kwa kumbandika jina ambalo linamchora kuwa mpishi bora kuliko wote ingawa chakula alichopika yeze pamoja na wenzake wa Dorm 1 kilionja vibaya sana. Kwa hivyo ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu mtafsiri alitafsiri nomino, *Mother Cook* kwa dhana *Mpishi Mkuu* kwa kuwa jina hili ni kinaya kwa mtu anayepika chakula kisicholika.

Mr Karanja called on the *Almighty* with a fervour which astonished us,  
*(Moses and the Ghost, uk 83)*

Tafsiri:

Bw Karanja aliita jina la *Mwenyezi Mungu* kwa hamasa, jambo lililotushangaza sana. *(Musa na Pepo, uk 83)*.

Jina *Almighty* lina maana ya *mwenye nguvu zote*. Hata hivyo, tafsiri hii mbali na kupoteza maana aliyokusudia mwandishi ingeupoteza ule mnato wa kisanaa na kuifanya kazi isionekane kama kazi kifasihi. Ili kupata ulinganifu kati ya MC na ML, tafsiri *Mwenyezi Mungu* imewasilisha maana iliyo wazi na isiyotatiza ya nomino *Almighty*.

Newmark (1988) amependekeza mkakati wa kulihamisha jina la kwanza moja kwa moja ikiwa halidokezi maana yoyote. Katika matini tulizozingatia katika utafiti huu, majina mengi hayadokezi maana yoyote. Kwa mfano, jina *Mukibi* halidokezi maana

yoyote muhimu katika matini hizi. Hata hivyo, jina *Old Mukibi*, neno *Old* linaashiria dhana ya *umri mkubwa*, yaani mtu aliyeishi kwa miaka mungi. Hii ndiyo sababu ili kuafikia ulinganifu wa maana, jina *Old Mukibi* limetafsiriwa kuwa *Mzee Mukibi*. Mara kadhaa katika kulihamisha jina *Kigali* ambaye alikuwa bawabu wa shule *jina Mzee* limeongezwa ingawa haliko katika MC. Taswira tunayoipata katika MC kuhusu bawabu Kigali ni kwamba alikuwa na umri mkubwa sana. Kwa hivyo, kuongeza jina *Mzee* kwa jina Kigali katika ML kulinua kuwasilisha dhana ya umri wa Kigali, ujumbe ambao ungepotea ikiwa neno mzee halikutumiwa.

## 5.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia mikakati ya kutafsiri nomino za pekee. Katika tathmini ya mikakati iliyotumiwa kutafsiri nomino za pekee, utafiti huu ulibainisha kuwa karibu majina yote ya watu isipokuwa mawili tu (Musa Mtakatifu na Mikono Mirefu) yamehamishwa moja kwa moja bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Majina mawili (Musa na Marekani) yametoholewa ili kulingana na matamshi ya LL. Jina moja tu (Mikono Mirefu) ndilo lililotafsiriwa kwa mwatiko wa utamaduni. Nomino mbili zimetafsiriwa kwa dhana; *mother cook* limetafsiriwa kuwa *mpishi mkuu* nalo jina Almighty likahamishwa kama Mungu Mwenyezi. Nomino tatu zimetafsiriwa kwa mkakati wa tafsiri ya moja kwa moja. Nomino hizi ni *makao ya wanyama yatima mjini Entebbe, Taasisi ya Elimu ya Mukibi na Ujia wa Wahepaji*.

Kuna majina matatu ambayo yametumiwa kurejelea taasisi waliyokuwa wakisomea Musa na wenzake na majina haya yametafsiriwa kwa njia mbalimbali. Jina Mukibi's Educational Institute for the Sons of African Gentlemen lilihamishwa kama liliyvo bila kufanyiwa mabadiliko yoyote lakini likaandikwa kwa herufi za mlazo (*Mukibi's Educational Institute for the sons of African Gettlemen*). Jina Mukibi's Educational Institute limetafsiriwa kwa njia mbili; Taasisi ya Elimu ya Mukibi na kwingineko jina hili limehamishwa bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Mtafsiri ameliandika kwa herufi za mlazo. Jina Mukibi's kumaanisha ile taasisi limetafsiriwa kwa namna sita; kama Taasisi ya Mukibi, Mukibi's, Shule ya Mukibi, Kwa Mukibi, Mukibi na Taasisi ya Elimu ya Mukibi.

## **SURA YA SITA**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha mikakati aliyotumia Matundura (2013) kutafsiri TU na NP ili kupata tafsiri linganifu. Katika kuchunguza tafsiri za TU, mikakati iliyotumiwa kutafsiri istiari, tashbihi na nahau ilichunguzwa ili kubainisha mikakati ambayo inafaa zaidi katika kuhamisha TU ili kuwasilisha ujumbe linganifu. Mikakati ambayo ilitumiwa kutafsiri NP pia ilichunguzwa. Aidha, ufaafu wa mikakati hiyo ulichunguzwa.

Uchunguzi huu ulibainisha kuwa hakuna mkakati mmoja ambao unatosha kutafsiri kila aina ya tamathali. Mseto wa mikakati ya kutafsiri inafaa kutumiwa ili kuweza kuhamisha ujumbe linganifu. Hii ni kwa sababu maana za tamathali za usemi hutegemea muktadha. Hivyo basi mkakati unaotumiwa unategemea maana katika muktadha husika. Uchunguzi pia uligundua kuwa mikakati mwafaka ya kutafsiri tamathali za usemi inabadilika kutoka aina moja ya tamathali hadi nyingine. Hata hivyo, mkakati wa kiufafanuzi unatumika katika kutafsiri aina mbalimbali za TU. Tulibainisha pia kuwa ubunifu wa mtafsiri una mchango wake katika kuhamisha ujumbe linganifu.

Katika tathmini ya mikakati ya kutafsiri NP, ilibainika kuwa mikakati inayotumika katika kutafsiri NP inategemea nomino ya pekee inayohusika na mchango wa nomino hiyo ya pekee katika matini.

#### **6.2 Hitimisho**

Baada ya kufanya uchunguzi huu, tulibainisha kuwa kutafsiri matini za kifasihi hakuhitaji tu ujuzi wa lugha zinazohusika bali pia ufundi na ujuzi wa kisanaa. Ingawa kuna mikakati ambayo inatumika sana kutafsiri tamathali za aina fulani, hakuna mkakati mmoja ambao umetosha kutafsiri TU kwa kuwa mikakati ya kutafsiri hutumiwa kimwingiliano. Kuna mikakati ambayo hutafsiri matini katika kiwango cha neno na mingine katika kiwango cha kimuktadha. Mtafsiri kwa hivyo hulazimika kuteua mikakati inayomwezesha kuhamisha ujumbe linganifu kati ya MC na ML.

Tuligundua kwamba kutafsiri NP katika kazi za kisanaa pia kunamhitaji mtafsiri kutambua mchango wa kila nomino ya pekee katika matini. Utambuzi huu ndio unaomsaidia kuamua mikakati mwafaka ya kutafsiri kila NP ili aweze kupitisha ujumbe linganifu kwa walengwa. Kama ilivyo katika kutafsiri TU mikakati ya kutafsiri NP hutumika kimseto kwa kuwa hakuna mkakati wowote ambao umetosha kutafsiri kila NP.

Kwa jumla hata kama makosa madogomadogo yalitokea katika mchakato wa kutafsiri TU na NP, makosa haya hayakutatiza uhamishaji wa ujumbe na kwa vyovytile tafsiri ilifanikiwa kuwasilisha ujumbe wa MC kwa ML. Mikakati ya kutafsiri iliyotumiwa kutafsiri NP na ile iliyotumiwa kutafsiri TU imemwezesha mtafsiri kuwasilisha ujumbe wa MC kwa walengwa bila kutatizika.

### **6.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi**

Utafiti huu ulichunguza mikakati ya kutafsiri TU na NP. Mbali na TU na NP, kazi za kifasihi hushughulikia mambo mengi ikiwemo mtindo wa mwandishi na mbinu za uandishi. Tunapendekeza uchunguzi zaidi kufanywa ili kubainisha nafasi ya ubunifu wa mtafsiri katika kuhamisha mtindo wa mwandishi ili kuafikia ulinganifu wa maana kati ya MC na ML. Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kubainisha mikakati ya kutafsiri mbinu za uandishi katika ushairi kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili ili kuafikia ulinganifu wa maana.

TU katika kazi za fasihi ni nyingi mno ikilinganishwa na tatu tu (istiari, nahau na tashbihi) zilizochanganuliwa katika utafiti huu. Uchunguzi zaidi unaweza kufanywa kuhusu namna ya kutafsiri tamathali nyinginezo za usemi kama vile uhuishi, chuku na taswira. Tunapendekeza pia utafiti zaidi kufanywa ili kubainisha uhusiano baina ya mikakati ya kutafsiri TU katika tanzu mbalimbali za fasihi.

## MAREJELEO

- Albert, S. H. (2010). *Oxford Advanced Learners Dictionary*. England: Oxford.
- Ali, C. (1981). *Problems of Translating from English to Kiswahili: Voice of Kenya Broadcasting*. Nairobi: Unpublished M A Theses.University of Nairobi. Nairobi:
- As-Safi, A. (2010). *Translation Theories, Strategies And Basic Theoretical Issues*. Jordan: Petra University.
- Baker, M. (1992). *In Other Words: A Course Book on Translation*. London: Routledge.
- Baker, M. (2005). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. London: Routledge.
- BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.
- Barnwell, K. (1986). *Bible Translation: An Introductory Course in Translation Principles*. Dallas: Summer Institute of Linguistics.
- Bassnett, S. (1988). *Translation Studies (3rd Ed)*. London: Routledge.
- Bell, R. (1991). *Translation and Translating*. London: Longman Group UK Ltd.
- Belloc, H. (1931). *On Translation*. Oxford: Oxford University Press.
- Broeck, R. (1978). The Concept of Translation in Translation Theory. Some Critical Reflections. In J. Holmes, J. Lambert, & R. Broeck, *Literature and Translation*. Leuven: Academics.
- Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.
- Culler, J. (1976). *Structuralist Poetics: Structuralism, Linguistics and the Study of Literature*. London: Oxford University Press.
- Dayan, L. (2012). Dynamic Equivalence and Formal Correspondence in Translation Between Chinese and English. *International Journal of Humanities and Social Science*, 79-86.
- Gaddis, M. (1981). *Translation Spectrum Essays in Theory and Practice*. Albany: State University of New York Press.
- Gutt, E. (1999). *Translation and Relevance: Cognition and Context*. Oxford: Basil Blackwell Publications.
- Hervey, S. and Higgins, I. (1992). *Thinking Translation*. London: Routledge.

- House, J. (1977). *Translation Quality Assessment: A Model Revisited*. Tübingen. Tübingen: Gunter Narr.
- Hugh, H. (1977). *A Handbook to Literature*, The Odyssey Press, Indianapolis
- Jakobson, R. (2000). On Linguistic Aspects of Translation. In . London: Routledge. In L. Venuti, *The Translation Studies Reader*. London: Routledge.
- Kimenye, B. (1968). *Moses and The Ghost*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kimenye, B. (1968). *Moses in Trouble*. Nairobi: Oxford University Press.
- Koller, W. (1989). *Equivalence in Translation Theory*. In Chesterman: Ed Op. Cit.
- Krings, H. (1986). Translation Problems and Translation Strategies of Advanced German Learners of French. In J. House, & S. Blum-Kulka, *Interlingual and Intercultural Communications*. Tübingen: Gunter Narr.
- Larson, M. (1984). *Meaning-based Translation: A Guide to Cross-Language Equivalence*. New York: University Press of America.
- Larson, M. (2001). *Meaning-based Translation*. New York: University Press of America.
- Leppihalme, R. (1997). *Culture Bumps: An empirical Approach to The Translation of Allusions*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Loescher, W. (1991). *Translation Performance, Translation Process and translation Strategies*. Tuebingen: Guten Narr.
- Lyons, I. (1977). *Semantics*, Vol. 1, Cambridge University Press: Cambridge.
- Mahmoud, O. (2007). *Translation Procedures, Strategies and Methods*. (Translational Journal, Ed.) Retrieved 7, 17, 2018, from Cultural Aspects of Translation: <http://translationjournal.net/journal/4/culture>
- Matundura, B. (2013). *Musa Mashakani*. Nairobi: Oxford University Press.
- Matundura, B. (2013). *Musa na Pepo*. Nairobi: Oxford University Press.
- Miremadi, S. (1991). *Theories of Translation and Interpretation*. Tehran: SAMT.
- Mollanazar, H. (2001). *Naturalness in The Translation of Novels from English to Persian*. London: University of Warwick Centre for British and Comparative Cultural Studies.
- Muirgai, M. (2005). *Ubunifu wa Mtafsiri*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: Haijachapishwa.

- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and applications*. London and New York: Routledge.
- Mutahi, K. (1987). Translation Problems in Oral Literature. *Linguistic Conference of S.A.D.C.C. Universities* (pp. 110-116). Harare: LASU.
- Namulungu, R. (1999). *Ukiushi Katika Tafsiri*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret: Haijachapishwa.
- Newmark, P. (1981) *Approaches to Translation*. Oxford: Pergamon Press
- Newmark, P. (1982). *Approaches to Translation*. Oxford: Pergamon Press.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. New York: Prentice Hal.
- Newmark, P. (2001). *Approaches to Translation*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Education Press.
- Nida, E., & Taber, C. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E. J. Brill, for the United Bible Society.
- Nida, E. (1943). *Towards a Science of Translation, with Special Reference to Principles and Procedures involved in Bible Translating*. Leiden: E. J. Brill, for the United Bible Society.
- Nida, E. (1964). *Toward a Science of Translating*. Leiden: E. J. Brill, for the United Bible Society.
- Nyangeri, N. (2014). *Vitendo Usemi na Ulinganifu wa Maana katika Tafsiri: Mifano Kutoka Kazi Mbili Teule za Barbara Kimenye*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: Haijachapishwa.
- Nzyoka, S. (2014). *Tathmini ya Tafsiri na Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi Katika Tamthilia ya Antigoni*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: Haijachapishwa.
- Oduma, R. (2006). *Phonological Adaptation of Loanwords in Ateso*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi: Unpublished.
- Omboga, Z. (1986). *Fasihi Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili. Matatizo na Athari Zake*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: Haijachapishwa.
- Omboga, Z. (2006). *Sitting Text, Culture and Pedagogy in Literal Translation: A Theorisation of Translation in Culture Transfer with Examples from selected Texts in Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: Haijachapishwa.
- Ondara, K. (2010). *Ufaafu wa Maana Katika Tafsiri ya Nyimbo Dini*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: Haijachapisha.

- Pierini, P. (2007). *Simile in English: From Description to Translation*. CIRCULO de Linguistica Aplicada a la Comunicacion (clac).
- Pym, A. (2010). *Translation and Text Transfer: An Essay on the Principles of Intercultural Communication*. Intercultural Studies Group, Tarragona.
- Shitemi, N. (1990). *Mawasiliano Katika Tafsiri: Uteuzi wa Mtafsiri*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi: Haijachapishwa.
- Snell-Hornby, M. (1988). *Translation Studies: An Integrated Approach*. Philadelphia: John Benjamin's Publishing Company.
- Toury, G. (1995). *Descriptive Translation Studies and Beyond*. Amsterdam: Benjamins Library.
- TUKI, (2010), *English – Swahili Dictionary*. Dar- Salaam: TUKI.
- TUKI, (2004), *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Tytler, A. (1797). Essay on the Principles of Translation. In D. Robinson (Ed.), *Translation*. Edinburgh: Cadell and Davies.
- Venuti, L. (1995). *The Translator's Invisibility: A History of Translation*. London and New York: Routledge.
- Venuti, L. (1998). Strategies of Translation. In M. Baker (Ed.), *Encyclopedia of Translation Studies*. London and New York: Routledge.
- Vinay, J. and Darbelnet, J. (1995). *Comparative Stylistics of French and English: a Methodology for Translation*. (J. Sager, & Hamel, Trans.) Amsterdam / Philadelphia: Benjamins.
- Wangia, J. (2003). *Aspects of Mistranslation in the 1951 Lulogooli Bible*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Williams, D. (2005). *The Belief Systems of Cultural Brokers in Three Minority Communities in America*. Indiana University of Pennysylvania. Indiana: unpublished.
- Wills, W. (1983). Decision Making in Translation. In B. Mona, *a Course Book on Translation*. London: Routledge.
- Xiang, Y. (2011). *Dynamic Equivalence: Features and Merits. Theory and Practice in Language Studies*. Chongqing Jiaotong University, School of Foreign Languages, Chongqing.
- Zhongde, L. (1991). *Ten Lectures on Literary Translation*. Beijing: China Translation and Publishing Corporation.

# KIAMBATISHO I BARUA YA IDHINI



## NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION

Telephone: +254-20-2213471,  
2241349,3310571,2219420  
Fax: +254-20-318245,318249  
Email: dg@nacosti.go.ke  
Website: www.nacosti.go.ke  
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kikuyu  
Off Waiyaki Way  
P.O. Box 30623-00100  
NAIROBI-KENYA

Ref. No NACOSTI/P/19/56899/27558

Date 15<sup>th</sup> January, 2019

Janerose Igoki Kamundi  
Chuka University,  
P. O. Box 109-60400  
**CHUKA.**

### RE: RESEARCH AUTHORIZATION

Following your application for authority to carry out research on "*Mikakati ya kuafikia ulinganifuwa maana katika tafsiri ya kifasihi: Tathmini ya tafsiri za kazini mbili teule za barbara kimene*" I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Tharaka-Nithi County** for the period ending **15<sup>th</sup> January, 2020**.

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Tharaka-Nithi County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

*G.Kalerwa*



**GODFREY P. KALERWA MSc. MBA MKIM**  
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner  
Tharaka-Nithi County.

The County Director of Education  
Tharaka-Nithi County.

## KIAMBATISHO II CHETI CHA IDHINI

<b>THIS IS TO CERTIFY THAT:</b> <b>MS. JANEROSE IGOKI KAMUNDI</b> <b>of CHUKA UNIVERSITY, 0-60400</b> <b>CHUKA, has been permitted to conduct</b> <b>research in Tharaka-Nithi County</b>	<b>Permit No : NACOSTI/P/19/56899/27558</b> <b>Date Of Issue : 15th January,2019</b> <b>Fee Recieved :Ksh 1000</b>
	
<b>on the topic: MIKAKATI YA KUAFIKIA ULINGANIFUWA MAANA KATIKA TAFSIRI YA KIFASIHII: TATHMINI YA TAFSIRI ZA KAZI MBILI TEULE ZA BARBARA KIMENYE</b>	
<b>for the period ending:</b> <b>15th January,2020</b>	
 <b>Applicant's Signature</b>	 <b>Director General</b> <b>National Commission for Science, Technology &amp; Innovation</b>

**KIAMBATISHO III  
IDADI YA MANENO**

Jumla ya maneno (kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya sita).....	28,856
Jumla ya kurasa (kutoka sura ya kwanza hadi sura ya sita).....	99